Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Hamsini na Nne – Tarehe 27 Agosti, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka 2006/2007 *(The Annual Report and Accounts of the Bank of Tanzania for the Year 2006/2007).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za *Twiga Bancorp* kwa mwaka wa fedha 2007 *(The Annual Report and Accounts of Twiga Bancorp for the Year 2007).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Benki ya Posta Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2007 *(The Annual Report and Accounts of the Tanzania Postal Bank for the Financial Year 2007).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Chuo cha Usimamizi wa Fedha kwa mwaka wa fedha 2006/2007 *(The Annual Report and Accounts of the Institute of Finance Management for the Financial Year 2006/2007).*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 37(4) naomba hati iliyowasilishwa ya taarifa ya mwaka na hesabu za Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka 2006/2007 *(The Annual Report and Accounts of the Bank of Tanzania for the year 2006/2007)* ijadiliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono, kwa wakati muafaka Spika atapanga wakati wa kujadili hoja hiyo lakini ikumbukwe pia na hoja ya kujadili *Accounts* za mwaka 2005/2006 bado ipo. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 477

### Uzingatiaji wa Kanuni za Afya

**MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza:-

Kwa kuwa takataka zimekuwa zikizagaa pembezoni mwa barabara za Jiji la Dar es Salaam kutokana na wananchi wengi kutokuwa na uelewa wa kuzingatia kununi bora za afya:-

(a) Je, ni hatua gani za kisheria zinazochukuliwa pale ambapo kanuni za afya zikiukwa?

(b) Serikali kwa kuendelea kulifumbia macho tatizo hilo, haioni kuwa kutasababisha kutumia fedha nyingi za kununulia dawa za kutibu na kuzuia magonjwa ya milipuko yanayotokana na uchafu yakiwemo ya kuhara na kipindupindu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, Kifungu 121 na 123, Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka ya Miji Namba 8 ya mwaka 1982 Kifungu cha 54A(g) na sheria ndogo zilizotungwa kuzuia uchafuzi wa mazingira, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Halmashauri za Manispaa za Ilala, Temeke na Kinondoni zimekuwa zikichukua hatua mbalimbali kudhibiti uchafuzi wa mazingira. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na ukaguzi wa maeneo mbalimbali yakiwemo maeneo ya biashara, makazi ya watu, maeneo ya wazi, barabara, mifereji na kuweka vibao vya Ilani. Pia kutoa onyo la mdomo na kutoa ilani kwa wanaokiuka Kanuni za afya na usafi wa mazingira na kuwafikisha katika vyombo vya sheria wale wanaoshindwa kutekeleza maagizo ya ilani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha mwezi Desemba, 2007 hadi Mei, 2008 jumla ya ilani 2,153 zilitolewa kwa wakiukaji wa kanuni za afya na usafi wa mazingira ambapo watu 387 waliokaidi kutekeleza maagizo ya ilani hizi walifikishwa Mahakamani. Aidha, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Manispaa zake tatu zimekuwa zikiendelea kuelimisha jamii juu ya usafi wa mazingira na uzingatiaji wa kanuni na sheria mbalimbali za afya na usafi wa mazingira. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijalifumbia macho suala la kuwachukulia hatua za kisheria wanaokiuka kanuni za afya. Serikali imeendelea kutumia vyombo vya sheria yakiwemo Mabaraza ya Kata katika kusimamia Sheria na Kanuni za Afya. Aidha, kwa Jiji la Dar es Salaam, Mahakama ya Jiji ndiyo inayoshughulikia maamuzi ya kesi mbalimbali zinazohusu ukiukwaji wa sheria na kanuni za afya. Kutokana na jitihada za Jiji la Dar es Salaam na Manispaa zake tatu katika kusimamia utekelezaji wa Kanuni na Sheria za Afya na Usafi wa Mazingira, milipuko ya magonjwa hasa ya kipindupindu imepungua kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, kwa mwaka 2006 kulikuwa na wagonjwa wa kipindupindu 11,249 na vifo 117. Mwaka 2007 wagonjwa wa kipindupindu walikuwa 374 na vifo vinne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu swali namba 437 la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, mnamo tarehe 21 agosti, 2008, Serikali inaendelea kutumia njia mbalimbali kuhakikisha kwamba suala la usafi wa miji yetu unazingatiwa. Njia hizi ni pamoja na kuwashirikisha wananchi na makampuni binafsi, vikundi vya kijamii, asasi za kiraia na wadau wengine wa maendeleo katika kuhakikisha kuwa Jiji, Miji na maeneo ya Makao Makuu ya Manispaa na Wilaya yanakuwa katika hali ya usafi wakati wote. *(Makofi)*

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tatizo hili la kukithiri kwa uchafu katika Jiji la Dar es Salaam limekuwa sugu na la muda mrefu hali ambayo inalishushia hadhi jiji hili je, Serikali iko tayari kutunga sheria kali ambayo itaweza kutoza kati ya shilingi 500,000/= na shilingi 1,000,000/= kwa makosa ya uchafuzi wa mazingira na utupaji wa taka ovyo na hasa kwa makondakta wa daladala ambao hutupa takataka na chupa za maji katikati ya barabara? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu anaonyesha jinsi ambavyo anajali kuhusu tatizo hili la uchafu katika maeneo yetu ya Jiji. Hatukatai kwa sababu kweli ni tatizo katika Miji. Miji mikubwa kama Beijing unapotaka kujenga mahali kwanza kabisa unapewa utaratibu wa kuhakikisha kwamba unasafisha eneo lako, unakuwa na mahali pa kupanda miti na utaratibu mwingine. Sasa anachozungumza Mbunge hapa ni kwamba tuweke utaratibu wa kutoka shilingi laki tano hadi milioni moja. Hili jambo linahusu mamlaka yenyewe inayohusika, wale Madiwani wa Jiji la Dar es Salaam wakiona kwamba ili tuondokane na tatizo hili tunahitaji kupitisha sheria ndogo ndogo ambayo

itatoza shilingi laki tano mpaka milioni moja basi watafanya hivyo kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja la nyongeza. Mbali na tatizo la wananchi kutupa taka ovyo ovyo lakini pia madampo ambayo yamewekwa na Halmashauri yenyewe nalo pia ni tatizo. Kwa kuwa Mkuu wa Mkoa ameshapata *feasibility study* inayoonyesha jinsi gani takataka zilizoko Dar es Salaam zinaweza kuzalisha umeme, je, Waziri anaweza akamuagiza Mkuu wa Mkoa kuitumia ile *study* aliyoipata kutoka Canada ambayo nilimkabidhi ifanyiwe kazi ili kuondokana na tatizo hili la takataka zilizo katika madampo ambazo zinasababisha uchafu pia? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed alimpelekea *feasibility study* Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam analifanyia kazi ili kuona kwamba takataka hizo tuweze kuzigeuza aidha, ziwe umeme au kuzalisha vitu vingine ambavyo vinaendana na utengenezaji wa takataka ngumu. Zoezi hilo limeshaanza na sisi wenyewe kwa kushirikiana na Jiji la Dar es Salaam tumeshaanza mchakato wa kuona ni vipi tunaweza kuzitumia hizo taka ngumu katika kugeuza aidha, umeme au vitu vingine vinavyoambatana na takataka ngumu. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa utaratibu unaotumika wa kukusanya taka kwenye makazi ya wananchi wa Dar es Salaam, magari ya taka kupita na kuchukua takataka haufahamiki au haupo wazi kwa wakazi wa Dar es Salaam, je, Halmashauri za Manispaa za Dar es Salaam pamoja na Jiji zitatoa taarifa rasmi kwa wakazi wa Dar es Salaam muda na siku za kukusanya takataka kwenye makazi ya watu ili wananchi wote waweze kufaidi utaratibu huo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu zote kuanzia kwenye Manispaa, Kata hadi kwenye Mitaa. Kwa hiyo, taratibu zipo, kwa mujibu wa taratibu hizo kila siku takataka zinatakiwa kukusanywa kwa sababu zinazalishwa kila siku na siyo kwa wiki au kwa mwezi. Kwa hiyo, ni wajibu wa kila Mtaa na Halmashauri kuhakikisha kwamba takataka zinakusanywa kila siku kwa kushirikisha vikundi mbalimbali na Manispaa zenyewe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ningewashauri mwende Accra, Ghana mkaone wanavyofanya. Kuna utaratibu mzuri kabisa wa kufanya usafi katika Miji. Tunaendelea na swali linalofuata. *(Makofi)*

Na. 478

**Matumizi ya Askari Mgambo Nchini**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni Jijini Dar es Salaam kulijitokeza hali ya mzozo kati ya mgambo na wafanyabiashara ndogo ndogo hasa katika maeneo ya Magomeni hali iliyosababisha uvunjifu wa amani:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani ili kuleta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo lililoleta hali mbaya nchini?

(b) Je, ni hasara kiasi gani ilipatikana kutokana na mzozo huo?

(c) Je, kisheria mipaka ya kikazi ya mgambo ni ipi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mnamo tarehe 4 Februari, 2008 katika eneo la Magomeni Jijini Dar es Salaam kulitokea vurugu kati ya askari mgambo wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni na wafanyabiashara ndogo ndogo (Wamachinga) wanaofanya biashara zao mikononi katika mitaa ya Magomeni Mapipa na Bonde la Jangwani. Vurugu hizo zilisababishwa na wafanyabiashara hao kuwafukuza askari mgambo wa Manispaa waliokuwa wanatekeleza majukumu yao ya kulinda na kuzuia biashara za mikononi katika eneo la barabarani (Magomeni) na Bonde la Jangwani ambayo hayaruhusiwi kufanyia biashara ndogo ndogo kwa mujibu wa sheria ndogo ndogo za Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, vurugu hizi zilitulizwa na Jeshi la Polisi kituo cha Magomeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiini cha vurugu hizo ni wafanyabiashara hao kufanya biashara katika maeneo yasiyoruhusiwa na pindi wanapozuiwa kufanya hivyo na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni wanadai hawatendewi haki. Aidha, wafanyabiashara ndogo ndogo hukaidi kuhamia maeneo yaliyotengwa na Manispaa kwa shughuli za biashara kama vile Tandale, Magomeni Sokoni, Manzese Urafiki, Kinondoni na Mabibo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya tukio hilo Serikali ilichukua hatua ili kuleta ufumbuzi wa tatizo hilo. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wafanyabiashara ndogo ndogo katika maeneo yaliyopimwa viwanja ishirini vya mradi katika Manispaa ya Kinondoni. Bado wafanyabiashara hao wanakaidi kwenda kwenye maeneo hayo kwa madai kuwa ni mbali hivyo kuendelea kuvunja sheria na kanuni zilizopo kwa kufanya biashara katika maeneo yasiyoruhusiwa. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hasara zilizotokana na vurugu hizo ni pamoja na askari mgambo tisa na wafanyabiashara watano kujeruhiwa kwa kupigwa mawe katika vurugu hizo tukio ambalo liliripotiwa katika kituo cha Polisi Magomeni na majeruhi

kupatiwa huduma katika Kituo cha Afya cha Magomeni. Pia kuvunjwa kwa vioo vya ofisi ya ulinzi ya Halmashauri na kuvunja vioo vya gari moja la Halmashauri na magari mawili ya wananchi yaliyokuwa yameegeshwa katika Kituo cha Afya Magomeni.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka ya kikazi ya askari mgambo wa Manispaa ipo kwa mujibu wa sheria ndogo ndogo za Halmashauri na Sheria Kuu zinazosimamia ajira ya askari mgambo. Kwa mantiki hiyo askari mgambo aliyeajiriwa na Manispaa anawajibika kusimamia sheria za nchi pamoja na sheria ndogo za Halmashauri kama ilivyo kwa askari polisi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Mipaka hiyo ni pamoja na kulinda mali za umma, kulinda usalama wa wananchi pamoja na mali zao na kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinazingatiwa wakati wote. *(Makofi)*

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa nchi yetu inatawaliwa na utawala wa sheria na kwa kuwa hawa mgambo wamekuwa na tabia ya kukusanya vitu na kwenda navyo wanakokujua wao na kwa kuwa ipo sheria ya kuwapeleka Mahakamani ili Mahakama iamue, kwa nini wanamgambo hao wanajichukulia hatua mikononi badala ya kuwapeleka katika Mahakama zinazohusika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoeleza hapa kuna swali tuliwahi kujibu la namna hii. Utaratibu haumtaki askari yeyote yule awe Mgambo au askari polisi kuchukua mali halafu aishie nayo moja kwa moja. Hakuna utaratibu wa namna hiyo, huo ni uvunjaji wa sheria na utaratibu huo tunaukataa haukubaliki. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa kama anayo mifano ya watu ambao wamefanya hivyo atupatie ili kwa kushirikiana na mamlaka zinazohusika tuchukue hatua zinazotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema ni kwamba wakati zoezi hili linafanyika la kwenda kukamata mali, kwa sababu tumeeleza hapa kwamba wale vijana wanakaidi, inawezekana kabisa pale ikatokea purukushani na ile purukushani ndiyo inaweza kuzaa mambo ya namna hiyo. Ombi letu kama Serikali na maelekezo yetu ni kwamba wakati hawa vijana wanapotakiwa kwenda kwenye Kituo cha Polisi au cha Halmashauri watii maelekezo yale ili kuzuia hali hiyo isijitokeze. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Lakini Mheshimiwa Mossy usimtake atoe ushahidi kwa sababu hiyo inakuwepo, Mheshimiwa Zungu ndiko huko unakotokea. *(Kicheko)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kero hizi zinaendelea siku hadi siku mgambo, takataka, ujenzi holela. Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka kwa Dar es Salaam kuwa na mpango maalum wa utawala zaidi ya mikoa mingine? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wote tunafahamu kwamba kuna kero nyingi Dar es Salaam na Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatoa agizo kwamba Jiji la Dar es Salaam liwe *treated* tofauti na sehemu nyingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa hivi kimeteuliwa kikundi kazi cha kuangalia miundombinu mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam ili kuondoa kero. Kwa hiyo, kwa Bajeti ijayo tunategemea kwamba Dar es Salaam itaangaliwa tofauti kama kioo cha nchi tofauti na majiji mengine. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa migogoro hii ya mgambo pamoja na vikundi vya wafanyabiashara iko nchi nzima na kwa kuwa sheria iliyoanzisha mgambo ya *Peoples Military* katika kifungu kimoja inazungumzia mgambo kupewa mafunzo na kwa kuwa kwa utaratibu wa sasa mgambo wanapata mafunzo ya kijeshi na siyo kama wanavyopata polisi ya taratibu mbalimbali zikiwemo za kisheria, je, Serikali iko tayari sasa kutekeleza kile kifungu cha sheria na kuandaa mpango rasmi wa mafunzo kwa mgambo kwa nchi nzima ili watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa sheria?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika mgambo mara nyingi wanajifunza mafunzo ya kijeshi lakini kwa Jiji la Dar es Salaam tuna wala *Auxiliary Police* ambao wanapata mafunzo kutoka chuo cha *CCP*, Moshi na mafunzo haya yanaendelea kwa awamu mbalimbali kulingana na mahitaji na uwezo wa kifedha. Kwa kweli kwa sasa hivi kusema kwamba wanamgambo wote nchi nzima waweze kufundishwa mafunzo ya kipolisi hili litakuwa gumu lakini tunalichukua kama ushauri ili tuweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Na. 479

**Kamati za Ushauri za Wilaya**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilitarajia kuongeza nguvu ya dhana za madaraka kwa wananchi, uongozi shirikishi na utawala bora kwa kuanzisha Kamati za Ushauri za Wilaya *(DCC)* na kwa kuwa Kamati hizo zilitarajiwa kuanza shughuli zake kuanzia mwaka huo wa fedha 2007/2008:-

(a) Je, mpaka sasa ni Kamati ngapi za ushauri za Wilaya zimeanza kufanya kazi na ni mafanikio gani na matatizo gani zimepata mpaka sasa?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kufafanua wajibu, majukumu na mahusiano kati ya Kamati hizo za Ushauri na Mabaraza ya Ushauri *(Full Council)?*

(c) Je, Serikali inaweka mikakati gani ya kupata mapato ya kutosha na kuziwezesha Kamati hizo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mbunge wa Mkinga. lenye sehemu (a), b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Kamati za Ushauri za Wilaya nyingi hazijaanza kazi kutokana na kutotengwa kwa fedha za kuendesha vikao hivyo katika Bajeti ya mwaka wa fedha uliopita yaani 2007/2008. Hii inatokana na ukweli kwamba maelekezo ya kuundwa kwa Kamati hizi yalitolewa tarehe 18 Juni, 2007 kipindi ambacho Bajeti za Mikoa zilikuwa zimekwishapitishwa na kuidhinishwa na Serikali. Hivyo ni vigumu kwa sasa kutaja mafanikio ya Kamati hizi ambazo bado hazijaanza kazi ipasavyo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua ya kufafanua muundo, majukumu, wajibu na mahusiano kati ya Kamati za Ushauri za Wilaya na Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri *(Full Council)* kwa kutoa maelekezo kuhusu muundo wa uendeshaji wa Kamati hizo. Maelekezo haya yalitolewa na kutumwa kwa wadau mbalimbali wakiwemo Wakuu wa Mikoa 21, Wakuu wa Wilaya 113 na Halmashauri 133 kwa barua Kumb. Na. CAB.CGA.307/314/01 ya tarehe 18 Juni, 2007. Aidha, ufafanuzi zaidi ulitolewa kwa wadau hao kuhusu utaratibu wa uendeshaji wa vikao vya Kamati za Ushauri za Wilaya ikiwemo wajibu na majukumu ya misingi ya Kamati hizo kama ilivyofafanuliwa kwenye kifungu cha 15B cha Sheria Na. 13 ya *The Local Government Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2006. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mahusiano kati ya Mabaraza ya Madiwani na Kamati za Ushauri za Wilaya ni kwamba Baraza la Madiwani *(Full Council)* ni chombo cha Maamuzi na Kamati ya Ushauri ya Wilaya ni chombo cha Ushauri. Kamati zote zina majukumu yanayolenga kuchochea na kuharakisha maendeleo ya wananchi kijamii, kisiasa na kiuchumi. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Serikali imehakikisha kila Mkoa umetenga fedha kwa ajili ya kuendesha vikao vya Kamati hizi. Hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka huu wa fedha vikao hivyo vitafanyika kama ilivyopangwa, tayari Mikoa imeelekezwa kuandaa ratiba ya vikao vya kisheria vikiwemo vikao vya Kamati ya Ushauri ya Wilaya *(DCC). (Makofi)*

**MHE. MBARUK K. MWANDORO**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Pia nashukuru kwa majibu mazuri na fasaha yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Kwa kuwa *DCC* ni chombo cha ushauri na Baraza la Madiwani ni chombo cha uamuzi, je, endapo patakuwa na mgongano wa maamuzi kati ya vyombo hivi viwili chombo gani kinachukua nafasi ya juu? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoeleza hapa hizi *District Consultative Committee* ndio zinaanza kazi na kwa kweli hazijachukua muda mrefu na hatujazifanyia kazi kwa maana hiyo niliyozungumza hapa.

Kimsingi kazi inayofanywa na *DCC* ni kama ile inayofanywa na *Regional Consultative Committee* na Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, anataka kujua kwamba endapo kutatokea mgongano hapo, jambo ambalo halitegemewi kwa kweli kwa sababu hawa wanafanya kazi ya ushauri na hao wengine kwa maana ya Madiwani wanafanya kazi ya maamuzi, lakini wote sisi hapa tunafanya kazi kama wadau muhimu katika jambo hili, iko ngazi iliyoko juu tu *immediately* pale ngazi ya mkoa ambayo inaweza kuingilia kati maamuzi yoyote ambayo yatakuwa yamefanyika pale na matumaini yetu ni kwamba Madiwani pamoja na hiki chombo watakuwa wanashirikiana kwa ajili ya kuleta maendeleo zaidi. *(Makofi)*

Na. 480

**Vipimo vya Lumbesa kwa Zao la Viazi**

**MHE. YONO S. KEVELA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Igosi na Imalinyi katika Jimbo la Njombe Magharibi ni wakulima wa viazi mviringo na kwa kuwa kuna kero kubwa ya vipimo vya kupimia zao hilo maarufu kwa jina la lumbesa ambavyo humnyonya mkulima:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuondoa kero hiyo ya vipimo vya lumbesa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yono Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba matumizi ya lumbesa ni kero kwa kuwa lumbesa ni kipimo batili cha ujazo wa mazao katika gunia kupita kiasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutoa kero hiyo ya lumbesa, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya vipimo sahihi kwa ajili ya biashara. Mathalani Serikali kupitia Wakala wa Vipimo Mkoa wa Iringa ilianza kutoa elimu kuhusu vipimo sahihi na vipimo batili kwa mazao ya wakulima kuanzia mwaka

2003. Aidha, elimu imetolewa kwa wananchi wa Wilaya ya Njombe wakiwemo wananchi wa Igosi na Imalinyi.

(ii) Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kupitia Kikao cha Kamati ya Uchumi, Ujenzi wa Mazingira cha tarehe 20 Mei, 2005 na Kikao cha Baraza Kuu la Madiwani cha tarehe 18 Agosti, 2005, ilitoa tamko la kuzuia matumizi ya lumbesa katika Wilaya ya Njombe na Watendaji wa Kata na Vijiji waliagizwa kusimamia zoezi hilo na kuchukua hatua za kisheria kwa wanaobainika kuendelea kutumia lumbesa.

(iii) Serikali imekuwa ikiwashauri wananchi kuuza mazao yao kupitia magulio au masoko ambapo kuna mizani ya kupimia mazao. Katika kutimiza azma hiyo, Halmashauri ya Njombe kupitia miradi mbalimbali imejenga masoko kumi yakiwemo masoko ya Igodivaha, Uhekule na Soko la Kimataifa la Igaga ambayo yapo katika Jimbo la Njombe Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo, Serikali kupitia Wakala wa Vipimo na Jeshi la Polisi imeendelea kusimamia Sheria na Kanuni za Vipimo kwa kuweka vizuizi barabarani na pia kufanya ukaguzi kwenye masoko kwa lengo la kubaini wafanyabiashara wanaoendelea kukiuka sheria hiyo. *(Makofi)*

**MHE. YONO S. KEVELA**: Mheshimwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa jibu la msingi anazungumzia Soko la Kimataifa la Igagala, yeye amesema Igaga, lakini inaitwa Igagala liko Njombe. Nijuavyo kuna mzani mmoja ambao ni hafifu na haujapitia hata *TBS* yaani Shirika la Viwango na kwa kuwa hata elimu anayoizungumza bado hawajapatiwa wananchi wa vijiji hivi, je, Serikali haioni kama itaendelea kumnyonya mkulima wa mazao kama elimu ya matumizi ya mizani na uboreshaji wa miundombinu katika soko hili haitatolewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kilimo kimeajiri karibu asilimia 80 ya Watanzania, je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuweka chombo maalum kama ilivyo kwa usafiri kuna *SUMATRA*, Nishati na Madini kuna *EWURA* ambacho kitasimamia bei ya mazao ili mkulima huyu mnyonge asiendelee kunyonywa kama anavyonyonywa kwenye mbolea? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ilitolewa kwa vijiji hivyo nilivyovitaja. Lakini kwa kuwa elimu haina mwisho tutaendelea kuwapa elimu wananchi hao ili waweze kuacha mitindo ya kutumia lumbesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba tangu Julai, 2007 mpaka Januari, 2008 walikamatwa wafanyabiashara 350 wanaotoka Wilaya ya Njombe walikuwa wamebeba mazao yakiwa kwenye magunia ya lumbesa na walitozwa faini ya shilingi

milioni 24.  Baadhi ya wananchi ndio walijulisha Serikali kuhusiana na wafanyabiashara hao. *(Makofi)*

Kuhusu chombo, chombo hicho tumeshaeleza hapa kwamba ni vyema kuanzisha Bodi ya Mazao mchanganyiko na sasa hivi tunasubiri Sera ya Masoko ikamilike tunaanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko ambayo ndiyo itakuwa inashughulikia suala la bei pamoja na haki za mazao ambayo hayana Bodi kama viazi, mahindi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa maelekezo kwa Wakala wa Mizani kwamba akaione mizani ambayo iko kule na kama si sahihi hatua muafaka ichukuliwe. *(Makofi)*

Kuhusu Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo sera iko njiani, tutashirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ili kuona kwamba hayo yote yanayohitajika yanafanyika ili kuimarisha biashara ya nafaka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:**  Mheshimiwa hili suala la lumbesa viazi na nini na mimi linanihusu.  Wakuu wa Mikoa wakihusika tu wameshika magunia yaliyozidi wakapeleka Magereza wakala wamekoma wale wahuni. *(Makofi)*

Ndiyo inavyotakiwa na tumefanikiwa kule Njombe kwa sababu ya Wakuu wa Mikoa ya Iringa na Mbeya waliwashika wale wote waliobeba viazi kuzidi kiwango kinachostahili na chakula kile kikapelekwa Magereza.  Kwa hiyo, na wengine wanajua kwamba watakula hasara basi wanaacha.  Kwa hiyo, naomba hatua zichukuliwe kwa haraka sana kwa sababu ni jambo muhimu.  *(Makofi)*

Na. 481

**Kilimo Bora cha Zao la Tumbaku**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA (k.n.y. MHE. JAMES D. LEMBELI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Kahama ni miongoni mwa Wilaya zinazozalisha Tumbaku kwa wingi; na kwa kuwa kilimo cha Tumbaku katika nchi yetu kinaaminika kusababisha uharibifu wa mazingira na hasa ukataji wa miti kwa ajili ya kukaushia Tumbaku:-

(a) Je, tangu kilimo cha zao hilo kianze Wilayani Kahama miaka ya 1970, Serikali imefanya jitihada gani za kuwasaidia wakulima wa zao hilo katika Kata za Ulowa, Ushetu, Bulungwa, Idahina na Kisuke ili kuepuka uharibifu wa mazingira?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani za kuzuia uharibifu wa kufyeka misitu kwa ajili ya kuni, uliofanyika katika pori la akiba la Kigosi - Moyowosi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kilimo cha zao la Tumbaku nchini kinafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Sekta ya Tumbaku Namba 24 ya mwaka 2001 na kanuni zake za mwaka 2005 ambazo zinaelekeza pamoja na mambo mengine suala la kupanda miti kwa ajili ya nishati ya kukausha tumbaku na utumiaji wa teknolojia zinazopunguza matumizi ya kuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania imeshirikiana na Wadau wa Sekta ya Tumbaku kutoa elimu kwa njia ya mikutano ya hadhara, semina na vipindi vya redio kuhusu suala la upandaji miti katika maeneo ya tumbaku yakiwemo ya Kata za Ulowa, Ushetu, Bulungwa, Idahina na Kisuke katika Wilaya ya Kahama. Aidha, wakulima wakipewa mbegu za miti na miche ya miti kwa bei nafuu sana kwa ajili ya kupanda katika maeneo yao.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuzuia ufyekaji miti katika pori la akiba la Kigosi – Moyowosi Serikali kupitia Idara ya Misitu imeweka utaratibu kwa ajili ya mahitaji ya kuni kwa kilimo cha Tumbaku. Utaratibu unaozingatiwa ni kwa Idara ya Misitu kutoa vibali vya kuokota kuni katika miti iliyokauka na kuanguka. Kwa mfano katika msimu wa mwaka 2007/2008, Wilaya ya Kahama ilitoa vibali 22 kwa ajili hiyo. Changamoto kubwa inayowasumbua katika hifadhi ya msitu wa Kigosi – Moyowosi ni wavamizi wanaokata miti kwa ajili ya mkaa na mbao.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na jitihada za kupambana na wavamizi hao kwa taratibu za sheria zilizopo. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa wananchi wakulima wa zao la Tumbaku wa Wilaya ya Kahama na Wilaya ya Bukombe wamesema kwamba wanasaidiwa na Serikali kwa kupewa miche kwa bei nafuu ni kitu ambacho sikiamini na sina uhakika nacho na wananchi hao wamejitahidi sana kuhakikisha kwamba wanatunza mazingira lakini Serikali haijatoa msaada mkubwa kwa ajili ya wananchi hawa.

Je, Serikali inawaahidi nini sasa wakulima wa zao la Tumbaku wa Wilaya ya Kahama na Bukombe katika utunzaji wa mazingira ili waendeleze zao hili?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme masharti ya kupanda Tumbaku ni pamoja na kupanda miti ya kutosha kwa ajili ya kukaushia tumbaku hiyo na kutumia majiko sanifu ambayo yatapunguza matumizi ya kuni kwa asilimia 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimjulishe Mheshimiwa Mbunge na nimhakikishie kwamba kuanzia mwaka 2006/2008 miti milioni 2.8 imeshapandwa katika Wilaya ya Kahama na majiko sanifu **200000.6** yameshajengwa katika maeneo ya kukaushia tumbaku katika Wilaya hii ya Kahama. Kwa hiyo, programu hii ya kupanda miti ipo na wanaoshirikiana wakulima pamoja na wale wanunuzi wa tumbaku Kampuni ya *Alliance*

*One Internationa* yanasaidiana kwa karibu kabisa kutoa hii miche pamoja na mbegu. Kwa hiyo, mazingira yanadumishwa kwa kutoa mbegu na pamoja na miche. Lakini hata hivyo Serikali itaendelea kutoa elimu ili iweze kusaidia katika suala hili. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii. Kwa kuwa wakulima wa tumbaku kwenye mikataba yao hii ya sasa kila mkulima wa tumbaku anayepewa mbolea mfuko mmoja anapanda miti 50; na kwa kuwa wamekuwa wanajitahidi sana kuhifadhi mazingira katika maeneo yao ya kilimo cha tumbaku. Sasa je, kwa kuwa bado maeneo mengine ambayo bado hayalimi tumbaku lakini mazingira yao yameendelea kuharibiwa kwa matatizo mengine tu kwa mfano moto, kuni na kadhalika. Je, Serikali sasa iko tayari kuleta taarifa ya uwiano wa waharibifu mazingira ili kuondoa dhana ya kuwa uharibifu wa mazingira unaofanywa katika maeneo tu yanayolima tumbaku peke yake?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali tutashirikiana na Mheshimiwa Said Nkumba ili tuweze kuona maeneo ambayo wakulima wa tumbaku wamekwenda kinyume pamoja na maeneo ambayo hayalimwi tumbaku lakini mazingira yanaharibiwa basi tutaonana naye lakini Serikali tuko tayari kushirikiana kwa vyovyote vile kutoa ripoti yoyote ambayo itasaidia kudumisha mazingira. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS**: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Waziri Kivuli wa Kilimo, kwa hiyo nalima tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utafiti wa kilimo cha tumbaku kwanza kina faida kidogo kwa kilimo za kiuchumi, lakini kina hasara kubwa sana kwa afya za wakulima na kwa mazingira. Kwa nini Serikali inasita kuwashawishi wakulima wa kuachana na kilimo cha tumbaku na kuanzisha zao mbadala badala ya lile? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Zao mbadala usiseme wewe. Umeshawaudhi wakulima wa tumbaku. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha tumbaku ni tofauti na matumizi ya sigara. Kwa hiyo, kuna kilimo cha tumbaku na kuna matumizi ya sigara ambayo yanaumiza afya zetu. Niseme tu kwamba tunachofaidika kwenye kilimo cha tumbaku ni pamoja na shilingi bilioni 75 ambazo tunazikusanya ni pamoja na shilingi bilioni 63 ambazo wakulima wa tumbaku wanazipata na ni pamoja na shilingi bilioni 4 ambazo Halmashauri katika maeneo ya tumbaku wanazipata. Kwa hiyo, tunachowashauri wananchi ni kwamba mtu halazimishwi kuvuta sigara. Lakini tunahimiza kilimo bora na uzalishaji kwa wingi kabisa wa tumbaku ili tuweze kuongeza uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Kivuli nakuomba ushauri kama eneo lako pia linafaa kulima tumbaku tutakuletea wataalamu kusudi tuweze kuongeza uzalishaji wa tumbaku. *(Makofi)*

Na. 482

**TBC Taifa Kusikika Kibondo**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa *TBC* Taifa haijawahi kusikika Wilayani Kibondo tangu ilipoanzishwa; na kwa kuwa ahadi ya Serikali ni kuhakikisha redio hii inasikika kwa wananchi wote:-

(a) Je, ni lini *TBC* Taifa itaanza kusikika Kibondo ili kuwawezesha wananchi wapate huduma hiyo?

(b) Je, nini mpango wa Serikali katika kushawishi redio binafsi ili zitoe matangazo ya *TBC* walau Taarifa za Habari?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (k.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Mheshimiwa Spika, aliagiza kwamba Mheshimiwa anayekaa karibu na kiti kile karibu na cha Waziri Mkuu basi awe anasimama simama na kujibu maswali. Hivyo kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhambwe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishamjibu Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum alipouliza swali kuhusu ukosefu wa masafa ya *TBC1* na *TBC* Taifa mkoani Singida kwamba Serikali bado inaendelea na juhudi zake za kuhakikisha kuwa huduma za *TBC1* na *TBC* Taifa zinawafikia wananchi kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni, Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alizindua mitambo ya *KW 2* ya kurushia matangazo ya redio katika mfumo wa *FM* katika mikoa kumi ya Tanzania Bara, ukiwemo Mkoa wa Kigoma.

Katika awamu ya pili *TBC* imepanga kufunga mitambo katika Makao Makuu ya mikoa mingine iliyobaki na baadae katika miji mikuu ya Wilaya ambazo upatikanaji wa *TBC* Taifa ni hafifu ikiwa ni pamoja na Kibondo ili kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata huduma hiyo. Kukamilika kwa zoezi hili kunategemeana na fedha zinazotengwa kwa ajili ya ununuzi wa mitambo. Kwa sasa Kibondo inapata huduma ya *TBC1* kupitia mtambo mdogo wa *KW 10* unaomudu kufanya kazi kwa kutumia jenereta ambao hata hivyo upatikanaji wa matangazo yake ni wa hafifu kutokana na uwezo mdogo wa mtambo huo. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vingi vya habari vya binafsi vinavyoanzishwa ikiwa ni pamoja na redio vina sera zake. Kwa muda mrefu sasa, baadhi ya redio hizo kama vile za taasisi za kidini, Halmashauri za Miji na kadhalika zimekuwa

zikijiunga na *TBC* (redio na televisheni) kwa hiari yake bila ya *TBC* kuzishawishi wakiamini kuwa taarifa hizo ni za kweli na uhakika, mfano taarifa za habari. *(Makofi)*

Napenda kuchukua fursa hii kuviomba vyombo hivyo binafsi kuendelea kupokea matangazo ya *TBC* ili kuwapa wananchi taarifa mbalimbali zinazotokea ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametoa majibu yake na amekiri moja kwa moja kwamba wananchi hao hawapati huduma hiyo ya kupata taarifa ya habari kama inavyotakiwa na kwa kuwa wananchi hao wamekuwa wakitegemea redio ama kupata habari kupitia Redio Kwizera ambayo ni redio inayohudumia Wakimbizi na kwa kuwa redio hiyo sasa inaondoka baada ya zoezi la *repatriation* la kuwarudisha Wakimbizi kukamilika, je, Waziri haoni kwamba kuna umuhimu wa kuharakisha kupeleka hiyo huduma kwa wananchi wa Kibondo na hususan mkoa mzima wa Kigoma ili wananchi waendelee kupata taarifa za ulimwengu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha Redio anachokitaja kinamilikiwa na Kanisa Katoliki jimbo la Rulenge kule Ngara na hatuna taarifa kwamba kuna mpango wa kuifunga. Ni matumaini yetu kwamba redio hii itaendelea kuhudumia maeneo hayo ikiwa ni pamoja na Kibondo. Hata hivyo matumaini makubwa ya redio kusikika katika mikoa ya Kigoma, Tabora na Rukwa ni hapo ambapo umeme wa kuaminika utakapofika Kigoma baada ya mradi mkubwa wa Malagarasi unaofadhiliwa na *MCC* kukamilika. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majawabu yake. Lakini kwa sababu amekubali bado *TBC* haijaingia katika nchi nzima Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu lile tangazo linalomshirikisha Onyango na ndugu yetu kutoka kule Pemba linalosema kwamba *TBC* Taifa inasikika nchi nzima, wewe unasikiliza redio inayoishia hapo Magomeni? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa bado tangazo lile ni kutoka kadri ile Redio Tanzania bado haijasikika nchi nzima?

**NAIBU SPIKA:** Si wamekwambia kwingine hakuna umeme tu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Naibu Spika, ukilinganisha na redio zingine hapa nchini *TBC* bado inaongoza na kwa kweli kwa sehemu nyingi sasa hivi *TBC* inasikika na hasa katika visiwa vya Unguja na Pemba. *(Makofi)*

Na. 483

**Skimu za Umwagiliaji Nzega**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa katika maeneo ya Mikoa ya Magharibi ikiwemo Wilaya ya Nzega kumekuwa na ukame wa mara kwa mara na upatikanaji wa mvua umekuwa si wa uhakika:-

Je, Serikali ina mpango gani kabambe wa kuanzisha Skimu za Umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za awali za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Wilaya ya Nzega zilianza chini ya Mpango wa *Smallholder Development Project for Marginal Areas* uliotekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka Shirika la Kimataifa la Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo yaani *International Fund for Agricultural Development (IFAD)*, pamoja na mchango wa Serikali ya Tanzania. Mpango huo ulitekelezwa kati ya mwaka 1990 na 1997 kwa kujenga miundombinu ya uvunaji maji *(Water Harvesting)* na kuhusisha Skimu za Lusu (hekta 200) na Nata (hekta 300), zote katika Wilaya ya Nzega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mpango kukamilika mwaka 1997, ilifuatia Programu Husishi ya Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji inayojulikana kama *Participatory Irrigation Development Programme (PIDP)* iliyoanza mwaka 2000 kwa mkopo kutoka *IFAD.* Jumla ya hekta 11,719 zimeendelezwa katika programu hiyo katika mikoa sita yenye ukame ikiwa ni pamoja na Wilaya Nzega, Mkoani Tabora. Katika mwaka 2001/2002, programu ya *PIDP* ilizifanyia ukarabati na kuongeza eneo linalomwagiliwa Skimu za Nata (hekta 300), Lusu/Ifumba (hekta 600) katika Wilaya ya Nzega na Skimu za Chomachankola (hekta 300) na Itumba (hekta 175) Wilayani Igunga. Skimu za Chamipulu (hekta 329), Lakuyi (hekta 92) na Sigili (hekta 315) ambazo hazikukamilishwa na *PIDP* kutokana na programu hiyo kufika mwisho, zilikamilishwa na Serikali mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka 2002, Serikali ilianzisha mpango kabambe wa Kitaifa wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani *(National Irrigation Master Plan – NIMP).* Mpango huu umebainisha kwamba Wilaya ya Nzega ina hekta 16,100 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji ambazo zimekaguliwa lakini kuna uwezekano mkubwa sana wa kuongeza eneo hilo kwa kujenga mabwawa. Kwa mfano, mabwawa ya Malolo na Nkiniziwa (Nzega) yamekarabatiwa, aidha, bwawa la Ulyanyama Wilayani (Sikonge) linaendelea kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2008/2009 mabwawa ya Ikundwa (Bukene) na Idudumo (Nzega) yataendelezwa kupitia Mpango wa Maendeleo ya Kilimo

ya Wilaya. Aidha, bwawa jipya la Kahamahalanga ambalo lilikuwa ahadi ya aliyekuwa Waziri Mkuu, Hayati Edward Moringe Sokoine nalo litajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanza kutekelezwa kwa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)* utaratibu wa kuomba fedha za miradi ya umwagiliaji unaanzia katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)* baada ya kuibuliwa na wananchi wenyewe. Miradi inayopitishwa na Halmashauri ya Wilaya na kutengewa fedha za *DADPs* hujadiliwa na kuombewa fedha za nyongeza kutoka katika mifuko ya *ASDP* ya *District Irrigation Development Fund (DIDF)* au *National Irrigation Development Fund (NIDF)* kutegemea na ukubwa wa mradi. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Majibu ya Waziri hayafanani na lengo la swali langu. Lengo la swali langu ni kuona skimu za umwagiliaji iwe mvua imenyesha iwe mvua haikunyesha, lakini skimu zote alizozitaja zote zinategemea mvua inyeshe ndiyo wamwagilie. Sasa je, Serikali ina mpango gani madhubuti hasa katika Mapinduzi haya ya kijani kuhakikisha skimu za umwagiliaji hazitegemei tena mvua badala yake kuwa na umwagiliaji ambao una uhakika au mvua imenyesha au mvua haijanyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, *irrigation* za Nata, Lusu, Chomachankola, Sigili na Lakuyi nazo hutegemea mvua hasa kupitia bonde la Mto Manonga. Skimu hizo kama bonde la Mto Manonga likifurika ndiyo zinapata maji. Je, Serikali ina mpango wa kujenga mabwawa makubwa katika skimu hizo ili umwagiliaji uwe na uhakika zaidi kuliko hali ilivyo sasa hivi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimfahamishe Mheshimiwa Lucas Selelii, kwamba hakuna kilimo chochote hata cha umwagiliaji kisichotegemea mvua. Kwa sababu maji yote hayo yanatokana na mvua, mengine yanakuwa katika mito, mengine yanaingia ardhini. Kwa hiyo, si sahihi kusema mvua ikipotea kabisa basi umwagiliaji ndiyo yatakuwa majibu ya kwanza na ya mwisho. Nilitaka niliweke sawa hilo kwamba mvua ni lazima iwepo na hata hii miradi yetu ya *Irrigation* lazima itegemewe. *(Makofi)*

Kuhusu hii miradi ambayo tumesema kwamba imekuwa ikipata msaada, kwa kweli matokeo ni mazuri. Tunachokifanya hivi sasa kutokana na fedha kuwa kidogo tunatumia maji ya mvua zinazonyesha mbali sana, mbali ya maeneo yale. Hata kama mvua haijanyesha katika Wilaya ya Nzega basi maji yale tunayavuna ili angalau yatupatie kilimo cha mpunga hata kwa msimu mmoja, kama tusingefanya hivyo basi hata hizi hekta 11,000 nilizozitaja zingewezekana. *(Makofi)*

Kuhusu bonde la Mto Manonga na mpango wa mabwawa tumesema katika hotuba yetu ya Bajeti ya mwaka huu kwamba tunalenga sasa kujenga mabwawa ambayo nayo hayatakidhi kila kitu, mabwawa yale yatatusaidia kupata maji ya *supplementary irrigation* na kipaumbele tumeweka katika mikoa hii hii kame ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Tabora na Manyara. *(Makofi)*

Na. 484

**Kuwawezesha Watanzania**

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI (k.n.y. MHE. PETER J. SERUKAMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nne ilianzisha Wizara ya Uwezeshaji mbali na mpango ulioanzishwa na Mheshimiwa Rais wa kutoa shlingi bilioni moja kwa kila Mkoa nchini:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani unaotekeleza katika kuwawezesha Watanzania?

(b) Kama msingi wa kukua kwa uchumi ni sekta binafsi, je, Serikali imefanya nini hadi sasa kwenye eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Mjini, napenda kutoa maelezo machache kuhusu dhana ya uwezeshaji. Katika hatua za kuwawezesha Watanzania kiuchumi mambo ya msingi yanayotakiwa kuzingatiwa ni pamoja na taratibu za upatikanaji wa mitaji, elimu na ujuzi wa ujasiriamali na fursa za dhamana (kama vile nyumba, shamba eneo la kupata biashara *(premises)*. Ukosefu wa mitaji, ukosefu wa dhamana kwa ajili ya kupata mikopo kutoka kwenye Mabenki, kutokuwa na elimu ya kutosha, hasa elimu ya ujasiriamali na kutokuwa na historia ya kukopa na kulipa *(credit history)* vimekuwa ni vikwazo vikubwa katika kuwawezesha Watanzania kupata mikopo itakayowawezesha kuboresha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Serukamba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwawezesha Watanzania kiuchumi, Serikali imebuni na kutekeleza mipango mbalimbali ambayo utekelezaji wake unakwenda hatua kwa hatua. Aidha, baadhi ya matokeo ya mipango hiyo ni ya muda mfupi na mengine ni ya muda mrefu. Mipango hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuwawezesha wananchi kupitia Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi *(Mwananchi Empowerment Fund);*

(ii) Mpango wa mabilioni ujulikanao mabiliano ya JK;

(iii) Mpango wa Huduma za Fedha Vijijini *(RFSP);*

(iv) Mpango wa Kurasilimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA);

(v) Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA); na

(vi) Mpango wa Mikopo wa Wajasiriamali Wadogo *(Small Enterprise Loan Facility – SELF)* na mengineyo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa msingi wa kukua kwa uchumi wa nchi ni sekta binafsi. Ili kuboresha sekta hiyo, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuboresha miundombinu ya barabara, umeme, mawasiliano, maji, elimu, afya na huduma za Benki. Mafanikio katika kukuza uchumi hasa kwa mchango wa sekta binafsi yameanza kuonekana japokuwa changamoto bado ni nyingi. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ili mpango huu uweze kufanya kazi ninaamini ni vyema mpango wenyewe kwanza ukawezeshwa kwa maana ya kutengewa fedha kama mpango. Nitaaminije kwamba huu ni mpango mahsusi wa kuwasaidia Watanzania kuwaondoa katika dimbwi la umaskini. *(Makofi)*

La pili, ni kwa kiasi gani mpango huu umewasaidia wananchi ukiondoa utaratibu wa shilingi bilioni moja za JK ambazo zimekwishasambazwa nchini? Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza huu mpango wa kuwawezesha Watanzania kiuchumi ni mpango mmoja lakini kuna mifuko mingi na kila mfuko una Bajeti yake. Namwomba Mheshimiwa Mbunge tukae pamoja ili niweze kumpa *details* mfuko kwa mfuko jinsi gani unavyoweza kutekeleza na kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa wananchi wengi sana walioko katika maeneo yetu hususan vijijini hawafahamu juu ya mipango hii na kwa kuwa Serikali inatoa fedha kidogo sana kwenye Bajeti ya mipango hii kama vile kwenye MKURABITA, MKUMBITA na kadhalika. Serikali itafanya nini ili kuwafanya wananchi waelewe juu ya mipango hii na vile vile kuongeza fedha katika mipango hii?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli kuna haja kubwa ya kutolewa kwa elimu ili wananchi wetu waweze kufahamu juu ya mipango hii. Tutashirikiana na hii mifuko ili iweze kutoa elimu wananchi wote waweze kufahamu juu ya mifuko hii na mipango hii. Lakini la pili ni suala la kuipatia fedha hii mifuko ili wananchi wengi waweze kufaidika. Nakubaliana naye na tutaangalia kila hali ya fedha itakavyokuwa inaridhisha basi tutaiongezea mifuko hii fedha ili wananchi wengi waweze kufaidika. *(Makofi*

Na. 485

**Idadi ya Madaktari Nchini**

**MHE. DR. ALI TARAB ALI (k.n.y. MHE. SAID A. ARFI)** aliuliza

(a) Je, kuna Madaktari wangapi waliosajiliwa nchini na wangapi wanafanya kazi kwenye Hospitali binafsi na wangapi Serikalini?

(b) Je, Madaktari hao wamegawanywa vipi nchini kimkoa na Kiwilaya na ni Mkoa upi una Madaktari wengi na upi una wachache?

(c) Je, idadi ya Madaktari Bingwa nchini ni ngapi na mgawanyo wao Kimkoa na Kiwilaya ukoje?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Madaktari waliosajiliwa katika Daftari la Usajili wa Madaktari ni 3,641. Idadi hii inajumuisha Madaktari wenye Shahada *(Medical Doctors)* na walio na Stashahada *(Assistant Medical Doctors –AMO).* Madaktari waliopo kwa sasa ni 2,612 na tumeandaa jedwali ambalo Mheshimiwa Mbunge tutampatia.

Tulifanya zoezi la kutambua Madaktari wetu wako wapi mwaka 2004 na ikadhihirika kwamba Madaktari wa Afya 343 walikuwa nje ya nchi na kati ya hao 111 walikuwa ni Madaktari. Madaktari wanaofanya kazi Serikalini ni 2,382 na Madaktari wanaofanya kazi katika Sekta binafsi ni 230. *(Makofi*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, nimeandaa jedwali vile vile linaloonyesha mgawanyo wa madaktari Kimkoa na Kiwilaya. Jedwali n refu na vile vile tutampatia muuliza swali. Mkoa ambao una madakatri wengi ni Dar es Salaam ambao una Madaktari 489 hii inajumuisha Madaktari waliopo Hospitali ya Muhimbili ambao wapo wengi wanaofanya kazi Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili, *MOI* na Hosipitali ya Saratani *Ocean Road. (Makofi*

Mikoa yenye Madaktari wachache ni Tabora na Singida ambayo kila mmoja una Madaktari 40. Mkoa wa Rukwa anakotoka muuliza swali kuna Madaktari 56 na kati ya hawa Madaktari 11 wapo Wilaya ya Mpanda. *(Makofi*

(c) Idadi ya Madaktari Bingwa walio katika ajira ya TAMISEMI hapa nchini yaani ukiondoa wale walio katika Rufaa wako 110 na vile vile mgawanyo kimkoa na kiwilaya umeonyeshwa kwenye jedwali Mkoa wa Ruvuma una Madaktari Bingwa wawili. *(Makofi)*

**MHE. DR. ALI TAARAB ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa mujibu wa jibu la Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii inaonekana ya kwamba Madaktari walioko nje ya nchi nikimaanisha Madaktari wenye Shahada na Stashahada ni 1,029 ambayo hiyo ni karibu asilimia 40 ya Madaktari walioko nchini na labda tungepiga mahesabu wenye Shahada peke yao asilimia hii ingeongezeka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge badala ya kuuliza unaanza hotuba. Tafadhali uliza maswali ya nyongeza.

**MHE. DR. ALI TAARAB ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Sasa mimi nataka kujua kuna utaratibu gani wa kusomesha Madaktari zaidi na kuwavutia wale walioko nje warudi nchini? Hilo la kwanza.

La pili, huu mgawanyo wa Madaktari kwa Mikoa kwa sababu ukiangalia Iringa Madaktari ambao wana Shahada ni Madaktari saba, Rukwa nane, Manyara tisa, huko kwingine angalau afadhili afadhali. Sasa kuna utaratibu gani wa ugawaji huu angalau na hii Mikoa niliyouliza nao wapande kidogo ku-*double figure? (Makofi*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango mzima wa *MAM* suala la kusomesha wafanyakazi wa afya limepewa kipaumbele na kwa kuanzia toka mwaka jana tumekuwa tukiboresha mazingira na kuwavutia wanafunzi na hivi sasa kwa mwaka huu tutakuwa na wanafunzi 681 katika vyuo vyetu vya Muhimbili, *IMTU*, Bugando, *KCMC* na Hubert Kairuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tutakuwa na wanafunzi 210 wa Uzamili. Kwa hiyo, nadhani tunakwenda vizuri na mategemeo yetu ni kwamba kila mwaka tutakuwa tunapanua wigo wa usajili. *(Makofi)*

Kuhusu swali la pili, jambo la kwanza tuwe na Madaktari wengi katika soko ili tuweze kuwapeleka lakini tunashauri Halmashauri ziweke mazingira ya kuweza kuwavutia. Utaratibu uliokuwepo ilikuwa kwamba nafasi zinapopatikana kwenye Halmashauri ilikuwa inawajibika kutangaza hizo kazi. Sasa katika maeneo mengine hayavutii.

Sasa utaratibu uliopo ni kwamba Halmashauri inaainisha mahitaji na kuyaleta Wizarani halafu yanaombewa kibali utumishi na jinsi watumishi na jinsi wahitimu wanavyopatikana basi tunawapeleka katika maeneo hayo. Lakini nikasema kwamba kama watakwenda halafu hakutakuwa na nyumba hawatakaa. *(Makofi)*

Na. 486

**Walimu Kutopenda kwenda Kufundisha kwenye Maeneo ya Wafugaji**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa maeneo ya wafugaji yana mazingira magumu ambayo yanasababisha walimu wasipende kwenda kwenye shule hizo na ndio maana ziko nyuma kielimu kuliko maeneo mengine.

Je, Serikali inachukua hatua gani kujenga mazingira mazuri kwenye maeneo hayo ili walimu wakubali kwenda kufundisha kwenye shule zilizoko huko?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba baadhi ya mazingira magumu husababisha walimu wasipende kwenda kwenye shule zilizomo kwenye maeneo hayo yakiwemo maeneo ya wafugaji. Serikali kwa kushirikiana na wananchi na wadau wengine inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kujenga mazingira mazuri katika maeneo mbalimbali ili walimu waweze kwenda kufundisha katika maeneo hayo. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha miundombinu ya kutolea elimu na kuweka vivutio katika maeneo hayo kadri fedha zinavyopatikana kwa kujenga madarasa, maabara na maktaba. Aidha, Serikali inaendelea kutenga fedha za ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu kwa kuzingatia kuwa kila panapojengwa madarasa mawili pia inajengwa nyumba moja ya mwalimu. Kwa mfano, katika shule ya Sekondari ya Longido, Serikali kwa kushirikiana na wadau imejenga nyumba za walimu 15 na kupeleka umeme wa jenereta. *(Makofi*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na viongozi wote kuendelea kuwahamasisha wananchi katika maeneo yote kuweka kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za walimu ili ziwe kivutio kwa walimu kukubali kufundisha shule za maeneo hayo. Napenda nitoe wito kwa wadau wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na Halmashauri zote kuangalia uwezekano wa kuimarisha miundombinu na huduma zingine katika Halmashauri ili kuwavutia walimu katika maeneo yao. *(Makofi*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa katika maeneo haya walimu wanapata shida sana hasa kufuatilia matatizo na huduma zao muhimu. Kwa mfano wanatumia robo ya mishahara yao kufuata mahitaji. Je, Serikali haioni ni muhimu sasa kuwapa kipaumbele au malipo kwa ajili ya gharama hizo ili walimu hao waweze kukaa katika maeneo hayo?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali imetoa ahadi kwamba miaka ya nyuma itajenga maabala katika shule zote za sekondari na mpaka sasa kuna sekondari ambazo zina kidato cha kwanza mpaka cha nne na bado hawana maabara, Serikali inasema nini juu ya

maeneo hayo ambayo maabara hizo zinasababisha kushuka kwa taaluma katika sekondari hizo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana ni kweli walimu hao wanatumia sehemu yao ya pesa kufuata mahitaji muhimu kama vile vifaa, chakula na kadhalika. Lakini nashauri kwamba kwa kushirikiana na Halmashauri zetu pamoja na Bodi za Shule pamoja na Mamlaka nyingine katika Wilaya na mahali ambapo shule ilipo wawasaidie hawa walimu kwa kuwapatia labda vifaa vya usafiri. Kwa mfano Mamlaka ya Ngorongoro imewasaidia walimu na shule kwa kuwapa magari. Kwa hiyo, haya yanasaidia usafiri ili walimu hawa wasiendelee kusumbuka na kuacha madarasa wakati wanafuata huduma hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maabara, mwaka huu wa fedha kama tulivyoongea kwenye Bajeti tutajenga maabara na kila Mkoa utapewa maabara kumi. Kwa hiyo, ni juu ya kila Mkoa sasa kwa kushirikiana na Wakuu wa Shule kuangalia ni shule zipi ambazo zinahitaji maabara zaidi ili waweze kuzipatia na kuendelea kufundisha masomo ya sayansi ambayo ni muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama mnavyoona muda umekwisha kabisa na tumezidi kidogo lakini na maswali yamekwisha. Waheshimiwa Wabunge sasa tutakumbuka kwamba mwenendo wetu wa kumalizia Wizara mbalimbali kutoa hotuba zao ilikwisha jana. Sasa tunaingia katika ngazi muhimu ambayo inaunganisha yote tuliyoyafanya tangu tumeanza kwa Wizara mbalimbali sasa tunaunganisha pamoja na kupitisha Sheria inayojumuisha mafungu yote mliyoyapitisha hiyo ndiyo inaitwa *Appropriation Bill. (Makofi*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu Utaratibu Mheshimiwa Ole Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE –SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Kanuni ya 68(7) Muongozo wa Spika, na Kanuni ya 37(4) na (6). *(Makofi*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapema tarehe 29 Januari, 2008 mara tu baada ya Waziri aliyekuwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji kuwasilisha maelezo kuhusu Ukaguzi wa Fedha za *BOT,* akaunti ya *EPA* hapa Bungeni nilisimama mimi na Mheshimiwa John Cheyo kuomba kwamba taarifa iliyowasilishwa na Waziri iweze kujadiliwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge na nilipoomba Mheshimiwa Spika ambaye alikuwa amekalia kiti alipokea ombi letu na baada ya kulitafakari kwa pamoja alitukumbusha katika *Hansard* hiyo akisema kwamba amepokea taarifa ya awali ya Mheshimiwa Lucy Mayenga iliyohusu Mahesabu ya *BOT* na kwa maana hiyo alisema kwamba shughuli hizo zingepangiwa muda ili ziweze kujadiliwa na kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 143 inasema hivi “Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atawasilisha kwa Rais kila taarifa atakayoitoa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ndogo ya pili ya Ibara hii. Baada ya kupokea taarifa hiyo Rais

atawaagiza watu wanaohusika kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Kikao cha Kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika Kikao kabla ya kupita siku saba tangu taarifa hiyo ilipowasilishwa," inaendelea kusema "Iwapo Rais hatachukua hatua za kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Bunge." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa ni matakwa ya Katiba yanayodai mara baada ya ukaguzi taarifa hiyo kuwasilishwa kwa Rais na hatimaye kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu na kwa kuwa Waziri aliyekuwa na dhamana wakati ule aliwasilisha taarifa hiyo ya ukaguzi wa *EPA* hapa Bungeni na mimi nilisimama kuomba ijadiliwe lakini baadae katika utaratibu wa utekelezaji bora mwingine katika upande wa utendaji Rais aliteua Kamati ya Mheshimiwa Mwanyika na katika hotuba ya Rais ya juzi sehemu ya hotuba yake iligusia masuala haya ya *EPA* na kwa mujibu wa Kanuni hotuba ya Rais itabidi ijadiliwe kwa siku ambayo Kamati ya Uongozi itapanga na kwa matarajio yangu sasa ni kwamba Kikao kijacho cha Bunge. *(Makofi)*

Sasa nilichotaka kuomba Muongozo ni kwamba kwa kuwa sehemu hiyo ya *EPA* ni sehemu ndogo tu katika hotuba ya Rais; na kwa kuwa ripoti hiyo kamili ya *EPA* haijawasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Katiba ambayo ni matakwa ya Katiba ya nchi; na kwa kuwa sisi kama Wabunge tulikwishakuomba taarifa hiyo ijadiliwe na ili kuweka ufanisi katika kujadili hotuba ya Rais kwenye Mkutano ujao wa Bunge naomba Muongozo wako kwamba sasa Ofisi yako inatueleza nini kuhusu kupatikana kwa ripoti hiyo kukidhi matakwa ya Katiba na kukidhi matakwa ya Kanuni na ili kuweka ufanisi kwenye kuchangia hotuba ya Rais. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ole-Sendeka amezunguka, amezunguka anachotaka ni kwamba ombi lao la kwamba taarifa ya *EPA* ijadiliwe haijatekelezwa ndiyo anachoomba. Ndivyo nilivyosema nilipoanza kwamba tunayo taarifa nyingine ambayo hatujaijadili ya *BOT* ya 2005/2006 na kwa mujibu wa Kanuni hizi hizi wakati wa Kikao cha Bajeti mambo yanayotawala zaidi ni mambo ya Bajeti.

Kwa hiyo, nikaeleza lile ombi la Dr. Slaa la sasa hivi kwamba tutawapangia muda. Hoja hizi zote tukija Bunge lijalo zitapangiwa muda na maandalizi ya Miswada yote Kamati ya Uongozi ndiyo yanayosimamia maandalizi ya vikao vyote vitakavyohusika. Kwa hiyo, haya yote mliyosema yatapewa muda kwa Bunge linalofuata. La sasa limekwisha muda wake kazi tulizonazo haziwezi kuruhusu hoja binafsi zozote zile.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge lijalo zitakuwa kazi hiyo. Nadhani tumeelewana na kama maandalizi ya hoja hiyo lazima ifanyiwe maandalizi, kama ile ya Madini wanaendelea na maandalizi na hata hizo nyingine zinaendelea na maandalizi yanayostahili ili tuweze kuwa na mjadala wenye kukidhi haja yetu. Kwa hiyo hilo nimeshaamua. *(Makofi*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Muongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu nini tena?
**MHE. DR. WILBROD P. SLAA**: Ni Muongozo wa Spika, Kanuni ya 68(7).

**NAIBU SPIKA:** Inakwambia unaweza kuomba muongozo. Sasa mimi nimekuruhusu, fungu gani?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA**: Kifungu ninachozungumzia ni kifungu cha utaratibu wa *order paper*. Katika *order paper* ya leo sehemu ya III ukurasa wa 12 *order paper* inasomeka Muswada wa Sheria ya Serikali ambao ndiyo utaratibu unaofuata na mambo yanayofuata ni Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa mwaka 2008 *(The Appropriation Bill, 2008).* Unaofuata ni Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2008 *(The Finance Bill, 2008).* Sasa uzoefu wangu unaanza kutengeneza kwanza fedha halafu ndiyo unagawa. Sasa kwa *order paper* ya leo tunaanza kugawa kabla hatujazitengeneza naomba muongozo wako kama utaratibu huu ni sawa au vipi.

**NAIBU SPIKA:** Utaratibu huu ni sawa kabisa. Chukua Kanuni ya 105(3) ambayo inazungumzia Muswada wa Fedha za Matumizi ndiyo *Appropriation Bill*. Kanuni ya 106 inazungumzia Muswada wa Sheria za Fedha ndivyo Sheria inavyosema.

Ukisoma Kanuni ya 105(3) inasema hivi; "Muswada wa Fedha za Matumizi hautapelekwa kwenye Kamati yoyote ya Kudumu wala Kamati ya Bunge zima na masharti kuhusu Miswada kusomwa mara ya kwanza hayatatumika."

Halafu ya (4) inasema "Muswada wa Fedha wa Matumizi hautatangazwa kwenye gazeti kabla haujawasilishwa Bungeni."

Halafu (106) inasema; "Baada ya Bunge kukamilisha kazi ya kupitisha Muswada wa Fedha za Matumizi, Muswada wa Sheria za Fedha utajadiliwa na kupitishwa na kuzingatia masharti yaliyowekwa na sehemu ya nane ya Kanuni hiyo." Kwa hiyo, hii ni sahihi tulivyopanga kwenye *order paper*. Ni kwamba tukimaliza Appropriation Bill ndiyo tunaingia kwenye Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mujibu wa Kanuni ya 106. *(Makofi*

Tunaendela, kuna matangazo, kwanza tunawageni wafuatao:-

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Mtwara na Lindi ni Bwana Steven Masson huyu ni Rais wa Kampuni ya *Artumas* ya Canada inayotengeneza Umeme wa Gesi ya *Mnazi Bay* kule Mtwara, anafuatana na Bwana Salvatory Mtola, Mkurugenzi Mkuu wa *Artumas Gas Tanzania,* Bwana Ambogasti Oiso, Meneja Mawasiliano wa *Artumas,* yupo na Bwana Aggrey Maleale, Mshauri Mkuu wa Mahusiano *(Public Relation Artumas)*. Karibuni sana watu wa *Artumas* tunawategemea sana kuleta umeme Mtwara na msaidie pia kujenga kiwanda cha gesi kama inabidi. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Beatrice Shellukindo hawa ni Mchungaji Mbena ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la Kimataifa la kidini *Compasion* lenye Makao yake

Makuu Arusha. Yupo na Bwana Joseph Mayala, *Programme Officer*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Michael Laizer ambao ni Nashipai Yohana Laizer na Elifadhili Ole Ngeresa, karibuni sana. Tuna walimu 13 kutoka shule ya sekondari ya Makole Dodoma, karibuni sana na tumefurahi kuwaona. Halafu tuna kundi la wanafunzi 40 pamoja na walimu kutoka shule ya msingi Mvumi hili ni kundi lingine ambalo linaendelea na ziara. Karibuni sana tunajua kwa Mheshimiwa John Malecela huko. Tuna wanafunzi wengine pamoja na walimu wao wako 30 kutoka shule ya Seminari ya Hijra hili ni kundi lingine tena. Karibuni sana tunawashukuru. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi. Mheshimiwa Spika anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Uongozi kwamba kutakuwa na kikao leo tarehe 27 Agosti, 2008 saa saba mchana mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge hapa. Kamati ya Uongozi maana yake ni Wenyeviti wote. *(Makofi)*

Tuna matangazo mengine, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 27 Agosti, 2008 kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo na Waheshimiwa Wabunge wa Namibia. Saa nne na nusu katika chumba 219. *(Makofi*

Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa tano asubuhi kutakuwa na Mkutano katika chumba 227.

Halafu Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anaomba niwatangazie wajumbe wake kwamba leo tena saa tano asubuhi hii kutakuwa na kikao na wengine wanaopenda kuchangia mawazo wanakaribishwa. Hajataja chumba, itakuwa kwenye Ukumbi wa Msekwa, lakini saa tano Wabunge wote itawezekana wapi. Haiwezekani saa tano kwa Wabunge wote maana yake nyumba haitakuwa na watu. Kwa hiyo, ni Kamati yake saa tano hiyo. Ingekuwa saa saba ndiyo ingekuwa kwa Wabunge wote lakini kwa saa tano haiwezekani au mnabadilisha saa saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama anawatangazia wajumbe wa Kamati yake leo hii saa tano pia, watakuwa na kikao kwenye chumba namba 231. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib anawatangazia wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo saa tano na nusu kwenye Ukumbi wa Msekwa. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge itabidi Kamati ya Uongozi izungumzie mambo haya kwa sababu kama mnakwenda Wabunge wote wakati wa Kikao cha Bunge haiwezekani.

Kuna tangazo lingine muhimu, Waheshimiwa Wabunge kama mnavyoelewa Serikali imeamua kuuza sehemu ya hisa za *NMB* na kwamba zoezi hili limeanza na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wangependa kununua fedha hizo ili kurahisisha Waheshimiwa Wabunge watakaopenda kununua hisa hizo.

Waheshimiwa Wabunge, huduma hiyo imeletwa hapa Ofisi ya Bunge kwa maelekezo ya *Consolidated Holding Cooperation* kutoka Dar es Salaam na kwamba zoezi hili litatekelezwa na Kampuni iitwayo na Kampuni iitwayo *Stock Blockers Obit Securities*. *(Makofi* )

Waheshimiwa Wabunge, wanaopenda kununua hisa hizo wawaone wahusika wapo kwenye eneo yanapouzwa magazeti. Nadhani Ofisi ya Bunge ingewatafutia nafasi ya kufanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo tunaendelea na ratiba ya leo. Katibu.

**MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2008**
***(The Appropriation Bill, 2008)***

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2008**
***(The Finance Bill, 2008)***

*(Miswada Iliyotajwa Hapo juu Ilisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2008**
***(The Appropriation Bill, 2008)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH. S. SUMARI)**Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa kutumia shilingi 7,218,130,000,000/= kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo itakayotekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na kutumia fedha zitakazotolewa na Serikali kwa ajili hiyo pamoja na marekebisho yake, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasilishe marekebisho machache ya kiuchapaji yaliyofanyika katika vifungu namba 4 na namba 6 (5) cha Muswada ambapo katika kifungu cha 4 maneno *section two* yanapaswa yasomeke *section three* na katika kifungu cha 6(5) katika mstari wa tano, maneno *section two and section three* yanapaswa yasomeke *section three and four*. Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ataandaa utaratibu wa kuhuisha marekebisho haya kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2008/2009 nilieleza shabaha na malengo ya Serikali ya kutumia shilingi 7,218,130,000,000/= kwa mwaka wa 2008/2009 kama ifuatavyo:-

Kwanza, matumizi ya kawaida, shilingi 4,726,650,000,000/=, pili, matumizi ya miradi ya maendeleo shilingi 2,491,480,000,000/= na jumla ni shilingi 7,218,130,000,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu limekwishajadili na kupitisha hoja mbalimbali za Waheshimiwa Mawaziri wakati walipowasilisha Makadirio ya Wizara zao.

Madhumuni ya Muswada huu ni kuliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe matumizi ya Serikali ya mwaka wa 2008/2009 ya jumla ya shilingi 7,218,130,000,000/= kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Matumizi ya Kawada na Miradi ya Maendeleo iliyokubaliwa na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja! *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa iamuliwe)*

**Muswada wa Sheria ya Kuruhusu Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009 *(The Appropriation Bill, 2009)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tumekamilisha yale mazungumzo yetu tuliyokuwa tumefanya hapa kwa zaidi ya siku 50. Tulipitia Wizara kwa Wizara, halafu jumla yake kama mtakavyoona *The Appropriation Bill* yenyewe inavyoonyesha sasa inajumlisha yote mliyokuwa mmesema, sasa tunayapitisha kisheria ndio maana inaitwa *The Appropriation Bill.*

Kwa hiyo, sasa tumekamilisha na hii *Appropriation Bill* hatuingii kwenye Kamati ya Matumizi. Tulivyomaliza sasa tumemaliza kwamba tunakubali yale tuliyofanya siku zote hizi, sasa yote yanakuwa *appropriated.* Sasa mabadiliko aliyosema Waziri kwa sababu yametajwa kwenye *Hansard* na yenyewe yataweza kuwekwa vizuri katika sheria yenyewe itakapokuwa inakamilishwa kikamilifu. Kwa hiyo, sasa tunaingia hatua ile ya Sheria ya Fedha.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Niabu Spika, najua hili ni jambo ambalo naweza kulizungumza hapo labda kwenye Kamati. Lakini mimi nataka kujua tu kwamba kwa sababu Bunge hili tayari lilishaelezwa na Mheshimiwa Rais kwamba kutakuwa na zaidi ya shilingi bilioni 60 ambazo zimetoka *EPA* ambazo zitaingia kwenye kilimo na zitaingia na *TIB,* sasa hizo fedha zitaingiaje kisheria? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza, mimi kama ningekuwa Mheshimiwa John Cheyo hili swali ningeliingiza kwenye mjadala mzuri kabisa katika sheria inayokuja, hii kwa sababu hiyo ni sheria ya mapato, yaani, ungelieleza vizuri kabisa, ukapewa dakika zako ukajieleza kwa sababu ni sheria ya fedha, hapo ndipo ungeingia vizuri sana na ukai-*discuss* vizuri zaidi kuliko kupata Mwongozo wa Spika, kwa sababu hata ningekuwa na Mwongozo, siwezi kusema fungua sasa tuingize mahali fulani, siwezi kufanya hiyo kazi. Lakini unaweza kuijadili vizuri katika sheria inayofuata sasa hivi na ukaiweka vizuri sana na Waziri akapata utalaam unaostahili, akakueleza vizuri zaidi. Kwa hiyo, naomba tuendelee na hatua inayofuata. *(Makofi)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2008
### *(The Finance Bill, 2008)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2008 yaani *The Finance Act, 2008* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati na pia tutaendelea kufanyia kazi mapendekezo mengine ipasavyo. Aidha, kwa mara nyingine napenda kutoa tena shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao walichangia katika hotuba ya Bajeti ya Serikali niliyowasilisha hapa Bungeni mnamo mwezi Juni, mwaka huu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuandaa Muswada huu, wadau mbalimbali katika sekta ya fedha, biashara na sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni utekelezaji kisheria wa hatua kadhaa za mfumo wa kodi, ushuru na ada mbalimbali zilizobainishwa katika hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2008/2009 iliyowasilishwa Bungeni tarehe 12 Juni, 2008 na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Aidha, Muswada huu unakusudia kuzifanyia marekebisho Sheria Kumi na Tisa zinazohusu masuala ya fedha, kodi na ushuru kwa lengo la kuweka, kurekebisha au kufuta viwango vya kodi, ushuru na ada mbalimbali na pia kuweka utaratibu utakaowezesha Serikali kukusanya mapato kutoka kwa wakala, mamlaka na asasi za Serikali zinazotoza kodi ya huduma ili kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kama nilivyobainisha wakati nikiwasilisha hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2008/2009, ni dhahiri upo umuhimu wa Taasisi na Wakala za Serikali na Mamlaka mbalimbali zinazotoza kodi ya huduma nazo kuweza kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zinazohusika na marekebisho haya ni kama ifuatavyo, Sheria ya Mamlaka ya Masoko ya Dhamana na Mitaji, Sura 273; Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Utoaji wa Huduma za Maji, Nishati na Bidhaa za Petroli Sura 414; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147; Sheria ya Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41; Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332; Sheria ya Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Serikali za Mitaa, Sura 407; Sheria ya Magari (Kodi ya Usajili na Uhamisho wa Umiliki wa Magari), Sura 124; Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Sura 284; Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura 282; Sheria ya Mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya Umma, Sura 372; Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma, Sura 371; Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410; Sheria ya Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali Sura 51; Sheria ya Bandari, Sura 166; Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura 413; Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Anga, Sura 80; Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Huduma ya Mawasiliano Sura 172; Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora wa Chakula, Madawa na Vipodozi, Sura 219 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya Muswada. Muswada huu umegawanyika katika sehemu Ishirini. Sehemu ya kwanza, inahusu masuala ya utangulizi, kama vile jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Muswada, sehemu ya pili inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Mamlaka ya Masoko ya Dhamana na Mitaji, Sura 273 kwa kuongeza kifungu kipya cha 9A ili kuwezesha utekelezaji wa matakwa ya kifungu cha 5(3) cha sheria mama ya Usimamizi wa Fedha za Umma Sura 348 kwa kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kufanya maamuzi kuhusu kiwango cha mchango wa mapato ya Mamlaka ya Masoko ya Dhamana na Mitaji kitakachochangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali na kiasi kitakachobaki kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka hii, sehemu ya tatu, kwa kuzingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Fedha na Uchumi wakati wakijadili Muswada huu, Serikali imeondoa Shirika la *DAWASA* katika orodha ya mamlaka zinazopaswa kuchangia kiasi cha mapato yake kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Zingatio hili limetokana na huduma muhimu zinazotolewa na mamlaka hii kwa wananchi ili kuiwezesha *DAWASA* kujiimarisha katika kutoa huduma muhimu ya maji. *(Makofi)*

Aidha, kufuatia hatua hii, sehemu ya tatu kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 49 cha Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Utoaji wa Huduma za Maji, Nishati na Bidhaa za Petroli Sura 414 kwa kuongeza kifungu

kipya cha 49A ili kuwezesha Waziri mwenye dhamana na mamlaka hii baada ya kuridhia Bajeti ya mwaka au Bajeti ya nyongeza ya Mamlaka, kuiwasilisha Bajeti husika kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kwa ajili ya idhini. Chini ya marekebisho haya Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha atabainisha kuhusu kiwango cha mapato ya mamlaka kitakachochangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali na kiasi cha fedha kitakachobaki kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 katika vifungu namba 124, na Jedwali la Nne kama ifuatavyo:

Kwanza, kurekebisha Kifungu cha 124(2) ili kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa katika huduma za simu za mkononi kutoka asilimia 7 ya sasa ya gharama ya matumizi ya huduma hadi kiwango cha asilimia 10 ya gharama ya matumizi ya huduma sanjari na mfumuko wa bei *(inflation).*

Pili, kurekebisha Jedwali la Nne kama ifuatavyo; kwanza kurekebisha, kwa asilimia 12 viwango vya Ushuru wa Bidhaa kwa bidhaa zinazotozwa ushuru huu kwa viwango maalumu isipokuwa kwa bidhaa za mafuta ya petroli. Viwango vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo; vinywaji baridi, kutoka shilingi 48 kwa lita hadi shilingi 54 kwa lita; bia nyingine zote, kutoka shilingi 294 kwa lita hadi shilingi 329 kwa lita; mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25, kutoka shilingi 940 kwa lita hadi shilingi 1,053 kwa lita; bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa, kutoka shilingi 173 kwa lita hadi shilingi 194 kwa lita; vinywaji vikali, kutoka shilingi 1,394 kwa lita hadi shilingi 1,561kwa lita na kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara kama ifuatavyo, sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 4,775 hadi shilingi 5,348 kwa sigara elfu moja; sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 11,266 hadi shilingi 12,618 kwa sigara elfu moja; sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 20,460 hadi shilingi 22,915 kwa sigara elfu moja; tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara *(cut filler)* kutoka shilingi 10,333 hadi shilingi kwa 11,573 kwa kilo na ushuru wa Bidhaa kwa *Cigar* unabaki kuwa asilimia 30. *(Makofi)*

Pili, kupunguza kiwango cha sasa cha Ushuru wa Bidhaa kwenye mafuta mazito *(HFO)* kutoka shilingi 117 kwa lita hadi shilingi 97 ili kupunguza gharama ya uzalishaji viwandani na hivyo kuongeza uwezo wa ushindani wa bidhaa zinazozalishwa nchini katika soko.

Tatu, kuweka ushuru wa bidhaa wa asilimia 120 kwa mifuko yote ya plastiki pasipo kuzingatia aina ya mifuko hii ili kupunguza uchafuzi wa mazingira. Hivi sasa mifuko ya plastiki isiyoruhusiwa hutozwa ushuru wa bidhaa wa asilimia 120 na ile inayoruhusiwa hutozwa asilimia 0. Hatua hii ni utekelezaji wa uamuzi wa nchi za Umoja

wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo nchi za Kenya na Uganda zimekwisha tekeleza.

Nne, kutoa ufafanuzi wa kiforodha kuhusu utambuzi wa aina ya magari kwa kuzingatia ujazo wa injini. Kurekebisha mfumo wa kutoza ushuru wa bidhaa kwenye magari kutoka mfumo wa sasa wa kutoza ushuru wa asilimia 10 kwa magari yenye ujazo wa injini unaozidi *CC 2000* na kuwa na viwango viwili vya asilimia 5 na asilimia 10 ili kupanua wigo wa utozaji wa ushuru wa bidhaa kwenye magari kama ifuatavyo, kwanza magari yenye ujazo wa injini unaozidi *CC 1000* lakini hauzidi *CC 2000* yatakuwa na kiwango cha ushuru wa bidhaa cha asilimia 5 ya thamani ya gari. Hivi sasa magari haya hayatozwi ushuru wa bidhaa. Pili, magari yenye ujazo wa injini unaozidi *CC 2000* yataendelea kutozwa kiwango cha ushuru wa bidhaa cha asilimia 10 ya thamani ya gari kama ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41 kwa kuongeza kifungu kipya cha 64A ili kuwezesha utekelezaji wa matakwa ya kifungu 5(3) cha Sheria ya Fedha za Umma Sura ya 348 kwa kumpa uwezo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuamua kiwango cha mapato kitakachochangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili maendeleo ya Taifa na kiasi cha fedha kitakachobaki kwa ajili ya kugharamia shughuli za chombo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya sita, kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 kama ifuatavyo, kwanza, kifungu cha 3 kwa kufuta tafsiri ya neon *turnover* na kutoa tafsiri mpya ili kubainisha katika tafsiri hii kwamba mapato ya mwaka kwa kampuni zitakazoonyesha kupata hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo yanatozwa kodi, pili, katika kifungu cha 4; kwanza kwa kurekebisha kifungu kidogo cha kwanza kwa kufuta aya (a) na kuiandika upya ili kubainisha kwamba kodi ya mapato itatozwa katika mapato ya mwaka kwa kampuni zitakazoonyesha kupata hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Pili, kurekebisha kifungu kidogo cha 3 kwa kufuta aya namba (a) na kuiandika upya ili kubainisha kuwa kiwango cha kodi kitakachotozwa kwa kampuni zitakazoonyesha kupata hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo ni kama kilivyobainishwa katika aya ya 3(3) ya jedwali la kwanza la sheria ya Kodi ya Mapato ambapo kiwango cha asilimia 0.3 ya mauzo ghafi *(gross turnover)* kitatozwa katika mwaka wa tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho haya ni kutoza kodi kwa kampuni zitakazoonyesha kupata hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo ili kampuni hizi zichangie katika huduma za maendeleo. Uzoefu umeonyesha kwamba kampuni hizi hupata faida ya kibiashara lakini katika kukokotoa faida inayostahili kulipiwa kodi, hujikuta zinaonyesha hasara *(tax loss)* kutokana na vivutio vya uwekezaji ikiwemo viwango vikubwa vya punguzo la gharama za mitaji *(capital expenditure)* vilivyowekwa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuongeza kifungu kidogo kipya cha 8 ili kutohusisha kampuni zilizowekeza katika miradi ya kilimo, elimu na afya katika

utaratibu wa kulipa kodi ya mapato ya asilimia 0.3 itakayotozwa kwa kampuni zitakazoonyesha kupata hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kurekebisha kifungu cha 83 kwa kuongeza kifungu kipya cha 83A ili kutoza kodi ya zuio *(withholding tax)* kwa kiwango cha asilimia mbili kwa malipo ya Serikali kutokana na ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka kwa wazabuni wasiosajiliwa chini ya utaratibu wa *TIN*. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba wafanyabiashara hawa wanalipa kodi na hivyo kuchangia huduma zinazotolewa na Serikali. Tatu, kurekebisha kifungu cha 117 kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha 10 ili kuipa Mamlaka ya Mapato Tanzania nguvu za kisheria kukusanya deni la mlipa kodi kutoka kwa wakala wake endapo wakala huyo katika kipindi cha siku 30 atashindwa kutekeleza wajibu wake kisheria wa kukusanya kodi husika kutoka kwa mlipa kodi na kuiwasilisha kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato. Lengo la marekebisho haya ni kuwawezesha mawakala wa walipa kodi kuwajibika ipasavyo kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Nne, kurekebisha kifungu cha 127 kwa kufuta aya namba (a ) na (b ) na kukiandika upya kifungu hiki ili kumpa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kukasimu madaraka yake kwa mameneja wa mikoa ili kuwawezesha kutoa adhabu baada ya mlipa kodi kukiri kosa. Hivi sasa kifungu hiki hakiruhusu Kamishna Mkuu kukasimu madaraka haya, tano, kurekebisha Jedwali la Kwanza aya ya kwanza kwa kupandisha kiwango cha sasa cha mapato kisichotozwa kodi kutoka shilingi 80,000/= kwa mwezi hadi shilingi 100,000/= kwa mwezi. Lengo la marekebisho haya ni kubadilisha mfumo wa sasa wa utozaji kodi binafsi ya mapato ili uwiane na kima cha chini cha mshahara cha Serikali kwa mwaka 2008/2009 na kulinda mapato binafsi dhidi ya athari ya mfumuko wa bei. *(Makofi)*

Aidha, kwa mapato yanayoanzia shilingi 100,001/= hadi zaidi ya shilingi 720,000/= kiwango cha kodi kitakuwa ni kuanzia asilimia 15 hadi 30 kulingana na mchanganuo ulioainishwa katika jedwali lililobainishwa katika aya ya kifungu cha 19 cha Muswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kurekebisha aya ya 1(t) ya Jedwali la Pili kwa kuongeza aya mpya ya 1(u) ili kutoa msamaha wa kodi ya mapato kwenye faida itokanayo na mauzo ya mitaji *(capital gains tax)* kwa vipande kutoka katika mfuko wa uwekezaji wa pamoja ulioidhinishwa. Lengo la hatua hii ni kuweka ushindani sawa wa kibiashara kwa kuipa mifuko ya uwekezaji wa vipande unafuu wa kodi kama ilivyo kwa uwekezaji wa amana ambao hautozwi kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya saba kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Serikali za Mitaa, Sura 407 kwa kuongeza kifungu kipya cha 4A vifungu vidogo vya (1), (2), (3), (4) na (5) ili kwanza, kubainisha kwamba Mfuko wa *LAPF* utakuwa wakala wa Serikali kwa ajili ya kuwalipa mafao wastaafu wa Serikali za Mitaa ambao wametumikia pia Serikali Kuu katika utumishi wao na ambao ni wanachama wa *LAPF*. Hivi sasa wastaafu hawa wanalipwa sehemu ya mafao yao Hazina na sehemu nyingine wanalipwa na *LAPF*.

Mafao wanayostahili kutoka Serikali Kuu na ambayo wanapokea kupitia Hazina ndiyo yatahamishiwa na kulipwa na *LAPF*. Lengo la marekebisho haya ni kuwapunguzia kero wastaafu. *(Makofi)*

Pili, kubainisha kwamba Serikali italipa ada ya uwakala na gharama za awali kwa *LAPF* na kiwango au kiasi cha ada hiyo kitaainishwa katika mkataba wa uwakala baina ya Serikali na *LAPF*. Aidha, katika kila kipindi cha mwezi mmoja au miezi mitatu, Serikali itakuwa inawasilisha fedha za mafao ya wastaafu hao katika Mfuko wa *LAPF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nane, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye jedwali la kwanza la Sheria ya Magari (Kodi ya usajili na uhamisho wa umiliki wa magari), Sura 124 kama ifuatavyo, kwanza kurekebisha aya ya 3 ili kuongeza viwango vya ada ya usajili wa magari kutoka shilingi 90,000/= ya sasa hadi shilingi 120,000/= na pili, kuongeza aya mpya ya 4 ili kuweka ada ya usajili wa pikipiki ya shilingi 35,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 9 na 10 kama zilivyorekebishwa kwa ujumla zinafanyia marekebisho sheria za Mamlaka ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro pamoja na Hifadhi za Taifa ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuamua kiwango cha mapato ya mamlaka hizi kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tisa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro, Sura 284 kwa kuongeza kifungu kipya cha 13A ili kubainisha kwamba baada ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya maliasili kuridhia Bajeti ya mwaka au ya nyongeza ya Mamlaka hii, ataiwasilisha Bajeti husika kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kwa ajili ya kupata idhini.

Aidha, Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha amepewa uwezo wa kubainisha kiwango cha mapato ya Mamlaka hii kitakachochangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya Taifa na kiasi cha fedha kitakachobaki kwa ajili ya kugharamia shughuli za mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kumi inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura 282 kwa kuongeza kifungu kipya cha 10A ili kwanza, kubainisha kwamba baada ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya utalii kuridhia Bajeti ya mwaka au Bajeti ya nyongeza, ataiwasilisha Bajeti husika kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kwa ajili ya kupata idhini. Aidha, Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha atabainisha kiwango cha mapato kitakachochangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kiasi cha fedha kitakachobaki kwa ajili ya kugharamia shughuli za mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 11, 12 na 14 kama zilivyorekebishwa zinafanyia marekebisho Sheria ya Mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya Umma Sura 372, Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma, Sura 371 na Sheria ya Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini Sura 51, ili kuwezesha Mifuko ya *PPF*, *PSPF* na *GEPF* kulipa

wastaafu wa Serikali mafao ya pensheni kama wakala wa Serikali. Lengo la hatua hii ni kuwapunguzia kero wastaafu. Aidha, marekebisho husika ni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kumi na moja inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya Umma, Sura 372 kwa kuongeza kifungu kipya cha 6A (1), (2) ,(3) (4) na (5 ) ili kwanza, kubainisha kwamba Mfuko wa *PPF* utakuwa wakala wa Serikali kwa ajili ya kulipa mafao ya pensheni kwa wastaafu walioorodheshwa katika daftari la pensheni na wanaopokea malipo ya pensheni ya kila mwezi, ambao walistaafu kabla ya tarehe 1 Julai, 2004; wastaafu ambao walilipwa mafao yao kwa mkupuo na kurejeshwa upya kwenye daftari la pensheni na watumishi walioajiriwa katika Taasisi za Serikali na wanaochangia katika mfuko huu ambapo hapo awali walikuwa wameajiriwa katika utumishi Serikalini. *(Makofi)*

Pili, kubainisha kwamba Serikali italipa ada ya uwakala na gharama za awali kwa *PPF* na kiwango au kiasi cha ada hiyo kitaainishwa katika mkataba wa uwakala baina ya Serikali na *PPF*. Aidha, Serikali itawasilisha fedha za mafao ya wastaafu waliohamishiwa *PPF* katika kila kipindi cha mwezi mmoja au miezi mitatu. *(Makofi)*

Sehemu ya kumi na mbili inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma, Sura 371 kwa kuongeza kifungu kipya cha 31A(1), (2), (3) na (4) ili kuuwezesha Mfuko wa *PSPF* kuwa wakala wa Serikali kwa ajili ya kulipa mafao ya pensheni kwa wastaafu wa Serikali. Chini ya utaratibu huu *PSPF* itashughulikia makundi yafuatayo, kwanza, wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Usalama wa Taifa *(TISS)*, pili, watumishi wa Serikali waliostaafu au kufariki kabla ya tarehe 1 Julai, 2004 ambao bado hawajalipwa mafao yao (kwa kuzingatia kwamba Sheria hii inashughulikia wastaafu walio chini ya utaratibu wa kuchangia pensheni ambao ulianza rasmi tarehe 1 Julai, 2004 na tatu, viongozi ambao wamestaafu na wenye stahili ya kulipwa pensheni sawa na 80% ya mshahara wa kiongozi wa ngazi husika aliyepo madarakani kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na kadhalika. *(Makofi)*

Aidha, marekebisho haya yamebainisha kwamba Serikali italipa ada ya uwakala na gharama za awali kwa *PSPF* na kiwango au kiasi cha ada hiyo kitaainishwa katika mkataba wa uwakala baina ya Serikali na *PSPF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itawasilisha fedha za mafao ya wastaafu waliohamishiwa *PSPF* katika kila kipindi cha miezi mitatu au mwezi mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kumi na tatu, kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 25 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 kwa kuongeza kifungu kipya cha 25A ili kuwezesha utekelezaji wa matakwa ya kifungu 5(3) cha Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 kwa kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuamua kiwango cha mapato ya mamlaka hii kitakachohamishiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kumi na nne kama ilivyorekebishwa inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini, Sura 51 kwa kuongeza kifungu kipya cha 3A(1) ,(2),(3) na (4) ili kwanza, kubainisha kwamba Mfuko wa *GEPF* utakuwa wakala wa Serikali katika kuwalipa mafao wastaafu wafuatao, wastaafu wa Jeshi la Polisi na Magereza ambao hawakuchangia kwenye Mfuko huu kabla ya Julai, 1999 na ambao mafao yao yatalipwa na Hazina; walimu walioajiriwa kwa mkataba, viongozi wa kisiasa kama Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wilaya pamoja na wastaafu wengine walioajiriwa kwa mikataba Serikalini. *(Makofi)*

Pili, kubainisha kwamba Serikali italipa ada ya uwakala na gharama za awali kwa *GEPF* na kiwango au kiasi cha ada hiyo kitaainishwa katika mkataba wa uwakala baina ya Serikali na *GEPF*. Aidha, Serikali itawasilisha fedha za mafao ya wastaafu waliohamishiwa *GEPF* katika kila kipindi cha mwezi mmoja au miezi mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 15, 16, 17, 18 na 19 kama zilivyorekebishwa kwa ujumla zinafanyia marekebisho sheria za wakala mbalimbali wa Serikali ili kuwezesha utekelezaji wa matakwa ya kifungu namba 5(3) cha Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 kwa kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuamua kuhusu kiwango cha mapato ya mamlaka hizi kitakachohamishiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kumi na tano inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 74 cha Sheria ya Bandari, Sura 166 kwa kuongeza vifungu vidogo vipya vya (4) na (5) ili kwanza kubainisha kwamba baada ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya bandari kuridhia Bajeti ya mwaka au Bajeti ya nyongeza ya mamlaka hii, ataiwasilisha Bajeti husika kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha ili kupata idhini. Pili, kifungu hiki kinampa uwezo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuamua kuhusu kiwango cha mapato ya mamlaka hii kitakachohamishiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kiasi cha fedha kitakachobaki kwa ajili ya kugharamia shughuli za Mamlaka ya Bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kumi na sita inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 47 cha Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura 413 kwa kuongeza vifungu vidogo vipya vya (6) na (7) ili kwanza, kubainisha kwamba baada ya Waziri mwenye dhamana na mamlaka hii kuridhia Bajeti ya mwaka au ya nyongeza, Waziri husika ataiwasilisha Bajeti husika kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha ili kupata idhini.

Pili, kifungu hiki kinampa uwezo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuamua kuhusu kiwango cha mapato ya mamlaka hii kitakachotolewa kama mchango kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kiasi cha fedha kitakachobaki kwa ajili ya kugharamia shughuli ya mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kumi na saba, inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 47 cha Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa

Anga, Sura 80 kwa kuongeza vifungu vidogo vipya vya (6) na (7) ili kwanza, kubainisha kwamba baada ya Waziri mwenye dhamana na usimamizi wa usafiri wa anga kuridhia Bajeti ya mwaka au ya nyongeza ya mamlaka hii, ataiwasilisha Bajeti husika kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha ili kupata idhini.

Pili, kifungu hiki kinampa uwezo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuamua kuhusu kiwango cha mapato ya mamlaka hii kitakachochangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kiasi cha fedha kitakachobaki kwa ajili ya kugharamia shughuli za mamlaka hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kumi na nane, inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 54 cha Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Huduma ya Mawasiliano Sura 172 kwa kuongeza vifungu vidogo vipya vya (6) na (7) ili kwanza, kubainisha kwamba baada ya Waziri mwenye dhamana na Mamlaka hii kuridhia Bajeti ya mwaka au ya nyongeza ya mamlaka ataiwasilisha Bajeti husika kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha ili kupata idhini. Pili, kifungu hiki kinampa uwezo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuamua kuhusu kiwango cha mapato ya mamlaka kitakachochangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kiasi cha fedha kitakachobaki kwa ajili ya kugharamia shughuli za mamlaka hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kumi na tisa, inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 7 Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora wa Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219 kwa kuongeza kifungu kipya cha 4A ili kuwezesha utekelezaji wa matakwa ya kifungu 5(3) cha Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 kwa kumpa uwezo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuamua kiwango cha mapato ya mamlaka hii kitakachohamishiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kiasi kitachobaki kwa ajili ya matumizi ya mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya ishirini kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kama ifuatavyo, kwanza kubainisha kuwa marekebisho yaliyofanyika kupitia kifungu cha 49 cha Muswada huu kuhusu hatua ya Serikali ya kupanua wigo wa huduma zinazotozwa kiwango cha asilimia sifuri ya Kodi ya Ongezeko la Thamani zinapokuwa zimetolewa kwa watumiaji wa nje ya nchi *(export of services),* itaanza kutumika rasmi tarehe 1 Januari, 2009 ili kutoa fursa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuandaa kanuni za usimamizi. *(Makofi)*

Pili, kurekebisha Jedwali la Kwanza (linalohusu bidhaa na huduma zinazotozwa kodi kwa kiwango cha sifuri) kwanza, kufuta (*notes*) zinazojitokeza baada ya aya ya pili ya Jedwali hili na kuiandika upya ili kupanua wigo wa huduma zinazotozwa kiwango cha asilimia sifuri ya kodi ya Ongezeko la Thamani zinapokuwa zimetolewa kwa watumiaji wa nje ya nchi ili kuhusisha huduma zifuatazo, ushauri wa kitaalam; huduma za mawasiliano ya simu; huduma zinazohusu mali zisizohamishika; huduma za kurusha matangazo ya redio na luninga; huduma zinazotolewa na wakala na huduma saidizi za uchukuzi na usafirishaji bidhaa *(the supply of ancillary transport activities). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu kuongeza aya mpya ya 13 ili kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwa magunia yanayotengenezwa hapa nchini na nne, kurekebisha Jedwali la Pili, (linalohusu bidhaa na huduma zilizosamehewa kodi *(exempt supplies and imports)* kwanza, kuongeza aya ya 12(4) ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye lami *(bitumen)* ili kupunguza gharama za matengenezo ya barabara na pili, kuongeza aya ya 25 ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mafuta mazito yanayotumika kama nishati ya kupikia ili kuhamasisha wananchi kutumia mafuta hayo badala ya kuni na mkaa kwa matumizi ya nyumbani na hivyo kulinda mazingira.

Aidha, katika Jedwali la marekebisho yamefanyika marekebisho kwa kuondoa maneno moto poa ili kuweka sahihi dhana iliyokusudiwa ya kusamehe bidhaa *(product)* ya mafuta badala ya kusamehe kampuni ili kuwezesha makampuni mengine yatakayoingiza bidhaa ya aina hii nayo yaweze kusamehewa kodi. *(Makofi)*

Tatu, kuongeza aya ya 26 ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye gesi asilia iliyosindikwa *(Compressed Natural Gas - CNG)* na mitungi ya kuhifadhia gesi hiyo, kama ilivyo hivi sasa kwa gesi ya kupikia ya *LPG* ili kuhamasisha matumizi ya gesi hiyo badala ya mafuta ambayo ni ghali au mkaa ili kulinda mazingira. *(Makofi)*

Nne, kuongeza aya ya 31 kama ilivyobainishwa katika jedwali la marekebisho ili kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa huduma za kuandaa mashamba, kukata, kupakia na kusafirisha miwa kwenda viwandani itakayotolewa na Umoja au Chama cha Wakulima kilichosajiliwa kwa wanachama wa umoja au chama husika. Uamuzi huu umezingatia hali halisi kuwa bidhaa inayozalishwa kutokana na miwa yaani sukari inatozwa *VAT* tofauti na bidhaa nyingine zinazozalishwa kutokana na mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali la tatu, kwanza, kurekebisha aya ya 2 kwa kuongeza aya mpya ya 2(2) ili kumpa uwezo Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuamua kuhusu idadi ya magari *(non utility vehicles)* yanayopaswa kupata msamaha wa Kodi chini ya kifungu cha 2(1) cha Sheria hii kutokana na mpango kazi wa mradi utakaowasilishwa kwake. *(Makofi)*

Pili, kurekebisha aya ya 10(1) ili kubainisha kuwa msamaha unaotolewa chini ya aya hii hautahusisha bidhaa za matumizi ya nyumbani na bidhaa au huduma ambazo ni mahsusi kwa matumizi ya kazi za kila siku za kiofisi kwa Taasisi zisizo za Kiserikali *(NGO's).* Aidha, katika jedwali la marekebisho, yamefanyika marekebisho ya kiuandishi ili kutohusisha taasisi za kidini na utaratibu huu. *(Makofi)*

Tatu, kuongeza aya ndogo za 10( 5), 10(6) na 10(7) ili kubainisha kuwa msamaha utatolewa kwa Taasisi zisizo za Kiserikali *(NGO's)* kufuatana na masharti yafuatayo, kwanza kuwasilisha uthibitisho kuwa bidhaa au huduma zitakazosamehewa kodi zitatumika mahsusi kwa ajili ya mradi husika na si vinginevyo, pili, Taasisi zisizo za Kiserikali *(NGO's)* zitapaswa kuwasilisha taarifa za mipango kazi yao ya kila mwaka

itakayobainisha miradi wanayokusudia kuitekeleza kabla ya kuanza kwa mwaka fedha wa Serikali na tatu kuwasilisha taarifa ya namna misamaha husika ilivyotumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kufuta aya ya 11 ambayo inatoa msamaha wa kodi kwa Taasisi zisizo za Kiserikali *(NGO's).* Taasisi hizi tayari zinapata msamaha chini ya aya namba 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kufuta aya ya 17 ili kufuta msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa huduma na bidhaa zitakazotumika na kampuni za *AES Tanzania Services Limited, Pan African Energy Tanzania Limited, Ocelot International Tanzania Limited* na *Songas Limited* ambazo zinahusika na mradi wa Gesi ya Songosongo. Hatua hii imechukuliwa baada ya mradi huu kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, kufuta aya ya 20 ili kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa bidhaa za kufungashia maziwa zitakazotumika na viwanda au watu wanaotengeneza maziwa kwa kuwa msamaha huu hauwanufaishi wananchi ambao ndio walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, kuongeza aya mpya ya 30 ili kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye *Ethanol, dyienstuff* na zitakazoagizwa na kampuni za ndani kwa ajili ya kutengeneza mafuta mazito ya nishati. Aidha, aya hii pia imefanyiwa marekebisho kwa kuondoa rejea ya maneno moto poa ili msamaha huu uweze kunufaisha kampuni nyingine zitakazoagiza bidhaa ya aina hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inapendekezwa pia kufanyia marekebisho jedwali la tatu kwa kurejesha aya ya 18 na 22 za jedwali hili ambazo zinatoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa bidhaa zinazoagizwa na viwanda vya kutengeneza dawa za binadamu na miwani. Lengo la hatua hii ni kutoathiri uzalishaji wa dawa nchini ambayo kwa kiasi kikubwa yanatumika na wananchi wa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba baadhi ya hatua zilizobainishwa katika hotuba ya Bajeti zimetekelezwa na Mawaziri husika kupitia Tangazo la Serikali *(Government Notice)* kwa mujibu wa matakwa ya sheria. Hatua hizo ni pamoja na kupunguza viwango vya ada ya mwaka ya leseni za magari ambapo baada ya kufanya marekebisho wakati Waziri wa Fedha na Uchumi alipofanya majumuisho ya hotuba ya Bajeti kwa mwaka 2008/2009, Waziri mwenye dhamana na masuala ya usalama barabarani alitoa Tangazo la Serikali Namba 94 la tarehe 27 Juni, 2008 ili kubainisha viwango hivyo kama ifuatavyo, ukubwa wa injini usiozidi cc 500 kiasi kilichopendekezwa wakati wa kusoma Bajeti ni shilingi 30,000/= na kiasi kilichopendekezwa wakati wa majumuisho ni shilingi 30,000/=. Ukubwa wa injini cc 501 hadi cc 1500 kiwango kilichopendekezwa wakati wa kusoma Bajeti ni shilingi 50,000/= na kiwango kilichopendekezwa wakati wa majumuisho ni shilinngi 50,000/=.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukubwa wa injini cc 1501 hadi cc 2500, kiwango kilichopendekezwa wakati wa kusoma Bajeti ni shilingi 120,000/= na kiwango kilichopendekezwa wakati wa majumuisho ni shilingi 100,000/=. Pia ukubwa wa injini cc

2501 hadi cc 5000 kiwango kilichopendekezwa wakati wa kusoma Bajeti ni shilingi 140,000/= na kiwango kilichopendekezwa wakati wa majumuisho ni shilingi150,000/= na kwa kubwa wa injini unaozidi cc 5000 kiwango kilichopendekezwa wakati wa kusoma Bajeti ni shilingi 150,000/= na kiwango kilichopendekezwa wakati wa majumuisho ni 150,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikiwasilisha hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Serikali ilipendekeza kuondolewa kwa ushuru wa forodha unaotozwa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya kula yanayoagizwa na wenye viwanda wa hapa nchini. Hatua hii ilikusudia kuviongezea uwezo viwanda vya hapa nchini kukabiliana na ushindani kutoka kwa wazalishaji wengine wa bidhaa hizo katika eneo la Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo ushuru huo hautozwi kwa kuzingatia viwango vinavyokubaliwa na nchi hizo, yaani *Common External Tariff*. Kufuatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge wengi wakati wa kuhitimisha mjadala kuhusu Bajeti mnamo tarehe 20 Juni, 2008, niliahidi kukutana na wadau wa mafuta ya kula ili kujadili pendekezo hili la Serikali pamoja na hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika mjadala wa Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mkutano wa wadau wa mafuta ya kula ulifanyika hapa mjini Dodoma tarehe 25 Julai, 2008. Mkutano huu ulishirikisha wakulima wa mbegu za mafuta na wenye viwanda vya kusindika mafuta ya kula yanayotokana na mawese. Aidha, kwa kuzingatia hoja zilizotolewa na wadau, Serikali imeamua kwamba kwanza, Tanzania iendelee kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 kwa mafuta ghafi ya kula yanayoagizwa kutoka nje, pili, Serikali itafanya utafiti kubaini mahitaji halisi ya Taifa ya mafuta ya kula na mazingira ya kuzalisha mbegu zaidi, kwa kuwa hadi sasa utafiti uliopo umeonyesha kwamba hakuna mafuta ghafi yanayoagizwa kutoka nje ya nchi badala yake mafuta yanayoagizwa kutoka nje yanakuwa tayari yamepitia hatua kadhaa za usindikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa masuala ya kodi ya ushuru wa forodha husimamiwa na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, hatua hii ya Serikali itabainishwa kupitia notisi itakayotolewa chini ya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, kama nilivyoeleza hapo awali, mengi ya marekebisho ninayopendekeza ni utekelezaji kisheria wa mapendekezo ya Serikali kuhusu Bajeti ya mwaka wa fedha 2008/2009 ambayo tayari yameridhiwa na Bunge hili wakati wa kuhitimisha hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Kwa hiyo, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye mkubali kuupitisha ili kuhalalisha kisheria Bajeti iliyokwishapitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Unanikumbusha kwenye mkutano mmoja wa siasa anasema nipigie makofi wee mpaka nitakapokaa. *(Kicheko)*

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kutoa maoni ya Kamati yangu juu ya Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2008 kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Bunge Toleo la mwaka 2007 Kamati iliupitia na kuuchambua Muswada huu wa sheria na hatimaye kutoa maoni na mapendekezo kwa Serikali juu ya Muswada huu. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati imetekeleza jukumu hilo na hatimaye Muswada huu kuletwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Muswada, tarehe 12 Juni, 2008 Waziri wa Fedha na Uchumi alipowasilisha Bajeti alipendekeza kupandishwa au kushushwa ada, ushuru na kodi mbalimbali pamoja na hoja kadhaa walizotoa Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, Muswada huu unakuja kutokana na hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha kuhusu ushuru, kodi na ada mbalimbali ambazo amepanga kuzitoza katika mwaka huu wa fedha. Kama wote tunavyofahamu, ili aweze kufanya hivyo ni lazima kuwepo na nguvu ya kisheria inayompa mamlaka hayo. Muswada huu unalenga kufanya marekebisho mbalimbali katika sheria mbalimbali ili kumpa Waziri wa Fedha mamlaka ya kisheria kutimiza yale aliyoahidi katika hotuba yake ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inampongeza Waziri wa Fedha kwa kuzingatia sehemu kubwa ya ushauri waliotoa Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia hotuba ya Bajeti na kwa mujibu wa ahadi alizotoa wakati akihitimisha hoja ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2008/2009 aliyoitoa tarehe 12 Juni, 2008. Michango mingi ya Wabunge imepelekea mabadiliko kadhaa katika Muswada huu yote ikiwa na lengo la kuboresha sheria na kuboresha maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii inakusudia kufanya marekebisho katika sheria ishirini zihusuzo masuala ya fedha, kodi na ushuru kwa lengo la kuweka, kurekebisha ama kufuta viwango vya kodi, ushuru na ada mbalimbali na pia kuweka utaratibu utakaowezesha Serikali kukusanya mapato kutoka wakala, mamlaka na taasisi za Serikali zinazotoza kodi ya huduma ili kuchangia katika mfuko Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati, lengo la maoni yaliyotolewa na wajumbe wa Kamati ni kuboresha sheria tajwa ikiwa ni pamoja na kupunguza makali sehemu ambazo zingepelekea kuongeza makali ya maisha kwa wananchi wa kipato cha chini. Kamati ilijadili maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa

mabadiliko kisheria ili utekelezaji wake ufanyike. Maeneo yaliyoguswa kupitia marekebisho ya sheria kadhaa, yamejielekeza katika kuweka utaratibu utakaowezesha Serikali kukusanya mapato kutoka wakala, mamlaka na asasi za Serikali zinazotoza kodi ya huduma ili kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,yapo marekebisho yanayohusiana na Sheria ya Fedha za Umma, sura 348 ya kumpa uwezo Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kufanya maamuzi kuhusu kiwango cha mapato ya mamlaka zifuatazo kitakachohamishiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ili kuchangia maendeleo ya Taifa, Mamlaka ya Dhamana na Mitaji, *SUMATRA*, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam, Mamlaka ya kusimamia Utoaji wa Huduma za Maji, Nishati na Bidhaa za Petroli, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Manunuzi ya Umma, Bandari, *SUMATRA* na Shirika la Chakula na Dawa ( *TFDA*). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imekubaliana na marekebisho haya kwa kuzingatia yafuatayo, kwanza upo umuhimu mkubwa wa Wizara husika kufanya majadiliano ya kina *(deep consultations)* na Mamlaka hizi ili kuondoa dhana ya kuipa nguvu kubwa Wizara ya Fedha na hivyo kuleta migongano baina ya viongozi wa Wizara wanaosimamia Mamlaka hizo na Wizara ya Fedha. Ni vyema maamuzi ya kifedha yatakayotolewa kuhusu viwango vya kuhamishiwa Mfuko Mkuu wa Serikali, yapate kibali *(consent)* au yakubalike na Wizara husika pamoja na viongozi wa Mamlaka husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili Kamati inatoa tahadhari kwa Wizara kuzingatia utekelezaji mzuri wa utaratibu huu, ili baadaye usije ukawa ni mwanzo wa kudumaza jitihada za kujiongezea mapato kwa mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ipo haja ya kuweka utaratibu mzuri wa kuhakiki kama ni kweli taasisi imepata hasara au faida ili kuepusha taarifa zisizo sahihi za utekelezaji *(under declaration)* na nne, bado ipo haja kubwa ni kuweka bayana vigezo vipi vitakavyotumika kubaini viwango vya fedha vitakavyohamishwa kutoka vyombo hivi kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuandaa utaratibu mzuri katika kanuni ambao utatoa mwongozo wa jinsi Serikali itakavyokuwa ikikusanya mapato toka katika taasisi na mamlaka zilizotajwa katika sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Kamati inaikumbusha Serikali kuwa si kiasi chote cha ziada ya mapato ya mamlaka hizi kichukuliwe kwenye Mfuko Mkuu. Kama Serikali ilivyofafanua kwenye majadiliano ya Kamati, ichukuliwe sehemu tu ya mapato hayo ili kubakisha kiasi kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu pia unampa kazi ya ziada Waziri wa Fedha kupitia na kuthibitisha Bajeti za mamlaka zilizotajwa na sheria hii. Kamati inadhani hili si jukumu la msingi kwa Waziri wa Fedha. Jukumu hili Kamati inasisitiza aachiwe Waziri mwenye dhamana ya mamlaka hiyo, ili kuepusha migongano isiyo ya

lazima baina ya Waziri wa Fedha na Mawaziri wa Mamlaka husika. Kwa hali yoyote ile hali hii itapunguza tija na ufanisi wa zoezi zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kukubaliana na marekebisho hayo, Kamati iliishauri Wizara kuiondoa *DAWASA* katika utaratibu huu kutokana na matatizo inayokumbana nayo katika kuboresha ugavi wa maji katika Jiji la Dar es Salaam. Serikali imeafiki ushauri wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza uamuzi wa Serikali kutumia Mifuko yetu ya Pensheni na Hifadhi za Jamii nchini kuwa wakala wa Serikali kwa ajili ya kuwalipa wastaafu pensheni zao, *LAPF* kuwalipa wastaafu wa Serikali za Mitaa, mfuko wa *PPF* na ule wa *PSPF* kulipa wastaafu wa Serikali mafao yao ya uzeeni. Utaratibu huu kwa hali yoyote ile ukitekelezwa kwa umakini utaongeza ufanisi katika eneo hili ambalo limekuwa na linaendelea kulalamikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema utaratibu huu ukaainishwa vyema, mapema, ili uendelee kufanya kazi kwa mantiki ya kupunguza kero katika eneo hili. Uamuzi wa Serikali kulipa gharama za uwakala utakaoanzishwa kupitia ada zitakazolipwa utaongeza tija na ufanisi. Kamati imeishauri Serikali kuzingatia kuwa kero zilizokuwa na zinazojitokeza zinazohusiana na ucheleweshaji wa utoaji wa maamuzi, urasimu na kutokujali muda zisitokee tena. Kamati inaamini kuwa utaratibu huu utapunguza usumbufu, urasimu na ucheleweshwaji wa malipo ya wastaafu hawa. *(Makofi)*

Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuandaa utaratibu utakaowezesha malipo ya pensheni kuongezeka sanjari na kuongezeka kwa kima cha chini cha mshahara ili kuboresha maisha ya wastaafu tofauti na ilivyo sasa ambapo kiwango kinachotumika ni sha siku nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unapendekeza kuanzishwa tozo ya asilimia 0.3 ya mauzo ghafi *(gross turnover)* kwa makampuni ambayo yataripoti kupata hasara kwa miaka mitatu mfululizo. Lengo ni kuyafanya makampuni haya yajitahidi kupata faida ili kuepukana na tozo hii, lakini pia kwa kuwa makampuni haya yananufaika na mazingira ya kibiashara yanayotolewa na Serikali, basi ni budi yachangie. Kamati inaunga mkono suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inaishauri Serikali kuwa katika kutoza kodi hii ni budi kuangalia lini kampuni husika imeanza biashara. Lazima vigezo vya tozo hili viwekwe wazi ili kuepuka migogoro. Kwa msisitizo Kamati inaishauri Serikali kuyachunguza yale makampuni ambayo yamekuwepo nchini kwa muda mrefu lakini yamekuwa yakitangaza hasara, ilhali bado yanaendelea kuongeza mitaji na kujipanua zaidi. Hii ipo hasa katika sekta ya madini. Lengo ni kuongeza utendaji wa tija na ili kutokujificha kwenye pori la uzembe au ujanja ujanja. Kamati inashauri kuwa kiwango hiki ni kidogo na kifikiriwe kuongezwa jinsi muda unavyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Kamati imeishauri Serikali kuwa azma isiwe tu kushika tozo la 0.3 la mauzo ghafi. Ni vyema pia Serikali ikachambua kwa nini

makampuni husika yanaingia hasara mfululizo. Kamati imeshauri ifuatavyo, Serikali ifuatilie kwa nguvu zote umuhimu wa Mashirika/Makampuni husika kutoa mahesabu yao kutokana na utaratibu wa Kimataifa *(IFRS)* na pale ambapo pana udanganyifu, adhabu kali zichukuliwe kwa mujibu wa Sheria. *(Makofi)*

Pia Serikali iangalie mfumo wake wa sheria za vivutio, kwani zinaweza kuwa chanzo cha hasara zinazojionyesha. Inawezekana ipo haja sasa ya kuhuisha Sheria za Vivutio katika Uwekezaji *(TIC)* na Sekta ya Madini pamoja na zile Sheria za Vivutio vya Mitaji. Mara nyingine viwango vya tozo visiwekwe tu bila ya uchambuzi wa kina *(arbitrarily).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi kwa mantiki ya kibiashara na kiuchumi, huwezi kuingia kwenye biashara ambayo haitakuletea faida. Mpango wa uwekezaji na kazi lazima uwe wa kibiashara na wala si ule wa kutokuzalisha faida *(philanthropic).*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo marekebisho yanayopendekezwa kufanywa kwenye ushuru wa bidhaa yatakayogusa huduma za simu za mkononi. Eneo hili linazungumziwa na Waheshimiwa Wabunge kuona ni athari gani zinaweza kujitokeza katika kuendeleza au kudumaza matumizi ya huduma hizi kwa wananchi walio wengi. Matumizi ya simu hivi sasa nchini si anasa bali ni huduma muhimu.

Kamati imeelezwa kuwa ongezeko la ushuru kwa huduma za simu limefikia asilimia 10 toka asilimia 7; ongezeko hili ni kubwa, lakini hata hivyo, Kamati imeelezwa kuwa katika nchi jirani ya Kenya ni 10% na Uganda kiwango hiki kinafikia asilimia 12. Hili ni eneo linalohitaji kuangaliwa kwa makini ili huduma za simu za mikononi zisambae kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majadiliano na Serikali, Kamati inaishauri Wizara kuimarisha mahusiano na mashirikiano na wadau wa sekta binafsi hasa katika maeneo yanayohusu kodi/ada na tozo mbalimbali, hali hii itasaidia sana kuondoa kodi/tozo ada ambazo sio la lazima na hivyo kuwa kero. Utaratibu huu utapunguza gharama zisizo za lazima za uendeshaji kwa upande wa Serikali na vile vile kupunguza uwezekano wakudumaza uwekezaji nchini au kuendelea kuibua uchumi. Aidha, ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kutoa maoni katika eneo la kodi kabla ya Bajeti, unaweza kuibua maeneo ambayo yataongeza mapato, bila ya kuwaumiza wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo moja la kutolea mfano ni Kamati kuipongeza Serikali kwa kufuta tozo la Kodi ya *VAT* kwa huduma za kukata, kupakia na kusafirisha miwa kwa wakulima wadogo wadogo wa miwa nchini. Serikali imefanya utafiti wa kina na kubaini kuwa kodi hiyo ni kero na hivyo kuisitisha kwa sharti kuwa watakaofaidika na ufutaji huo ni pale huduma zitakapotolewa na umoja wa vyama vya wakulima wadogo wa miwa vilivyosajiliwa. Uamuzi huu utawapa wakulima hawa *(out growers)* unafuu katika gharama za uzalishaji na hivyo kuwaongezea mapato yao. Aidha, faida nyingine itakuwa ni ukuzaji kiuchumi sekta ya uzalishaji sukari. Kamati inaishauri Serikali isiishie katika zao la miwa tu, bali vile vile iangalie mazao mengine inayofuata mfumo wa *out growers* kwa kuzingatia vigezo vilivyotafitiwa na vinavyohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inashauri kwa upande wa mazao ya mifugo kodi ya ngozi ghafi ibadilishwe kutoka kwenye asilimia na badala yake iwe kwa kiwango cha fedha. Sababu kubwa ni kuepukana na *under declaration* ya idadi na thamani ya ngozi na hivyo kulipa kodi ndogo. Hali hii inasababisha kupungua kwa mapato na pia kuzorota kwa viwanda vya ngozi nchini. Kamati inawashauri wadau watoe mapendekezo ya viwango vya kodi ama kwa uzito, idadi au thamani hii itasaidia kuwa na sheria ya kutumia iliyokuwa kubwa kati ya vigezo hivyo ili Serikali itoze ushuru husika. Kamati inaipongeza Serikali kwa kupanua uwigo wa huduma zinazotozwa kwa kiwango cha asilimia sifuri ya kodi ya *VAT* kwa wale wanaouza huduma nje pamoja na magunia yanayotengenezwa hapa nchini. Msamaha wa kodi ya *VAT* kwenye lami, mafuta mazito na gesi asilia iliyosindikwa ni hatua nzuri. Aidha, Kamati imeafiki uamuzi wa Serikali wa kuendelea kutoza asilimia 10 kwa mafuta ghafi kutoka nje ili kuondoa tatizo la kuvunja moyo wakulima wa zao la mafuta nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Tume ya Kamati ya Madini na Nishati iliyoongozwa na Mheshimiwa Mark Bomani tayari imeshatoa mapendekezo yake, yapo ambayo maeneo Serikali inaweza kufanya marekebisho kwa maana ya kuongeza mapato yake kutokana na tozo na kodi mbalimbali. Yapo maeneo ambayo utekelezaji wake unaweza kuanza kwa muda mfupi, wa kati na mrefu. Kamati inaishauri Wizara ijiandae mapema ili kukamilisha marekebisho hayo mara tu baada ya taarifa hiyo kujadiliwa na Bunge lako Tukufu katika Mkutano ujao wa Oktoba, 2008. Kamati ingependa kuona marekebisho yakianza mapema hali hii itasaidia sana kutunisha mfuko mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zote za Serikali kuimarisha ukusanyaji wa mapato kutokana na ada, ushuru na kodi ni lazima zikutane na changamoto za ukwepaji kodi. *Tax evasion,* kwa kuwa sayansi na teknolojia inakua kwa kasi sana na kasi hii inaendana na uvumbuzi wa njia mpya za kukwepa kodi Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudi za kuwapa mafunzo mara kwa mara watendaji wa mapato ili waweze kukabiliana na wimbi hili la kukua kwa kukua kwa ukwepaji wa kodi. Utaratibu uliopo sasa wa kuwapeleka mafunzoni watalaam wa mamlaka hii kwenye nchi zilizo na utalaam wa masuala ya kodi uendelee ili kuwapa uwezo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustapha Mkulo, Naibu Mawaziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Sumari pamoja na watalaam wao kwa umahiri wao katika kuwasilisha Muswada vizuri kwa Kamati. Kamati pia inawashukuru sana Maofisa kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwezesha Muswada huu kueleweka kwa wajumbe wa Kamati na kwa kutoa ufafanuzi wa kisheria katika masuala mbalimbali hatimaye kutuwezesha kujadili na kutuletea maoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ambao wameweza kutoa maoni

na michango ya mawazo mbalimbali katika kuboresha Muswada huu ili hatimaye uletwe mbele ya Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Naomba nitumie fursa hii kuwatambua wajumbe wote kama ifuatavyo, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati ni Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Suleiman Saddiq, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na Mheshimiwa Andrew Chenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Kaimu Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashillilah, pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuwashukuru Ndugu Anselm Mrema na Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati hii kwani sote kwa pamoja tumeweza kukamilisha maandalizi ya Muswada huu wa Sheria ya Fedha ya mwaka *(The finance Bill, 2008)* kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI (k.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED- MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningependa kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2008 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6) Toleo la mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika, kwa wewe Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuendesha Bunge hili. Sambamba na hilo naomba kutoa shukrani zangu za pekee kwa kazi kubwa inayofanywa na Naibu Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Dr.Wilbrod Slaa katika kuhakikisha kuwa hotuba zetu zinakuwa katika *standard. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitowashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani, kwa ushirikiano wao katika matayarisho na mawasilisho ya hotuba zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kutoa salaam za pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mwenyezi Mungu awape roho ya ustahamilivu katika kipindi hiki kigumu. Pia nitoe pole kwa Mheshimiwa Savelina

Mwijage kwa kuondokewa na mwanae mpendwa, mjukuu wake pamoja na dereva wake katika ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani naomba nitoe maelezo mawili yafuatayo, la kwanza maoni tunayotoa kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2008 ambao kimsingi ndiyo inayoomba kibali au idhini ya Bunge kupitisha kodi na vianzio mbalimbali imepitwa na wakati baada ya *appropriation bill* ya mwaka 2008 kupitishwa. Kwa maoni ya Kambi ya Upinzani kuna mkanganyiko mkubwa katika Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2007 na kifungu 105 (3) na (4) na kifungu cha 106. *(Makofi)*

Kwa mantiki yoyote ile haiwezekani kabisa Bunge liidhinishe kwanza matumizi kisha linarudi nyuma kujadili idhini ya vyanzo hivyo. Kambi ya Upinzani inataka vifungu hivyo virekebishwe haraka iwezekanavyo ili kuondoa mgongano huo wa kikanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Kambi ya Upinzani inasikitika na utaratibu unaotumiwa na Serikali wa kufanya mabadiliko makubwa katika sheria hii ya fedha, wakati Wabunge hawana sheria mama zilizobadilishwa. Jambo kama hili lilifanywa miaka minne iliyopita kwa kuingiza kifungu kidogo cha *redeem tax* kwa Kampuni za Makampuni matokeo yake leo Taifa linakosa si chini ya *Tanzanian shillings* bilioni 800 za mapato. Kambi ya Upinzani inaomba uratibu huu uachwe kwani Taifa linaweza kukosa fedha nyingi za mapato. Wabunge wanalazimika kujadili jambo ambalo wao hawalielewi vizuri au hawapati picha kamili lakini wanalazimika kuliidhinisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, sasa naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2008 kama ifuatavyo, marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, kifungu cha nne cha Muswada huu kinabadilisha kiwango cha 7% hadi kiwango cha 10% kwa huduma za simu. Hii ni kodi kubwa sana na mzigo kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ongezeko hili Tanzania itakuwa ni nchi ya pili kwa kutoza kodi kubwa kwenye huduma ya mawasiliano ya simu za mkononi. Ni muhinu ikaeleweka kwamba huduma ya simu sio huduma ya anasa, bali ni huduma ya msingi na muhimu kwa wananchi katika harakati zao za kujiletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, makampuni ya simu yanalipa kodi inayofikia shilingi bilioni 49.6 kwa mwaka, kitendo cha kupandisha kodi kwa kiwango hiki kutasababisha watumiaji kupungua hasa ukizingatia kwamba gharama zitapanda. Pia ongezeko hili la kodi litapelekea uwekezaji wa makampuni ya simu kupungua hasa vijijini, je, tunakwenda wapi?

Katika Bajeti ya mwaka jana tulifanya maamuzi ya pupa ya kuongeza ada ya mwaka ya leseni za magari kwa kiasi kikubwa matokeo yake watu hawakulipa kodi kama ilivyotakiwa hatua ambayo imeilazimu Serikali kuleta mabadiliko mengine. Hali hii inaweza kutokea kwenye huduma za simu tusipokuwa makini. Isitoshe nadharia ya uchumi ni kuwa mapato ya Serikali yanakuwa makubwa *turnover* inapokuwa kubwa, na

*turnover* inakuwa kubwa watumiaji wanapokuwa wengi na watumiaji wanakuwa wengi gharama inakuwa ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kwamba kiwango hiki cha 7% kisiongezwe ili kuwahakikishia wananchi wanapata huduma ya mawasiliano ya simu za mkononi na wasibebeshwe mzigo mkubwa wa kodi hasa ukilinganisha kwamba hii sio kodi pekee ambayo wananchi wanalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali isiishie tu katika kupandisha ushuru wa bidhaa na huduma mbalimbali, bali pia ifute misamaha isiyo ya lazima. Mfano msamaha wa ushuru wa mafuta kwa makampuni ya Madini kama inavyotolewa na sheria hii. Msamaha huu unalikosesha Taifa mapato makubwa yatokanayo na ushuru huo na linapunguza uwezo wake wa kutoa huduma kwani ni vigumu kutambua na kudhibiti mafuta yanayopata msamaha baadhi ya wakati mafuta hayo huuzwa ndani ya nchi badala ya kutumika kuzalisha madini. Hivyo ushuru huu ufutwe na makampuni yalipe ushuru huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Kambi ya Upinzani inapenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kutekeleza kile ambacho Kambi ilipendekeza wakati Serikali ilipoleta Muswada wa sheria wa kuanzishwa *Law School*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko haya ya sheria yatawapatia fursa ya kupata mikopo hali ambayo itawawezesha kuhudhuria mafunzo ya sheria kwa vitendo kutakakopelekea kukamilika kwa shahada zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sasa utaratibu ulio wazi ukawekwa ili kuwawezesha wanafunzi hawa kupata fedha zilizotengwa mahsusi kwa ajili yao ili kuepusha migomo ambayo tumeishuhudia hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu pia umakini ukatumika katika mfumo wa kujua ni wanafunzi wangapi wana uwezo kujilipia. Wanafunzi wengi wanashindwa kulipia hata asilimia inayobaki wanayotakiwa kujilipia wenyewe. Hili liangaliwe kwa mtazamo wa mbali na wa kina hasa kutokana na ukweli kwamba katika kipindi hiki vyuo tofauti vya elimu ya juu hasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam vimeshapandisha ada ya masomo mara mbili zaidi ya ile iliyokuwepo. Kana kwamba haitoshi taratibu za Vyuo vya Elimu ya Juu huwa havitoi vyeti vya kumalizia masomo iwapo mwanafunzi hajamaliza kulipia ada inayotakiwa. Kwa msingi huu na kwa kulinganisha na ongezeko la ada za masomo vyuoni tutakuwa na wahitimu wengi ambao hawana vyeti vya kumalizia masomo kwa sababu tu wameshindwa kukamilisha asilimia iliyoachwa na Bodi ya Mikopo na hivyo hawataweza kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kufahamu kutokana na marekebisho haya ni kiwango gani cha mikopo kitatolewa hasa kwa kuzingatia kuwa haya ni mafunzo maalum yanayohitaji wanafunzi hao waonekane kuwa ni *proffessionals* kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mabadiliko haya ya Sheria ya Bodi ya Mikopo, kuna haja pia ya kufanya mabadiliko katika ya kifungu cha tatu, yaani *interpretation section* cha Sheria ya Bodi ya Mikopo kinachotoa tafsiri ya maneno ya *higher education*, *accredited institution* na *student. (Makofi)*

Kambi ya Upinzani inataka kufahamu ni lini Serikali italeta marekebisho ya sheria ili nia hii njema ya kuwasaidia wanafunzi wetu isikwame kwa muda mrefu. Hata hivyo tafsiri ya sheria inahitaji mabadiliko katika maneno yafuatayo, kwanza ni *higher education.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Mikopo, elimu ya juu ni ile inayotolewa katika kiwango cha Shahada na Stahahada ya Juu na haijumuishi mafunzo ya *certificate*. Lakini Shahada ni dhana pana ambayo inajumuisha Shahada ya Kwanza, Shahada ya Pili (Uzamili) na Shahada ya Tatu (Uzamivu). Kwa kawaida kwa sasa Bodi ya Mikopo inatoa mikopo kwa wanafunzi wa Shahada ya Kwanza, Shahada ya Pili kwa uchache na kwa masharti magumu sana na Stashahada ya Juu kwa uchache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho tunayoyafanya yatajumuisha *Certificate in Legal Practice*. Hivyo tafsiri ya neno *higher education* (elimu ya juu) lifafanuliwe zaidi lijumuishe mafunzo hayo ili pia wanafunzi wake waweze kupata mikopo kwa urahisi zaidi. Hii ni kwa sababu marekebisho haya yamekuja kutokana na mafunzo haya hapo awali kuitwa *Postgraduate Diploma in Legal Practice* na sheria ikawa hairuhusu kupewa mikopo, leo tunaweka dhana ya *certificate* (cheti) ambayo pia haijawekwa vizuri kisheria. *(Makofi)*

Pili ni *accredited institutions. Interpretation* (tafsiri ya kimatumizi) ya neno hili pia iongezwe ili kujumuisha taasisi yenye kutoa mafunzo ya elimu ya *Certificate in Legal Practice* yaani *Law School of Tanzania* ili marekebisho haya yalete maana na tatu, *student*. Sheria ya Bodi ya Mikopo inasema mwanafunzi anayepaswa kupewa mkopo chini ya sheria hii ni yule aliyedahiliwa kwa ajili ya mafunzo ya shahada au stashahada ya juu. Hivyo iongezwe na kusomeka *and any person pursuing studies in Law School of Tanzania. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo maoni yetu haya ya awali yatazingatiwa, Kambi ya Upinzani haina pingamizi na marekebisho ya kifungu hiki cha Sheria ya Bodi ya Mikopo yanayoongeza ibara ndogo ya (f) kwani inakusudia kuwarahisishia vijana wetu kupata elimu ya sheria kwa vitendo ili kuwa watendaji bora. Kwa mfano hivi juzi Chuo hiki cha mafunzo kwa vitendo kilitangaza majina ya wanafunzi 86 na kuwataka wasisajiliwe na kuanza masomo kama hawakupeleka risiti ya malipo ya ada, wengi wao katika hawa walishindwa kutokana na kutokuwa na fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria 11 zinazokusudia kutoa mamlaka kwa Waziri wa Fedha kuamua kiwango cha fedha kutoka mamlaka mbalimbali kuingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Katika Muswada huu takriban Sheria

kumi na mbili zinafanyiwa marekebisho ili kutoa mamlaka ya kisheria kwa Waziri mwenye dhamana ya fedha kuamua kiwango cha fedha zitakazohamishwa na kuingia katika sehemu ya fedha za Umma katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Sheria hizo ni kama zifuatazo, Sheria ya Masoko ya Mitaji (sura ya 79), Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti ya Maji na Nishati (sura ya 414), Sheria ya Michezo ya Bahati Nasibu (sura ya 41), Sheria ya Ununuzi (sura ya 410), Sheria ya Mamlaka ya Bandari (sura ya 166), Sheria ya Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (sura ya 413), Sheria ya Mamlaka ya Usalama wa Anga (sura ya 80), Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano (sura ya 172), Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi (sura ya 219), Sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro (sura ya 284) na Sheria ya Hifadhi za Taifa (sura ya 282). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho yanayokusudia kuingiza kipengele hiki ni mazuri kwa vile yanakusudia kuchukua sehemu ya fedha zinazotokana na makusanyo na mapato katika mamlaka hizo ili zichangie katika matumizi ya umma. Pamoja na hayo, tatizo ambalo Kambi ya Upinzani, inaliona linaweza kutokana na nyongeza ya vifungu hivi katika sheria hizi ni kama ifuatavyo:-

(1) Vifungu hivi vitatoa mamlaka makubwa na yasiyo na mipaka ya kuamua kiwango ambacho kitahamishiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Waziri anayehusika na fedha.

(2) Hakuna vigezo na utaratibu unaoonyeshwa kwamba utatumika kuhakikisha kiwango hicho kitakachohamishwa.

(3) Nyongeza ya vifungu hivi haijazingatia na kuweka wazi kuhusu gharama za uendeshaji na hasara zitokanazo na uimarishaji wa huduma zitakazopelekea makusanyo ya mapato ya mamlaka hizi.

(4) Muingiliano wa Kimamlaka.

(5) Bunge linaacha jukumu lake la kusimamia na kutoa idhini ya kutoza kodi, kwani mamlaka inakabidhiwa mikononi mwa Waziri, bila Bunge kuwa na mamlaka ya udhibiti. *(Makofi)*

Pia kuruhusu Waziri wa Fedha kuidhinisha Bajeti za mamlaka nyingine ni kusababisha muingiliano wa kimamlaka miongoni mwa mamlaka za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa nyongeza ya vifungu hivi iangalie kwa makini vipengele hivi ili kuleta ufanisi katika makusanyo yanayokusudiwa kuhamishiwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali, kama sehemu ya fedha za umma na kuepusha migongano kati ya Serikali na Mamlaka husika na Bunge lipate kujulishwa kuhusu hatua zitakazochukuliwa na Waziri ili liwe na nafasi ya kuingilia mapema pale inapoona Waziri katumia mamlaka yake visivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Pensheni na Mafao, Muswada huu pia unafanya marekebisho ya sheria mbalimbali ili kuzifanya

mamlaka hizi kuwa wakala wa Serikali katika kulipa mafao na pensheni kwa niaba ya Serikali. Katika mpango huu zaidi ya sheria tano zinazoongoza mifuko mitano ya mafao na pensheni zinarekebishwa ili iweze kuwa wakala wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mifuko hii imekuwepo muda mrefu na ina wanachama au wachangiaji wake ambao wanafaidika na huduma zake. Kufanywa kuwa wakala wa Serikali sio jambo baya ila nafasi hiyo itumike vizuri. Ninachokusudia kusisitiza ni kwamba Serikali ipeleke asilimia ya michango ya wafanyakazi inayotakiwa kupelekwa na sehemu ya gharama na malipo ya uwakala bila kuchelewa ili kuwezesha mifuko hii ifanye shughuli zake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa kwa sasa mifuko hii ni nyenzo muhimu kwa Taifa kwani inatumika katika kufanikisha miradi yetu mbalimbali ya kimaendeleo hasa ya ujenzi, hivyo kufanikiwa kwao ni chachu ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004, katika Muswada huu viwango mbalimbali vya kodi vinaongezwa na kupunguzwa, ni jambo zuri kwani vile vinavyoongezwa vinakusudia kuongeza kiwango cha mapato na vile vinavyopunguzwa vinakusudia kuwasaidia wananchi katika kuyafikia maendeleo yao. Lakini pamoja na hayo ukusanyaji mkubwa wa kiwango kikubwa cha kodi kutoka kwa wananchi unatakiwa uende sambamba na upatikanaji wa huduma muhimu kama vile huduma za maji, umeme, barabara na nyinginezo ila kwa Tanzania hili ni tofauti. Kodi kubwa inakusanywa huduma bora bado hazipatikani. *(Makofi)*

Kilio kingine cha Kambi ya Upinzani ni uwepo wa misamaha mingi ya kodi isiyo ya lazima katika sekta mbalimbali za uchumi inayotolewa kupitia sheria hii na sheria nyingine zinazokwenda sambamba na sheria hii. Mfano sekta ya madini na uwekezaji kutoka nje. Hizi ni sekta za msingi ambazo zingeweza kuliingizia Taifa hili fedha ya kutosha ya kujiendesha lakini misamaha mingi ya kodi kwa kisingizio cha kuwavutia wawekezaji ni tatizo. Kwa mujibu wa taarifa kutoka chapisho la *The Demystification of Mining Contracts in Tanzania*, Tanzania ni mzalishaji mkubwa wa tatu wa dhahabu kwa Afrika ukitoa Ghana na Afrika ya Kusini lakini sekta hiyo ya madini inachangia kwa 3.2% ya *GDP* na 3.6% tu ya mapato ya Serikali yatokanayo na kodi. Hali hii inatokana na kutunga Sheria na kuingia katika mikataba na wawekezaji yenye masharti ya kutobadilisha viwango vya kodi mbalimbali vinavyostahili kulipwa na makampuni hayo hata kama viwango hivyo vitabadilika katika hali ya kawaida ya mabadiliko ya sheria. *(Makofi)*

Kwa mfano ibara za 11.1, 11.1.2, 11.1.7 za *Development Agreement* baina ya Serikali na *Pangea Minerals Limited* kwa ajili ya Mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi uliosainiwa tarehe 17 Februari, 2007, *Gold Mine Development Agreement* baina ya Serikali na *Samax Resources Limited* na *Ashanti Goldfields (Tanzania) Limited* kwa ajili ya uchimbaji madini ya dhahabu Geita yaliyosainiwa tarehe 24 Juni, 1999 chini ya ibara ya 10.1, 10.1.3, 10.1.7 zinaonyesha hali halisi ya ukweli huu. Mfano (a) misamaha ya kodi chini ya Sheria ya Marekekebisho ya Sheria mbalimbali za fedha ya mwaka 1997. Misamaha hii inatolewa kwa makampuni yanayojishughulisha na uchimbaji na utafutaji

wa madini na pia wawekezaji katika sekta mbalimbali nchini. Kwa kulizingatia hili tunaweza kuona kwamba kiwango tunachokikusanya ni kidogo kuliko tunachokisamehe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika marekebisho haya maoni yetu ni kama ifuatavyo:-

(a) Marekebisho yanayoongeza kiwango cha kutoza kodi katika pato la mtu yaani *Personal Income Tax Structure* kwa kweli ni kikubwa sana hasa ukilinganisha hali halisi ya maisha ya sasa ya Mtanzania ambayo kuna upandaji mkubwa wa bei za bidhaa na huduma, hivyo kiwango hiki hakitaweza kwenda sambamba na nia ya Serikali inayokusudia kuongeza kiwango cha chini cha mshahara na kulinda mapato yatokanayo na ajira kutokana na athari ya mfumko wa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano pato la mtu kwa mwaka la kati ya shilingi 1,200,000 na lisilozidi shilingi 4,320,000/= atatakiwa kulipa kiwango cha 15%. Huu ni mzigo kwa sababu 15% ya kipato hiki kwa mwaka ni shilingi 648,000/= ambazo ukikokotoa kwa kiwango cha kipato hiki ni mshahara au pato la shilingi 360,000/= na kwa *rate* hii atatakiwa kulipa kodi ya shilingi 54,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitakachobaki kwa mtu huyu kwa mwezi ni shilingi 30,600/=. Je, kiasi hiki kinatosha kwa maisha halisi ya Mtanzania? Hii inampa Mtanzania matumizi ya siku kwa shilingi 10,200/=. Tukiangalia kima cha chini cha mshahara ni shilingi 100,000/= na hata maslahi ya wafanyakazi sio mazuri kiasi cha kuwekewa kodi za juu za aina hii na huku bei za bidhaa na huduma zimepanda kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwa mujibu wa taarifa za *BOT* kupitia *economic bulletin for quarter ending March, 2008,* zinaeleza kuwa mfumuko wa bei umeongezeka kwa asilimia 8.9 katika kipindi kilichoishia Machi 2008 kutoka 6.9% iliyosababishwa na kuongezeka kwa bei za mafuta na nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi kwa mujibu wa *BOT monthly economic review May 2008*, inaeleza kuwa mfumuko wa bei umepanda kwa 9.7% kutoka 9.0% kwa mwezi uliopita. Mfumuko wa bei za chakula imepanda kwa kiwango cha 11.6%. kwa mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo la kodi la mapato binafsi (mishahara) baina ya 15% na 30% kwa mapato yanayoanzia shilingi 100,000/=. Hii inapelekea mabadiliko ya mishahara kutokuwa na tija na kuwa ni hasara zaidi. Mfano mshahara wa shilingi 100,000/= ukitoa 15% ya kodi inabaki kiasi cha shilingi 85,000/= tu, ni kiwango kikubwa kuchukuliwa katika mshahara wa mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kwamba badala ya kuongeza kiwango kikubwa cha kodi katika mapato ya mtu mmoja mmoja, Serikali irekebishe Sheria za Kodi mbalimbali na fedha zinazohusu Sekta ya Madini na Uwekezaji kwani kuna misamaha mingi sana isiyo ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuondolewa kwa nafuu ya ziada ya gharama za uendelezaji migodi ambazo hazijakombolewa ya 15% kwenye sekta ya madini iliyowekwa kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004. Hii ni kwa sababu kiwango hiki ni kikubwa na inaisababishia Serikali hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali pia kuondoa unafuu wa asilimia mia moja wa gharama za uwekezaji kwa makampuni ya madini kwa mwaka wa uwekezaji katika ukokotoaji wa mapato katika mwaka wa uwekezaji. Nafuu hii ni kubwa sana, hivyo basi tunashauri kwamba nafuu ya gharama za uwekezaji itolewe kama ilivyo katika Jedwali la tatu la Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 9 cha Muswada huu kinarekebisha Sheria Kuu ya Kodi, kwa kuongeza kifungu cha 83A kuipa Serikali mamlaka ya kuzuia kodi inayopaswa kulipwa kwa kiwango cha 2% kutokana na malipo yanayotokana na malipo ya bidhaa na huduma kwa Serikali na watu ambao hawana hati za utambulisho za mlipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kitu cha ajabu katika nchi zilizoendelea kuona mlipa kodi yeyote hata wa kiwango cha chini hana hati ya utambulisho ya mlipa kodi. Inashangaza kwa Tanzania kutunga sheria zinazoashiria kuruhusu watu kutokuwa na utambulisho wa mlipa kodi kama inavyoonyeshwa na nyongeza ya kifungu hiki. Kwa msingi huu hatutakuwa na sababu ya kuwalaumu wanaokwepa kodi kwani hata kuwatambua rasmi tunakataa wenyewe, je, wao wasitumie udhaifu huo kwa faida yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *fourth schedule* ya Sheria ya Kodi ya Mapato, inatamka wazi kuwa mikataba yote *(all contracts)* lazima kuwe na hati ya utambulisho ya mlipa kodi kwa watu wanaohusika ikijumuisha mikataba ya usambazaji wa bidhaa na huduma. Pia kifungu cha 133(1) kinatamka Kamishna Mkuu wa Kodi kutoa namba ya utambulisho ya mlipa mkodi yaani *(TIN)* kwa kila mtu anayeendesha/anayefanya biashara/*business* nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kuuliza je, nyongeza ya kifungu hiki haijaona matakwa ya *fourth schedule* na kifungu 133(1) ambacho kinamtaka kila mtu anayepata mapato yanayopaswa kutozwa kodi ya mapato ajisajili katika Ofisi ya Mamlaka ya Mapato nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza ya ibara hii ni kinyume na sheria kuu ya kodi chini ya kifungu cha 133(4) (5) na *fourth schedule* ambazo kwa pamoja zinaeleza kuwa taasisi zilizoanishwa hapo ni lazima zipate nakala ya *TIN* ya mlipa kodi kabla ya kutoa huduma ya kiuchumi ya mtu huyo. Taasisi zilizoainishwa hapa zinajumuisha Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, Wizara zote na wakala zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inapenda kuiuliza Serikali kwa nini ikubali kusambaziwa bidhaa na huduma na watu au makampuni wasiokwenda

sambamba na matakwa ya sheria? Je, nyongeza ya kifungu hiki haikusudii kutoa mwanya kwa mapato yanayostahili kukusanywa kupotea au kwenda mikononi mwa wachache kutokana na kukataa kutumia utaratibu maalum uliowekwa kisheria? *(Makofi)*

(c) Uanzishaji wa Kodi Mbadala *(Alternative Minimum Tax)* ya kiwango cha 0.3% kwa makampuni yanayopata hasara kwa miaka mitatu mfululizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unaongeza kipengele kinachowapa kodi mbadala ya 0.3% kwa makampuni yanayopata hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Hii ni nafuu bora kwa wawekezaji lakini kwa upande wa Taifa linalotegemea mapato ili kuboresha uchumi wake na kuondoa umaskini, kodi hii mbadala ni kikwazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, taarifa zinaeleza kwamba mpaka mwaka 2006 makampuni makubwa yanayojishughulisha na utafutaji na uchimbaji wa dhahabu pamoja na kufanya kazi hiyo kwa muda wa miaka mitano na bei ya dhahabu kuwa imepanda katika soko la dunia kwa wakati huo, hakuna kampuni hata moja ya uchimbaji dhahabu nchini iliyotangaza/iliyoeleza pato linalopaswa kutozwa kodi yaani *corporate tax* ya 30%. Hii ni kwa sababu ya visingizio kwamba hawajapata faida, leo tunaanzisha kiwango hiki cha kodi mbadala, hivi jamani tunafanya nini na rasilimali zetu na tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kuiuliza Serikali, je, pamoja na misamaha mingi sana ya kodi inayowapa wawekezaji katika viwango na kwa kupitia sheria mbalimbali bado wawekezaji hao hawajatosheka? Je, Serikali italihakikishiaje Bunge hili Tukufu kwamba kodi hii mbadala haitatumika kama ni kificho cha kukwepa kulipa kodi halisi ya 30% inayotakiwa kulipwa na makampuni hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa uanzishwaji wa kodi hii mbadala ni kikwazo kwa maendeleo ya uchumi na isipitishwe kabisa kwa ajili ya kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, ni wazi kuwa kiwango cha Kodi ya Ongezeko la Thamani la 20% kinachotozwa na Tanzania hasa ukilinganisha na viwango vinavyotozwa na nchi jirani kama Uganda na Rwanda.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya *schedule* ya kwanza ya Sheria ya Kodi ya Mapato ambayo inafuta *"b(aa)" and "(bb)"* na kuweka *item* mpya (1) hadi (7). Marekebiso ya jedwali la tatu la sheria kuu ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (b) katika *item* 10 kwa kuongeza maneno *excluding house hold consumables*, haionekani kuwa na umuhimu kutokana na dhana mzima ya kodi inayosamehewa kupitia kifungu hiki iko wazi. Kwani ukishasema uingizaji au manunuzi ya ndani ya bidhaa na huduma na au kwa niaba ya jumuia za kidini zilizosajiliwa, jumuia za kujitolea misaada na taasisi nyingine zinazoendeshwa bila kukusanya faida kwa ajili ya kutekeleza majumu yao hayo, hakuna

haja ya kusema unatenga manunuzi ya huduma kwa ajili ya matumizi ya nyumbani yaani *excluding households consumables. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki kimejitosheleza na hasa ukitumia tafsiri lengo ya kifungu hiki yaani *purposive approach of interpretation.* Nyongeza ya kifungu hiki kimewekwa kwa madai kwamba taasisi na jumuiya hizi hutumia nafasi hizi na msamaha unaotolewa na kifungu kinachorekebishwa kukwepa kodi inayopaswa kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kwamba kuweka sheria ambazo ni pana sana sio sababu ya kukusanya pato kubwa bali tathmini bora na ya uhakika, kubuni vyanzo vingi vya mapato na utendaji bora wa mamlaka za kukusanya mapato ndio misingi pekee ya kukusanya mapato stahili na makubwa ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msamaha wa *VAT* kwa wafanyabiashara wakubwa chini ya sheria ya *Hotels Act, Cap 105, Re. 2002,* kifungu cha 73A cha marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Hoteli, kinatoa msamaha kwa wafanyabiashara wakubwa kwa kusema kuwa sheria hiyo inatoa msamaha wa kutolipa kodi ya ushuru wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mtu yeyote au jumuiya yeyote ya watu ambao wamesajiliwa chini ya sehemu ya (iv) ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kuanzia siku ya kuanza kutumika kwa Sheria hii. Msamaha huu ni sawa na kuwapa nafasi wafanyabiashara hawa kutolipa kodi ambayo kimsingi kila mtu anayeuza bidhaa na kutoa huduma zinazopaswa kulipwa kodi hii analazimika kuilipa kwa mujibu wa kifungu cha 3(1) na 4(1) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 1998. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi ya ushuru wa hoteli ya 20% inayotakiwa kulipwa chini ya kifungu cha 26(1) imekuwa kero kubwa hasa kwa wafanyabiashara wadogo wadogo katika sehemu tofauti za miji, majiji, manispaa na nyenginezo. Hii ni kwa sababu kiwango cha 20% ni kikubwa na hakizingatii gharama za uendeshaji kwa biashara hiyo. Mfano tarehe 10 Januari, 2008 Umoja wa Wafanyabiashara wa Nyumba za Kulala Wageni Mwanza (UWANZA) ulimuandikia barua yenye kumbukumbu namba UW/MZ/06, Waziri wa Fedha wakilalamikia kodi hii na manyanyaso wanayoyapata kwa sababu ya kodi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko haya yalijibiwa kwa barua yenye kumbukumbu namba TYC/R/160/32 ya Waziri wa Fedha, kwamba atalishughulikia jambo hili lakini hadi leo hii halijashughulilikiwa ipasavyo. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia jambo hili kwa makini na kuchukua hatua zinazofaa ili kupunguza usumbufu kwa wafanyabiashara hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kifungu hiki cha sheria kinawaondoa Watanzania wenye mitaji midogo katika biashara na kuwapa fursa wafanyabiashara wakubwa kuendelea kwenye biashara hii (dhana ya ushindani iko wapi?). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kwanza kabisa bahati nzuri, maneno uliyosema kuhusu Kanuni kwenye hotuba yako hayamo, habari nzuri. Kwa sababu Waheshimiwa Wabunge nadhani ni kutokuelewa *concept.* Katika nchi nyingi wakati wa kutunga Bajeti wakati Waziri wa Fedha alipowasilisha makadirio yake pale, ingekuwa ndiyo inaingia *Finance Bill.* Lakini kwa utaratibu wetu tunachambua Wizara hadi Wizara, Wizara hadi Wizara kila Wizara ina fungu lake, kila Wizara ina fungu lake.

Kwa hiyo, tunapotunga sheria hii hatutungi kwa ajili ya Wizara moja moja, tunatunga kutokana na Bajeti aliyoiwasilisha Waziri wa Fedha. Ndiyo maana *appropriation bill* haina maneno mengi. Ni kwamba tuna-*sum up* yote tuliyoyafanya katika siku zote hizi, Wizara moja moja tume-*sum up* kwamba *in real sense* tulichosema ni kile chenye *appropriation bill*. Kule kwingine tulikuwa tunashauri Mawaziri, *how best they can run the business* huku, kukosoa, kufanya nini na nini. Lakini hoja yenyewe ya Bajeti ni ile aliyotoa Waziri siku ya *Budget Day.* Hiyo tunaikamilisha kusema yote tuliyosema ukweli yanarudi pale pale Waziri aliyosoma hapa kwamba ni shilingi trilioni 7 na nukta ngapi, ndiyo hiyo ndiyo tuna-*appropriate* hapa. *(Makofi)*

Sasa tukitoka hapo ndiyo tumesema sasa Serikali mwaka huu itatumia fedha zake hizi zote kwa namna tulivyozungumza hapa. Lakini kabla hawajaanza kutumia, lazima tuwape ruhusa, mnapata wapi hizo fedha, *that is a Finance Bill* ya sasa. Mnapata wapi hizo fedha ndiyo tunaletewa Muswada na ndiyo maana ninafurahi kusema safari hii hata wachangiaji wenyewe wako wengi. Miaka mingine wengine wanasema mradi tulipitisha pale basi imeisha. Hapana, hii ni sheria kabisa inayomruhusu Waziri wa Fedha kutoza fedha wapi, kutafuta wapi na kama tungekuwa *active enough* nafikiri Kamati ya Fedha na Uchumi wamefanya na kushauri mahali fulani fulani kwamba tubadilishe, labda tubadilishe hili, tubadilishe hili. Kwa hiyo, kazi lazima ifanyike hapo, hiyo ni sehemu ya pili. Hii nyingine ilikuwa kwamba Serikali inakusudia kutumia hivi. Sasa hii inasema Serikali inakusudia kupata mapato yake kutokana na sehemu hii. Kwa hiyo, ni sehemu mbili tofauti. Hakuna mkanganyiko wowote ule, *it is really clear* na sheria hizi, Miswada ya Sheria iko na Miswada ya Nyongeza ya Matumizi ya fedha. Hiyo nayo pia wanaweza kuileta. Sasa ungesema tunafanya hii basi ingekuwa tunasubiri mpaka *budget session* ndiyo tulete Sheria namna hii. Hapana, hiyo inaweza kutokea wakati wowote. Kwa hiyo, *we are not very right* kusema kwamba Kanuni zimechanganyika. Hazichanganyika kabisa. *(Makofi)*

Mimi nafurahi sasa hivi mnachambua, kitu ambacho hamruhusiwi kufanya ni kupunguza. Katiba inawakatalieni kabisa kabisa hamtaruhusiwa kupunguza. Mtasema tu ili mradi ilingane na hiyo lakini siyo pungufu ya hiyo. Kwa hiyo, tuko *in order* kabisa na tunatekeleza Katiba. Maana kusema hatutekelezi Katiba hapa ni ki-*session* ni *very serious.* Lakini nadhani hamkuilewa vizuri. *(Makofi)*

Sasa tunaendelea, tunao wachangiaji, kama nilivyosema wengi zaidi ya 12 na ni jambo zuri kwamba wako wengi. Kwa hiyo, tutaanza na utaratibu wetu ule ule ambao hawajachangia kabisa kabisa wataanza. Kwa hiyo, ataanza na Mheshimiwa Joseph

Mungai, atafuatiwa na Mheshimiwa Job Ndugai, kwa sababu katika hii hoja Kambi ya Upinzani ukiondoa wewe uliyetoa hoja wako watu wawili tu. Kwa hiyo, nimemwingiza Mheshimiwa John Cheyo. Halafu atakuja Mheshimiwa Mohamed Missanga, atakuja Mheshimiwa Aloyce Kimaro, atakuja Mheshimiwa Gosbeyt Blandes. Yuko Mheshimiwa Kilonsti Mporogomyi, yuko Mheshimiwa Esther Nyawazwa, yuko Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, yuko Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, yupo Mheshimiwa Michael Laizer na yuko Mheshimiwa Kabwe Zitto. Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Joseph Mungai na Mheshimiwa Job Ndugai kwa muda wetu huu. Halafu Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Mohamed Missanga tutaangalia hapo. Mheshimiwa Mungai.

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nimepata *technical assistance* hapa. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha inayohusu Sheria ya Fedha. Napenda kabla ya kuchangia nikupongeze sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufafanuzi mzuri na sahihi ulioutoa kuhusu mipangilio. Napenda kuthibitisha kwamba huu ndiyo utaratibu ambao tumekuwa tukiutumia katika Bunge hili tangu nilipoingia katika Bunge hili mwaka 1970. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi na katika kuunga mkono napenda kuchukua nafasi hii kutoa maoni na ushauri katika maeneo manne na kama ulivyosema katika hoja hii haturuhusiwi kupunguza. Kwa hiyo, mimi nachangia kwa maana ya kutoa maoni na ushauri katika maeneo manne. Eneo la kwanza linahusu sehemu ya pili, ya tatu na ya nne ya Muswada. Katika sehemu hizo tatu, ya pili, ya tatu na ya nne za Muswada, Waziri tunampa kupitia Sheria hii madaraka ya kuchota baadhi ya mapato ya mamlaka za usimamiaji. Nadhani hiyo *summary* ni *summary* nzuri ya tunachofanya katika sehemu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchota mapato kwenye *regulatory authorities* kwa mfano *CMCA* yaani mamlaka inayosimamia masuala ya masoko na mitaji pamoja na mengine ambayo yameorodheshwa katika sehemu hizo tatu nilizozitaja. Ushauri wangu katika eneo hili ni kwamba kwanza Mheshimiwa Waziri ahakikishe kabisa kwamba Mamlaka hizo zinaachiwa fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake na hapa mimi napenda kuunga mkono sana na kumshauri Mheshimiwa Waziri azingatie ushauri uliotolewa na Kamati ya Fedha kwamba jambo hili lisifanywe kwa maguvu ila lifanywe kwa mashauriano ya kutosha na Wizara za sekta husika pamoja na uongozi wa mamlaka zenyewe ili tuhakikishe kwamba vyombo hivyo ambavyo viliundwa kwa nia nzuri vinaachiwa fedha za kutosha kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa pili Wizara, pamoja na kuchota fedha kutoka huko na yenyewe ihakikishe inawasimamia vya kutosha, inazisimamia vya kutosha mamlaka hizo kutekeleza wajibu wao vizuri. Kwa sababu kuna baadhi ya mambo tunayaona yanafanyika na mamlaka hizi zipo, hayafanyiki vizuri au wakati mwingine yanayotakiwa kufanyika hayafanyiki. Sasa nashauri Wizara isiwe tu mchukuaji wa fedha, lakini pia iongeze macho yake katika kuvisimamia vyombo hivyo vitekeleze wajibu wake kwa mujibu wa sheria. Kwa mfano, Mamlaka ya Masoko na

Mitaji inao wajibu wa kisheria, imepewa wajibu wa kisheria kabisa wa kuwalinda wenye hisa wadogo katika makampuni mbalimbali, kuwalinda kwamba wapate haki kutoka kwenye makampuni hayo na siyo kwa mashirika ya umma tu ili mradi ni kampuni ina wawekezaji wenye hisa. Mamlaka hii imepewa wajibu wa kisheria kusimamia kwamba wawekezaji wadogo wanapewa haki wanazostahili katika makampuni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya haki ni kwamba wawe wanapewa taarifa zenye uwazi wa kutosha. Kwa hiyo, ningeshauri kabisa kwamba Mamlaka ya Masoko na Mitaji *(CMCA)* wawe wanazipitia taarifa za makampuni na mashirika na kuona kwamba zinatoa taarifa zenye uwazi yaani zinafanya kinachoitwa kwa lugha ya wataalam *adequate disclosure.* Taarifa za mashirika zingine ukizisoma hakuna *adequate disclosure.* Si vizuri mtu mzima niseme bila kutoa mfano. Nataka kutoa mfano wa Benki ya *CRDB.* Benki hii si shirika la umma, lakini ina wanahisa zaidi ya 10,000 na ina hisa zaidi ya milioni 260 ile jumla ya hisa zilizo katika benki hii milioni 260, wana hisa zaidi ya 10,000. Hapa ni mahali ambapo inatakiwa *CMCA* itupie macho kwamba taarifa zinatoa *adequate disclosure.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma taarifa za benki hii kwa miaka kadhaa, hawatoi taarifa kuhusu faida kwa kila hisa kila mwaka. Wanapotoa taarifa yao *audited accounts* lakini hawasemi kile kipengele cha *earning per share* yaani faida kwa kila hisa. Wala *dividend per share* gawio kwa kila hisa hawatoi na matokeo benki hii imekuwa ikiwapa wanahisa wake magawio madogo sana kulinganisha na mapato kwa kila hisa. Napenda nitoe mfano, kwa mfano mwaka 2006 mimi nime-*take trouble* kufanya *compatation* kufanya hesabu kuona katika faida yao walipata shilingi ngapi kwa kila hisa. Faida yaani *earning per share* ilikuwa shilingi 260/= kwa hisa. Lakini gawio lilikuwa shilingi 17/=. Faida ya shilingi 260/= kwa hisa gawio shilingi 17/= kwa hisa. Mwaka 2007 faida shilingi 156/=, gawio tena shilingi 17/=. Kwa hiyo, utakuta kwamba hii *disclosure* haitolewi kwa hiyo mwenye hisa hana pa kupimia, anadhani amepata gawio nono kumbe sio nono. Kwa hiyo, nilitaka kuzungumzia hili suala kigezo hicho cha *adequate disclosure* kiwe kinatazamwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu katika baadhi ya makampuni yetu kuna d*iscrimination* wanazofanyiwa baadhi ya wanahisa. Kwa mfano, katika benki hiyo wanasema mtu akiwa mwanasiasa haruhusiwi kuwa Mkurugenzi, au Mkurugenzi akichaguliwa kuwa Mbunge tu kawa mwanasiasa kwa hiyo lazima ajiuzulu. Sasa katika sheria *Cap. 212* nashangaa mambo kama hayo na chombo kinachoweza kuangalia kwamba mambo hayo yanawekwa sawa ni *CMCA.* Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri utupie macho na utoe maelekezo yanayohitajika. Nimetoa *CRDB* kama mfano, na tutafurahi Mheshimiwa Waziri kama utatuambia unaweza kuchukua kusaidia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ningependa kuchangia linahusu msamaha wa kodi ya *VAT* ambalo Mheshimiwa Waziri ulitamka jana na umerudia leo katika sheria hii kuhusu uvunaji na usafirishaji wa miwa. Sasa mimi napenda kuuliza, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri vipi ameishia tu kwenye miwa wakati kuna mazao mengine yenye hali kama hiyo hiyo. Nikitaka kuwa muwazi niseme kabisa vipi uvunaji na usafirishaji wa chai? Huko kwenye chai nako kuna *out growers* na kuna hali

kama hiyo hiyo, vivyo hivyo kwenye magogo. Kwenye uvunaji wa magogo, uvunaji wa misitu kwa mfano, msitu wa *Sao Hill* nako kuna uvunaji wa magogo na usafirishaji. Kwa hiyo, ningependa kumsihi sana Mheshimiwa Waziri, labda ninukuu kutoka lugha ya kiingereza maneno yanayosema *what is good for the goose is good for the gender* yaani kilicho sahihi kwa *goose* nadhani huyo ndiyo jogoo ni sahihi pia kwa *gender. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sijui ndiyo temba wa bata huyu *gender*. Nasema pia nirudie kwa tafsiri maneno hayo kwa kusema kilicho sahihi kwa miwa basi ni sahihi kwa chai. Ni sahihi kwa magogo ya msitu wa *Sao Hill*, kama ni vyama vya wavunaji, vyama hivyo pia vipo. Kule Rungwe kuna *Rungwe Tea Growers Tea Association* ndiyo inayowaunganisha wakulima wa chai. Vivyo hivyo katika msitu wa *Sao Hill* wanacho chama cha wavunaji wa magogo.

Kwa hiyo, kuhusu chai ningeshauri kabisa inafaa chai *VAT*. Isiwe kwenye majani mabichi wala kwenye usafirishaji wa majani mabichi kama vile ilivyofanywa kwenye miwa bali iwe kwenye *packed tea*, chai ambayo imekwishawekwa kwenye paketi iko *blended*. Iko tayari kwenda kwenye soko, vivyo hivyo kwenye magogo isiwe kwenye misitu isiwe kwenye magogo wala usafirishaji wa magogo bali *VAT* iwekwe kwenye mbao, hapo tutakuwa kile kinachofanyika kwenye miwa kitakuwa pia kinafanyika kwenye chai na kwenye magogo.

Ningependa kusema na kwa mazao mengine yanayofanana na hayo, nimezungumzia mimi chai na magogo kwa sababu hayo ni mazao ninayoyajua vizuri yako katika jimbo langu la Mufindi Kaskazini na pia yako katika jimbo la mwenzangu Mheshimiwa Benito Malangalila, Mufindi Kusini. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri kama alivyofanya kwenye miwa, atutamkie hapa Bungeni kwamba utaratibu kama huo *VAT* itafutwa kwenye majani mabichi na kwenye magogo na kwenye usafirishaji wa mazao hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ambalo ningependa kuchangia linahusu kiwango cha *VAT* cha asilimia 20. Ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri hii asilimia 20 ya *VAT* kwa Tanzania inafananaje na wenzetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani wenzetu wa Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi? Kumbukumbu zangu zinaniambia wenzetu wako kwenye karibu asilimia 16. Mimi nashauri wakati umefika na sisi tungeteremka tufanane na wenzetu iwe asilimia 16. Kufanya hivyo siyo kwa kutaka tufanane tu ni kwa kutaka tupate mafanikio wanayopata wenzetu kutokana na kuwa na asilimia 16, *compliance* inaongezeka ukipunguza asilimia inayotozwa. Kwa hiyo, ule muitiko wa wafanyabiashara wenyewe kwenda kulipa unaongezeka zaidi kiwango, ile *percentage* ikiwa imepungua na matokeo ni ongezeko kubwa la mapato ya Serikali. Kwa hiyo, ningemshauri sana Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa kuchukua hatua kama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la nne linahusu kodi ya mapato *income tax*. Kiwango cha chini katika kumbukumbu yangu cha kuanza kulipa *income tax* ni shilingi milioni 20. Nashauri Wizara iangalie uwezekano wa kupandisha kiwango hicho kiende milioni 30 au milioni 40 lakini wafanye mahesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi kama huo utasaidia kukuza kwa haraka sekta isiyo rasmi *informal sector.* Tukichukua hatua ya kukuza kwa haraka *informal sector* kuna faida sana ya kuongeza watu wanaotajirika. Kwa miaka mingi katika Bunge hili kuzungumzia katika kukuza matajiri lilikuwa linaonekana kama jambo baya. Lakini ninachozungumzia hapa hatua…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mungai, naona ya pili hii.

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Ni ya pili, basi nadhani mchango wangu wamekwishausikia, napenda kumalizia kwa kusema naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Isipokuwa hukusema na mimi nalima chai. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Job Ndugai, nafikiri na Mheshimiwa John Cheyo sijui yuko wapi?

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye *Finance Act, 2008* kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa na Waziri wa Fedha. Mimi ni Mhifadhi Kitaaluma na ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Sheria hii kuna maeneo imenigusa nikakosa uvumilivu nikasema ngoja nisimame niseme kidogo. Ninachotaka kusema kinahusu sana sana sehemu ya 10 na sehemu ya 11 ya Muswada huu.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha anataka tumpe nguvu ya kisheria ili apate madaraka ya kuchukua kiwango fulani cha fedha kitakachoingizwa kwenye *Consolidated Fund* na kuwa *treated* kama *public fund.* Pia kwa sehemu ya 10 na sehemu ya 11 Mheshimiwa Waziri wa Fedha anaomba mamlaka ya *approval* ya *budget* za *TANAPA* na Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata taabu kidogo katika mambo haya mawili. Nilipotazama sana Sheria hii inaelekea kama Mheshimiwa Waziri alikuwa na nia ya kuchota fedha hizi na madhumuni ya kuchota fedha hizi nimeyaelewa wala sina matatizo nayo. Lakini inaelekea alikuwa na nia ya kuchukua fedha hizi kutoka kwenye mashirika fulani fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiyatazama yale mashirika mlolongo wake hayaowani na alipoingiza Ngorongoro na *TANAPA* ziko *regulatory authorities* na yako mashirika mengine ya huduma. Halafu akaingiza Ngorongoro na *TANAPA*, nikashindwa kuelewa hii Ngorongoro na *TANAPA* ameiingizaje katika *group* hili ambalo linaonekana kama ni mafuta na maji. Kwa sababu mashirika haya mawili Ngorongoro na *TANAP*A si mashirika ya biashara, ni mashirika ya uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni masharika ya kukuza utalii katika nchi yetu. Ule utalii katika nchi yetu una faida nyingi zaidi ya kile ambacho kinakusanywa na *TANAPA* na Ngorongoro ambako Serikali inapata huko kwingine kwingi tu. Tuchukue mfano wa Ngorongoro, imeanzishwa kwa Sheria ya Bunge, Ngorongoro imepewa majukumu

makubwa matatu. Jukumu moja ni kukuza utalii, jukumu la pili kuangalia rasilimali ile ya wanyamapori pamoja na malikale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la tatu ni kuhakikisha inaendeleza wakazi walioko ndani ya hifadhi ya Ngorongoro, kuwaendeleza Wamasai. Jukumu ambalo lilikuwa la Serikali lakini limepewa mamlaka hii ambayo nayo ni ya Serikali.

Kwa hiyo, hakuna maneno. Katika kazi hizo wanazofanya wale wananchi wa Ngorongoro hawaruhusiwi kulima mle ndani. Kwa jinsi hiyo Mamlaka ya Hifadhi inafanya kazi nyingi sana za kusaidia kuhakikisha wanapata chakula, kuhakikisha mahitaji ya mifugo yao yanatekelezwa, kuhakikisha wanajenga majosho, kuhakikisha huduma za maji zinapatikana, kuhakikisha mashule yanajengwa, kuhakikisha zahanati na hospitali zinajengwa na kadhalika kule Ngorongoro ambayo ni majukumu ya msingi ya Serikali. Shirika lake linafanya, sasa leo tena Waziri anataka kwenda kuchota kule kule, inanipa taabu kidogo. Mashirika haya ndiyo yanayoongoza katika kutangaza utalii wa Tanzania na vivutio vyake nje ya nchi, *The Land of Kilimanjaro, The Land of Serengeti, The Land of Zanzibar.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wimbo huu unaimbwa dunia nzima ni mashirika haya yanayoongoza katika juhudi za kutangaza utalii na hata Mheshimiwa Rais alikuja hapa juzi akaeleza kutangaza utalii ni ghali. Ndiyo ukaja ule mfano sitaki kuurudia. Hata *Tanzania Tourist Board (TTB),* kwa sehemu kubwa ambao wana jukumu kubwa la kutangaza utalii wanapata uwezesho kutoka *TANAPA* na Ngorongoro ili waweze kutangaza utalii katika nchi yetu. Ni jukumu kubwa sana, wanapaswa kuangaliwa kipekee. Mashirika haya yanalipa kodi inaitwa *Corporation Tax.* Mwaka jana Ngorongoro peke yake imelipa karibu shilingi milioni 800 kwa miezi mitatu.

Kwa hiyo, imelipa karibu shilingi bilioni tatu kwa mwaka mmoja Ngorongoro peke *Corporation Tax*, *TANAPA* imelipa karibu shilingi bilioni 10, 11 kwa Serikali. *TANAPA* mwaka jana tuliposema tuwatoe watu Ihefu zoezi la Kitaifa, wametoa fedha karibu shilingi bilioni tano katika kufidia wale wananchi wa kutoka pale au zaidi. Ngorongoro imekuwa ikitoa watu wavamizi walioko kule ndani kwa kutumia zaidi ya shilingi bilioni tatu mwaka jana na wataendelea na mwaka huu na mwakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya huduma na kuboresha huduma ndani ya Hifadhi za Taifa, barabara zote zilizoko ndani ya Hifadhi za Taifa na ndani ya Ngorongoro hakuna hela ya *TANROAD* pale, kununua magreda, kujenga madaraja, kuchonga barabara, kila shughuli iliyofanyika, kujenga nyumba za wafanyakazi na kadhalika ni masharika haya yanafanya yenyewe hayapati fedha moja kwa moja kutoka Hazina baada ya Serikali kusema sasa tumieni sasa hizo, jambo ambalo ni jema kabisa. *(Makofi)*

Vile vile *TANAPA* inasaidia wananchi ambao wako jirani na hifadhi zote za Taifa kwa kusaidia ujenzi wa shule, ujenzi wa zahanati na kadhalika na sehemu zote zenye hifadhi. Lakini hifadhi zenye mapato kwa mfano kwa *TANAPA* ni kama tatu tu au nne, Serengeti, Ngorongoro, Manyara kidogo, tatu, nne hivi. Nyingine hizi lazima zijengwe

taratibu, zijengewe utaratibu kidogo kidogo zikijengewa miundombinu zilindwe vizuri baada ya muda zitafikia kiwango na zenyewe za kupata watalii wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano juzi hapa Bunge hili tumewapa *TANAPA* Hifadhi ya Mkomazi, tumewapa *TANAPA*, Hifadhi ya Kitulo, zinahitaji miaka mitano hadi kumi au zaidi ya kufanya ulinzi kamilifu ili idadi ya wanyama iongezeke ili ifike mahali hifadhi zile ziweze kupata watalii. Katika miaka yote hiyo maana yake unatumia kidogo ulichonacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikumbushe tu hapa katika mambo haya ya utalii tunashindana na majirani, nchi ya jirani yetu Kenya, wana shirika lao moja tu kubwa linaitwa *Kenya Wildlife Service*. *Kenya Wildlife Service* wanatumia hela yote wanayokusanya kukuza utalii, pamoja na kutumia hela yote wanayokusanya *Kenya Wildlife* inapata ruzuku ya Serikali ya Kenya kuiongezea uwezo. Sisi tunafikiria tena shirika letu tuweke sindano pale tufyonze tena kidogo, halafu tunategemea tutapata wakimbiaji wazuri kama wale wa kwenye *Olympic*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ninayoisema hapa ni kwamba jambo hili litazamwe vizuri mashirika haya yameingizwa, iko hali ambayo imejengeka ya kufikiri kwamba kuna hela zinalala lala pale, mambo haya sio kweli. Utalii ni kitu ambacho ni *very fragile!* Biashara hii ni *very sensitive!* Ikitokea tu kukuru kakara fulani kidogo tu, watalii wanakatika kesho asubuhi. Pakitokea tu labda *terrorism* au mambo mengine yoyote, watalii wanapotea. *TANAPA* na Ngorongoro ni lazima waangalie, ikitokea kipindi kama hicho kikachukua miaka miwili/mitatu, hifadhi zetu zitakuwaje? Zitasambaratika!

Kwa hiyo, ni lazima katika kufanya kwao kazi waweke na akiba kidogo ya kesho, siku ya jua, siku ya ukame, pakitokea hali imekuwa sio nzuri tunafanyaje? Sasa Mheshimiwa Waziri akisema pale pale ndio anapiga panga tena, itakuwa sio sawasawa katika masuala ya uhifadhi. Wanyama hawa hawana mtu wa kuwasemea. Siamini sana kama Wizara ya Fedha kweli kuna huruma ya wanyama. Sisi wengine tumesomea mambo hayo na tunawaonea huruma sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sema, wewe ndio unayesema sasa.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni rahisi sana mtu aliyesomea fedha akaona fedha akakata fedha, lakini asiwaone wanyamapori. Ni rahisi sana! Kwa hiyo, naomba sana jambo hili litazamwe vizuri. Ile sheria yenyewe, tatizo langu pale inasema kwamba yeye Waziri wa Fedha atakuwa na mamlaka ya kuchukua fedha na kazi ya Waziri wa Maliasili na Utalii itakuwa ni ku *submit* zile bajeti.

Sasa ninachotaka mimi angalau basi liwekwe neon, haya mambo yatafanyika *in consultation with* na Kamati husika imependekeza jambo hili. Imependekeza kwamba, tuondoe mgongano kati ya Wizara husika na mamlaka husika na Wizara husika ile Wizara mama. Tusiweke tu hapa kwamba Waziri wa Fedha ana mamlaka, ninamwamini kabisa Mheshimiwa Waziri Mkulo, sina tatizo naye wala Manaibu Waziri wake, lakini

tunapotunga sheria tunaangalia jambo la miaka mingi. Mara nyingi *sweeping powers* zina matatizo. Ukishaiweka katika sheria, kesho watasema, Wabunge si mlipitisha?

Kwa hiyo, ninachopendekeza hapa, liwekwe suala la majadiliano. Kwanza suala lenyewe ikiwezekana lisiingizwe humu ndani, la italazimika kwamba ni lazima liwemo, basi pawepo na majadiliano na katika sheria hii vitajwe, kama Kamati ilivyosema, vigezo vipi vitatumika kama mwongozo wa makato hayo? Isibakie tu kwamba Waziri wa Fedha atakata, ni mwongozo gani utatumika katika kukata fedha hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamalizia kwa kusema kuwa tutazame suala la uhifadhi katika nia yetu ya kuendeleza utalii. Majuzi hapa tuliita mkutano mkubwa sana wa Sulivan na Mheshimiwa Rais yuko ziarani Marekani, pamoja na mambo mengine ni kutangaza utalii. Tuna nia kubwa ya kutangaza utalii kwa faida kubwa zaidi za nchi yetu.

Kama nilivyosema mwanzo, ni kwamba mashirika haya ndio yanayotusaidia kwa kiwango kikubwa kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, tuyatazame kipekee, tuyawezeshe, tuyape fursa katika kushindana na majirani zetu *Kenya Wildlife Service*, shirika moja peke yake na linawezeshwa. Uganda wana shirika moja tu linaitwa *Uganda Wildlife Authority (UWA),* wanatumia fedha zao na Serikali inaongeza fedha pale.

Kwa hiyo, twende katika utaratibu huo ambao hata katika *region* ndivyo inavyokwenda. Tukienda na utaratibu huo ambao nimeshasikia hata kwenye magazeti baadhi ya Wizara ya Fedha, huko kuna hela zinatumika vibaya, nyimbo ambazo wakati mwingine sio kweli sana, kama yako matatizo, tuyasaidie mashirika yetu haya yakae sawasawa. Kama wako watendaji ambao ni wabovu, turekebishe. Tupeleke Wahasibu wanaojua kazi kuliko kuyashutumu na kuanza kuyaingiza kwenye mpango wa kukata hela.

Jambo hili la kukata hela wala sio geni, Tanzania tuna hizi hifadhi nilizozitaja, tuna mapori ya akiba *(game reserves)*. Mapori ya akiba yamekuwa yakikatwa hela na Hazina miaka nenda, miaka rudi kama *Selou* ambayo juzi Mfalme wa Swaziland alikuwa kule. *Selou* imekuwa inaingiza hela nyingi, hela wanayopata haifiki asilimia 30 ya fedha wanazoingiza kwa sababu ni *game reserves,* ziko Serikalini, hela inakatwa na Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa sasa na wasaidizi wake angalau mwaka huu wanawapa *Selou* nusu ya fedha watakazokusanya, asilimia 50. Sasa ninachoona, inatakiwa sasa *TANAPA* na Ngorongoro nao wanaingizwa kwenye utaratibu huu huu wa *Selou* ambao tumekuwa tukikata hela wale wana-*suffocate.* Kaangalie miundombinu ya *Selou* leo, *Selou* ndio mbuga kubwa Afrika nzima, *Selou* ndio majivuno ya Tanzania, ina tembo wengi zaidi. Hakuna hifadhi Afrika nzima na dunia nzima yenye tembo wengi kuzidi ya *Selou.* Mpaka Mfalme wa nchi nyingine anakuja kwa ajili ya kwenda *Selou,* lakini bajeti yake iangalie! Angalia miundombinu yake! Lakini inaingiza mapato ya kutosha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya hii *concept* hii, ndio maana nikasema nisimame niongee maneno haya kwa upendo kabisa, nimwombe Mheshimiwa Waziri aliangalie jambo hili linavyopaswa litazamwe. Mambo haya ya uhifadhi kwa kweli yanahitaji yatazamwe kivyake, tuyalee vizuri ili yaweze kwenda tusiyaangalie kama vile ni biashara tu na kukata hela hapa na pale. Tuyape uwezo, tuyajengee uwezo na nitashukuru sana kama hoja yangu itasikilizwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia machache kwenye hoja hii muhimu. Kwanza, nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hiyo na pili nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wote wawili, Katibu Mkuu na Wakurugenzi na watendaji wote ambao wanafanya kazi chini ya Wizara hii. Baada ya shukrani na pongezi hizo, unisamehe kwa mara nyingine tena nitoe rambirambi kwa wananchi wangu wa Jimbo langu kwa sababu juzi tena kaliwa mtu mwingine wa 16 na simba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo kama nilivyoeleza mara ya kwanza. Pamoja na jitihada kubwa za Mkuu wa Mkoa, *DC* na vijana wetu wa Wizara ya Maliasili, lakini bado juzi kaliwa mtu mwingine wa 16 katika kipindi kifupi tu. Inasadikiwa kwamba wako, ingawa wameuwawa simba wawili, lakini bado wako simba wawili na watoto wawili. Sasa hao wenye watoto naambiwa ndio wakali zaidi. Simba akishazoea kula nyama ya mtu, basi sasa anasahau habari ya nyama nyingine, yeye kila wiki atatafuta nyama ya mtu. Naomba sana Waheshimiwa wote viongozi wanaohusika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Maliasili, washirikiane na Mkuu wangu wa Mkoa na *DC* wangu ili tuondoe tatizo hili kwa sababu wananchi sasa wanashindwa kufanya kazi zao kwa hofu ya simba.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anawasilisha maelezo yake hapa, amegusa kitu kimoja tu kwamba amegusa vitu vingi, lakini nasema kitu kimoja ambacho nataka niseme, ni lile suala la kupunguza ushuru katika mafuta mazito kwa minajili ya kusaidia kupunguza gharama za uendeshaji za viwanda vyetu. Ni wazo zuri, lakini tatizo langu, hii sio mara ya kwanza ama ya pili, kwa azma nzuri ya Serikali ya kupunguza ushuru ili kusudi viwanda hivi vipunguze gharama za uendeshaji.

Mimi nadhani shabaha yake ni kwamba viwanda vikishapunguza gharama za uendeshaji na sisi sasa au mlaji naye atapata nafuu katika gharama hizi. Mheshimiwa Waziri Mramba, bahati mbaya tu hayupo hapa, alipokuwa Waziri wa Fedha alifanya hivyo hivyo, ilikuwa mwaka 2002 kitu kama hicho, lakini wewe ni shahidi hakuna siku bati, simenti, sijui chuma, sijui nini kimepungua bei. Pamoja na jitihada hizo, hakuna hata siku moja bei imepungua. Kazi ni moja tu, bei kwenda mbele, hakuna kurudi nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndio najiuliza, hii misaada inayotolewa na nafuu mnazotoa hata katika maeneo mengine, tunasema kwamba tunatoa misaada ili kusudi angalau gharama zipungue tumsaidie huyu mwananchi. Hakuna! Mimi sioni! Wapi! Sasa hii kwa kweli tunawatajirisha na kuwafaidisha hawa wenye makampuni na wenye viwanda ndio wanaofaidika, lakini mimi kama mlaji au mwananchi wa kawaida mlalahoi

masikini ya Mungu anaendelea kubeba mzigo siku hadi siku. Wewe ni shahidi kwamba bei ya simenti, afadhali kule Mbeya karibu na jirani zako, ninyi angalau mna kiwanda cha simenti pale, bei inawezekana ikawa ni ahuweni, sina hakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Singida, Tabora, Mwanza, Kigoma, Rukwa, ni hoi bin taabani kwa sababu ya bei hizi, lakini tunaambiwa hapa tunatoa nafuu ili kusudi gharama za uendeshaji zipungue na hatimaye gharama za bei za bidhaa mbalimbali kama nilivyosema bati, simenti, na kadhalika nazo zipungue, hamna!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niambiwe hivi, Serikali ina *mechanism* gani watakayoitumia katika kuhakikisha kwamba hili kusudio zuri ambalo wamelifanya kweli mnamsaidia mwananchi wa kawaida? Ningependa Mheshimiwa Waziri aje aniambie kwamba wameweka nini? Watafanya nini ili kusudi kuhakikisha kwamba hili lengo zuri kweli linamsaidia mwananchi wa kawaida na sio linaendelea tu kumjazia faida huyo mwenye kiwanda au wenye viwanda? Kwa mfano, tulipoambiwa kwamba sasa hawatatumia mafuta ya kawaida, watatumia gesi, tuliambiwa nia ni kuwapunguzia gharama za uendeshaji na kwamba bei zetu zitapungua. Wapi?

Gesi wanatumia sasa karibu viwanda vingi, lakini hakuna kupungua simenti, hapana kupungua bati, hapana kupungua sijui nyundo, kazi ni moja tu hiyo hiyo kila siku, bei zinapanda kiasi kwamba hata ile nia nzuri kwamba mwananchi atapata maisha bora, nayo haionekani. Basi naomba Mheshimiwa Waziri aniambie baadaye kwamba wataweka *mechanism* gani ya kuhakikisha kama Serikali, hili kusudio zuri linapata mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nilitaka niliseme katika kifungu cha 50(a)(iii) katika masuala ya *VAT*, shughuli za upakuzi na upakizi bandarini, wataalamu wanaita *still dowering.* Kwa namna nilivyosoma inaonekana kwamba wanastahili kulipa *VAT* ya asilimia 20 na wakati sheria ya *VAT* inaanza mwaka 1997 kama nakumbuka sawasawa shughuli za upakizi na upakuzi bandarini yaani *still dowering activities* zilikuwa *zero rated,* lakini marekebisho yalifanywa mwaka 1999 na shughukli hizo sasa zikaanza kuwa zinatakiwa kulipiwa *VAT.* Sasa maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba wenye meli au *agent* wa meli ndiye atakayelipa hizi asilimia 20 na akishalipa *definately* wenye meli wataona kwamba bandari yetu hasa ya Dar es Salaam itakuwa *the most expensive port* katika *region* yetu hii. *Already* wanajua kama tunayo matatizo ya msongamano ambayo hivi sasa yapo ambayo yanaifanya bandari yetu ionekana kwamba sio nzuri sana kupitisha mizigo. Sasa tatizo lipo na wewe unakwenda kubandika msumari mwingine wa moto, maana yake ni bandari hii itakuwa haifanyi kazi sawasawa, wenye meli watakimbia watakwenda katika bandari nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, yamekuwepo mawasiliano mengi sana kati ya Wizara ya Fedha na *TPA* na Wizara Mama, kwa maana ya Wizara ya Miundombinu, kueleza jambo hili. Hata mimi juzi hapa nimekwenda kwenye Kamati ya Fedha ili nipate nafasi ya kuwasiliana na Waheshimiwa hawa kwa sababu kwenye Kamati yangu ya

Miundombinu jambo hili tumelizungumza sana, sasa sina hakika pengine sijasoma vizuri, nimepata kitabu hiki haraka haraka hapa, inawezekana yale ambayo tuliyazungumza kule wameyatilia maanani na watayachukulia hatu. Sina hakika, kwa sababu sijayaona hapa. Kama wamefanya hivyo, nawapongeza, nawashukuru, lakini wanivumilie nimalizie kwa sababu ndio utaratibu ulivyo kwamba bado sijaona hilo limefanyika.

*TPA* wamejaribu kujenga hoja, wamekwenda mpaka kwenye vyombo mbalimbali vya rufaa ambavyo vinasaidia kutoa sijui niite haki au ufafanuzi au msaada wa tatizo lao hilo, kwa mfano, kwanza, walienda kwenye *Tax Revenue Appeals Board* miongoni mwa vyombo ambavyo wamekwenda. Walipofika kule ikaonekana kwamba kwa sheria ya wakati ule ilivyokuwa, *TPA* walilazimika kulipa kwa sheria ilivyokuwa wakati ule, lakini wataalamu wakasema hawa wana hoja lakini hoja hii kwa sasa hivi haiwezekani kwa sababu sheria haiwaruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyo Mwenyekiti wa hiyo Bodi akasema hivi, naomba kunukuu: "*The appealant is strongly advised by the Board to revive the ministrial intergration regarding the possibility of reintroducing zero rating of still dowering services in the first schedule to the VAT Act.*" Mwanzoni walienda kwenye chombo cha *TRA* ambacho kilikuwa *chaired* na Mheshimiwa Kasera, naye akaamua hivyo hivyo kwamba kwa sheria ilivyo lazima walipe.

Lakini wakasema, naomba nisome walivyosema: *"However he have the view that idealy these services should be zero rated,"* anasema: *"idealy these services should be zero rated as the case of other services relating to foreign going ships and aircrafts including pilot charge, towege, handling and towege of all which are currently zero rated, he advised TPA to propose to the Minister for Finance for zero rating average services on that if the proposal is accepted with the restropective effect the assessment will be adjusted accordingly."*

Hivi vyombo vinasema kwamba, hoja ipo. Sasa haya waliyoaingiza *TPA*, wamefanya wamepeleka hoja yao kwamba jamani ee, huko tumemalizana, tumeambiwa tulete, tumeleta. Sasa nasema, siioni humu katika Muswada huu, sina hakika kama hilo limezingatiwa au halikuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Mombasa hawana kitu kama hiki, wenzetu wa Afrika Kusini hawana kitu kama hiki, wenzetu wa Msumbiji katika bandari zao kule hawana kitu kama hiki na hizo ndio bandari ambazo tunashindana nazo. Kama mambo yetu sisi sio mazuri, maana yake watu watakimbilia kwenda Mombasa, kwenda Msumbiji na kwenda Afrika Kusini. Soko sisi hapa linazidi kupotea. Hivi kuna tatizo gani? Hivi hiyo kweli *economicaly* ita-*affect* uchumi wa nchi hii kwa kiasi gani kwa kuifanya hiyo shughuli ya *still dowering* kuwa *zero rated?* Itaathiri kiasi gani uchumi mpaka ishindikane? Watu wanalia siku zote hapa ma misamaha chungu nzima kwenye madini ambayo yana fedha chungu nzima lakini watu wametia pamba masikioni, hawasikii wala hawaoni. Eeh! Leo hili dogo tu linaonekana kwamba labda limekaliwa wee, utafikiri sijui kuna tatizo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, athari ambazo zitatokea kama hilo likitekelezwa athari zake ni kwamba wakishatumia bandari hizo nyingine huko fedha zinazokwenda Serikalini, *TRA* kupitia *corporation tax* na kupitia hizi kodi za kawaida kwenye *VAT* na kadhalika haitakuwepo kwa sababu kutakuwa na upungufu wa shehena ya mizigo kwa wastani wa asilimia 40, kutakuwa na ukosefu wa mapato yanayotokana na *pilot charge, dokage, salvage, boyage, wafage, sawhandling and storage.* Kutapungua shughuli za wakala wa meli na wakala wa uondoaji wa usafirishaji mizigo bandarini, lakini pia kutapunguza kodi ya mapato inayolipwa Serikalini na *TPA* na wakala wa huduma za uondoaji wa usafirishaji mizigo bandarini kwa maana ya *clearing and fowarding agencies.*

Sio hivyo tu, kutapungua kodi ya ongezeko la thamani ya *VAT* kwenye huduma zinazohusiana na *domestic cargo.* Aidha kutapungua kodi ya ongezeko la *VAT* kwenye huduma zinazohusiana na mizigo ya *transit* kwasababu kama haji hapa kuleta mizigo yake hata *transit* atapeleka Mombasa, ana sababu gani kuja hapa? Kama hana *local cargo* ya Tanzania, atakwenda Mombasa atapeleka *transit cargo* atapeleka na *local cargo,* kwa hiyo, wewe yote hayo utakuwa hupati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile tunazungumzia hapa habari ya ajira milioni moja. Ajira itapungua hasa za vibarua. Sasa sera hapa inasema tuongeze ajira, wengine wanataka ajira zipungue. Sasa hizo sio *contradiction?* Kwa hiyo, ninachosema nilishazungumza na Mheshimiwa Waziri kupitia Kamati, walinielewa na kweli nilipoondoka pale mimi nilifikiri nimeeleweka, lakini nasema bado, inawezekana nimeeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tupate maelezo, lakini athari za kuweka *VAT* kwa *still dowering activities* zitaathiri sana uchumi wa nchi hii, bandari ya Dar es Salaam ambayo tayari imeanza kukimbiwa na wenye meli, itakimbiwa zaidi na itakuwa maana yake ndio haifanyi kazi, lakini Serikali pia isiangalie zile tu ambazo watapata, lakini watakopa *corporation tax* na kodi nyingine ambazo mamlaka wangelipa, ambazo *clearing agent* wangelipa, ambazo watumiaji wengine wangelipa kama wenye meli wataendelea kutumia bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nasema naunga mkono hoja, lakini *seriously* naomba Waziri aliangalie hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.  Sasa namwita Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, lakini ziko dakika 10 tu.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba ni dakika 10 nitajitahidi kwa kadiri ninavyoweza angalau niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Fedha kwa kuleta hii *Financial Bill* nzuri, nawapongeza watendaji wake, wanajitahidi vizuri sana, naipongeza *TRA* kwa kujitahidi na kukusanya mapato makubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naungana na Wizara kwa kuamua kuchukua pesa kwenye mashirika yetu ambayo yanazalisha vizuri. Haya mashirika ni ya kwetu, lazima pesa nyingine ziende kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Lakini waangalie mashirika yawekwe yaweze kuendelea na wananchi pia waweze kupata hizo pesa kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kwa hiyo, shirika liwepo na lizalishe vizuri na pesa nyingine ziende kwenye *consolidated fund*, vizuri kabisa. Wao wafanye bidii ya kuzalisha zaidi na hiyo pesa inayokwenda kwenye *consolidated fund* ni lazima tuhakikishe kwamba inakwenda kwenye shughuli za maendeleo kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kodi kwa viwanda vya mafuta. Viwanda vya mafuta, yaani mafuta ya kula, kila mwaka vinakuwa vinalalamika viondolewe ushuru. Hakuna mwaka ambao hawalalamiki. Lakini nakwambia hawa wanadekezwa sana. Mbona viwanda vingine havilalamiki? Wanachukua mafuta kutoka Malaysia wanasema ni mafuta ghafi, lakini mafuta haya sio ghafi kwanza Malysia hawataki kuuza mafuta ghafi ili bei iongezeke, ni lazima wao wasafishe. Kwa hiyo, wale nadhani wanachukua kule wanajidai ni mafuta ghafi, lakini wakifika hapa wanapaki kwenye magaloni wanauza.

Kwa hiyo, hawa wamedekezwa sana. Mimi nashauri tena ushuru uongezeke ili wakanunue alizeti ambazo zinazalishwa hapa nchini wapunguze gharama za uzalishaji. Alizeti iko karibu kila Mkoa, sasa badala ya kununua alizeti za Watanzania wakulima Watanzania wanakwenda kununua alizeti za Malaysia, hiyo sio sahihi kabisa. Naomba Wizara iliangalie hilo. Kuna mafuta ya pamba, kuna mafuta ya karanga, yote hayo tunatakiwa tutumie sisi Watanzania tuondokane na utegemezi wa kutegemea watu wa nje. Sisi tunakusanya kodi, *then* kodi hii tunakwenda kulipa viwanda vya nje, viwanda vya Malaysia, viwanda vya Singapore, tujenge viwanda vyetu hapa ili Watanzania waweze kuendelea na wapate ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo nataka niingie kwenye ushuru wa mazao ya misitu. Mwaka jana wakati wa bajeti hapa Wizara ilipandisha ushuru wa mazao ya misitu pamoja na ushuru wa mazao kutoka maliasili kama wanyama kwa wawindaji wa kitalii. Kwa kuwa wale wawindaji wa kitalii wana pesa nyingi wamefanya *lobbing* kwa Serikali. Serikali imerudisha ushuru ule ule ambao ndio walikuwa wanatoza kabla. Lakini hawa Watanzania ambao wanavuna mbao kwa ajili ya kutumia kwa Watanzania wenzao, kwa kuwa wao hawana nguvu ya *lobbing*, ushuru huo haujabadilishwa. Sasa naishauri Serikali, kama walivyoondoa *VAT* kwenye mazao ya miwa na mazao haya ya misitu iangalie ni jinsi gani itapunguza kwasababu tunatumia sisi wenyewe hapa na ajira kwa vijana ni nyingi sana kutokana na uzalishaji wa samani.

Halafu la pili, niishauri Serikali sasa itamke kabisa kwamba kuanzia bajeti hii haitanunua tena samani kutoka nje, watu binafsi acha wanunue, lakini Serikali inatupa samani za mininga zilizotengenezwa imara inakuja kuagiza fanicha za kutoka Malaysia. Viwanda vya Malaysia ndio Serikali inapeleka kule pesa, kama kweli wao Serikali inataka maendeleo kwa Watanzania, wale Malysia waje wazalishe hizi samani hapa ili tununue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kila Wizara, sasa hivi ni samani za kutoka nje lakini hazidumu, ukiangalia ambazo zimeshaharibika nenda kwenye magodauni unakuta ni nhyingi mno kwa hiyo, ni pesa ambazo Serikali wananchi wana-*deposit* pesa, lakini Serikali kazi yake ni kutoa na kutumia bila utaratibu. Nashauri katika hilo Wizara ipige marufuku kabisa uagizaji wa samani kutoka nje, vijana wetu wanaweza kutengeneza. Hata hiyo meza hapo kwenye *podium* imetengenezwa na Magereza. Angalia, ni imara sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu naomba nizungumze mengine kwenye matumizi ya magari. Kama huko tunatazamia kwenda kwenye maisha bora ya Watanzania hatutafika kama hatutadhibiti matumizi ya Serikali. Hakuna sababu ya wafanyakazi wa Serikali kutumia magari makubwa ya shilingi milioni 120, shilingi milioni 100, lakini ya bei nzuri yapo na yanafanya kazi hizo hizo. Tanzania ni mojawapo ya mataifa ambayo yanatumia magari ya kifahari kuliko mataifa mengi mno hapa duniani, lakini sisi ni masikini. Kwa hiyo, kile kipato tunachopata tukitumie vizuri kwa faida ya wote, kama ni kuagiza magari tuagize kwa jumla. Nenda kwenye kiwanda, sema Serikali inataka kutumia magari 500 mwaka huu, uki-*order* kwa jumla kiwanda kitakupa kwa bei kama nusu, lakini tunatangaza tenda, atakaye-*win* ndiye atakayepata. Kwa hiyo, hawa ma-*agent* wa magari ndio wanatunyonya.

Kwa hiyo, naishauri Serikali iache kutumia magari ya kifahari. Barabara zetu sasa ni nzuri, kama yapo ambayo yanatakiwa kwenda kwenye *pool.* Kununua magari sio tatizo sana, lakini vipuri vyake, mafuta yanayotumia, pesa ndio inaishia pale kwasababu ukishanunua ni lazima uweke mafuta, ni lazima ununue *spare parts* na zile *spare parts* ndio ghali sana. Kwa hiyo, naishauri Serikali ipange vizuri ili pesa kidogo tuliyonayo itumike kwa Watanzania wote waweze kufaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, muda umekwisha. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Umesema machache na ukasema vizuri na watu wamekusikia vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, naomba, wanaoomba kuhusu kuchangia nimefunga orodha, sitapokea mwingine. Kwa sababu mchana tutakapoingia wafuatao ndio watapewa nafasi Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Dialo, Mheshimiwa Mporogomyi, Mheshimiwa Nywazwa, Mheshimwia Dokta Charles Mlingwa, Mhshimiwa *Professor* Mwalyosi, Mheshimiwa Lekule Laizer na Mheshimiwa Mnyaa na Mheshimiwa Kabwe Zitto. Hawa wakipata nafasi maana yake tutabakia na dakika 10 tu kabla ya kufunga saa, kwahiyo tutatumia madaraka ya kuongeza muda tupitie. Sasa haitakuwa Kamati ya Matumizi itakuwa Kamati ya Bunge zima, kwahiyo siombi majina mengine.

Baada ya kusema hivyo naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 07.00 Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Mchana nilishawataja ambao watazungumza, lakini naona moja mpaka tatu hawapo, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi atafuatiwa na Mheshimiwa Nyawazwa, Dr. Mlingwa na halafu Mwalyosi, Lekule Leizer.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza mchana wa leo ili nami nitoe mchango wangu kwenye *Finance Bill* hii. Jana nilipokuwa nazungumza nilichangia mambo mbalimbali yanayohusu uchangiaji wa kodi na nilieleza baadhi ya sehemu ambazo nilifikiri sikuridhishwa nazo na ambazo tumetoa misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba nipewe majibu nilipokuwa nachangia, lakini sikupewa majibu ambayo niliyahitaji na hasa kwenye maeneo yale ambayo najua tumekuwa tukitoa misamaha kwa *programmes* ambazo nafikiri ni *ant people*. Sasa nitaomba majibu sahihi na wala sitaunga hoja hii mkono. Kwa mara ya kwanza katika historia yangu ya kuchangia ndani ya Bunge sitaunga mkono hoja kwa sababu nimechangia hoja ya kwanza inayohusu mafuta ya kupikia. Naliomba Bunge lako Tukufu liniunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mafuta ya kupikia, ni dhambi kubwa sana kwa Taifa hili kwamba tunatoa unafuu wa kodi kwa mafuta yasiyokuwepo. Katika Taifa hili hakuna mfanyabiashara hata mmoja ambaye ana-*import* mafuta ya kupikia kutoka Malaysia, nitaeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, malighafi yote ambayo imekuwa inaingia katika nchi hii inakuja katika mikondo kadhaa. Mkondo wa kwanza ni ule unaosema *raw materials*, malighafi. Malighafi ili iingie hapa iweze kutengenezwa katika miaka ya 1990 ilitakiwa ifanyiwe mambo matatu. Jambo la kwanza ni kuya-*deodorise* haya mafuta. Jambo la pili ni kuya-*bleach* haya mafuta na jambo la tatu ni kuya-*nuerterlize* mafuta haya ili yaweze kutumiwa na binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo tulitakiwa tuwe na mashine au *equipment* inayoitwa *fractionation plants*. Taifa hili kwa miaka kumi iliyopita kutoka 1996 hadi 2006 tulikuwa hatuna *fractionation plants*. Lakini ukiangalia *imports* zote za mafuta yaliyoingia hapa nchini katika miaka ya 1990 mpaka 2000 na 2000 mpaka 2005 hatukuwa na kiwanda chenye uwezo wa kuyachambua chambua mafuta haya ili yaweze kuwa *fit for human consumption*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliteuliwa nikaenda Malaysia na Maofisa wa Hazina na najua hakuna Afisa wa Hazina anayeweza ku-*risk* jina lake kusema mafuta yale ghafi yanakuja. Nitaeleza utaratibu. Ili malighafi iruhusiwe kutoka Malaysia ni lazima nchi unayoyachukua yale mafuta uwe na *joint venture partnership* nao, kama huna unakuwa *subjected* kwa kodi ya kati ya thelathini mpaka arobaini *export tax* unatozwa na ukitozwa

kodi hii siyo wengi wanaweza kuichukua wakaenda kutoa kodi hii kwa sababu wewe utaiuza vipi uilete hapa? Kwa sababu wao wana mambo mawili wanayotaka kufanya, wanataka kulinda ajira zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, wanataka kupata *value addition* kwenye mazao wanayoyazalisha. Sasa kwa nini nasema hii ni *ant people?* Ni *ant people* kwa sababu hawa wafanyabiashara wengi wamekataa kuingia mikataba ya uzalishaji, walime mazao yale yanayoweza kutengeneza mafuta katika nchi hii, sisi hatuna *capacity* hiyo, wamekataa kwa sababu wana njia rahisi ya kupata faida. Tuna mawese, michikichi inalimwa Kigoma, tumewaambia wachukue mashamba kule Kigoma, hakuna anayetaka kuchukua mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, nenda Uganda, hawa akina Mkwana wote wamekuja hapa, wamechukua mashamba Uganda wanalima sana na wanatengeneza mafuta yanayotokana na malighafi ya ndani ya nchi. *So local capacity potential* yake ina-*generate employment* lakini mbali na ku-*generate employment* ni kwamba kuna *value addition* wanafanya na wana-*export* nchi nyingine na sisi *potential* hiyo kama Tanzania tunayo, ila sisi tunatumia ujanja ujanja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze, nchi hii tunaipeleka pabaya kwa sababu tunaingia humu Bungeni tukija na mikakati ya namna ya kutajirika katika Bunge hili. Hivi kuna biashara umewekeza humu Bungeni ili uje utajirike badala ya kufanyia watu kazi na waione? Ndiyo maana humu ndani tumegawanyika, lakini tumesema wale tunaokataa tunaochukia ufisadi Mungu anatuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimesema twende Malaysia, *I will be proved wrong* lakini kwamba tunatoa mafuta kwa kitu ambacho ni *obvious*, miaka miwili iliyopita tulikwenda kule tukaja ku-*convince* Serikali ikaweka kodi, *East Africa* nzima hata tulivyokuwa tuna-*negotiate customs tariff* za kwetu *basis* yake ilikuwa uchunguzi huo nilioufanya Malaysia. Nimetembea mpaka India, *they have a special programme* ya ku-*develop agricultural sector* ya kila kitu kama ni *Swiss* wanao utaratibu, lakini sisi ni ujanja ujanja tu wa kudanganya. Mafuta yanayoingia hapa nchini ni *95% to 98% refined* lakini hapa kodi *worthy billions and billions* inatumika, tunaambiwa kuna watu wanaleta malighafi hapa, hakuna anayeleta malighafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, humu Bungeni hakuna biashara ya kutajirika, wale wanaotaka kutajirika kupitia Bungeni hapa wakawaambie waliowachagua kwamba, sisi tumeshatajirika, sasa Bunge basi. Tuwe wakweli na maisha yetu! Neema tuliyopewa na Mwenyezi Mungu ni kuja humu ndani ya Bunge kuwatumikia watu waliotuleta humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumekuja humu ndani tunawatendea maovu wale waliotuchagua wanaotufanya tuonekane tuna neema mbele za Mungu. Mussa alipokuwa akifanya kazi ya Mungu, alipokufa, alimchagua Joshua akamwambia Joshua nakupa ujasiri na ushupavu kaifanye kazi yangu maana mimi sitakuacha. Wale mnaoamini kwamba tunahitaji kuwatetea maskini wa Taifa hili tuendelee kufanya hivyo na mafisadi

waendelee na mambo yao lakini nchi hii tuiendeshe kama watu wenye akili, sio kwamba hawajui, wanajua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza mwaka 1996 na 1997 kulikuwa na saga ya minofu ya samaki na naitamka kwa mara ya pili. Kilo moja ya *fish fillet* katika soko la Kimataifa ni dola tano mpaka sita, mwambie mfanyabiashara yeyote katika Taifa hili akwambie, anauza kwa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, humu ndani watu waliandika barua tuuze dola moja. Ukiuza dola moja wote hawa wanapata hasara. *So, they are subjected to exemption of tax*, hawalipi kodi, lakini ukweli wenyewe hakuna hata anaye-*export* kwa dola mbili, wale wanao-*export skinon fillet* ndiyo wanapata kati ya dola tatu na dola nne, nyingine zote *pure hundred percent fish fillet* ni dola tano au sita katika soko la Kimataifa, tunashindwa nini kufanya utafiti kisha tufanye yaliyo sawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewaambia shilingi bilioni mia tatu tunazokusanya *can not sustain this economy any longer*, ni 3.75 ya fedha wanazokusanya Kenya sio kwa sababu ya *difference* ya *development pattern* ya kwetu na ya Kenya, *the difference is huge*, lakini nchi hii tukijitahidi *the minimum we can collect and I bet* tunazoweza ni shilingi bilioni mia sita mpaka mia nane ya nchi hii, nyingine zote zinapotea kwa wizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapitia *Finance Bill* milioni mia tatu, lakini maskini kila siku wanaongezeka katika nchi hii, tunawapa mipango ya kwenda kuondoa umaskini huko kwenye vijiji vyetu, tunatoa mipango mingine hewa. Tunazungumza mipango ya *NGO* ndiyo inakuja kumsaidia maskini, una makubaliano gani na *NGO* kwamba ndiyo itakufanyia kazi ya kuendeleza watu? *NGO* wafanye kazi zao, Serikali ifanye kazi yake ya kuwajibika kulinda maslahi ya Watanzania. Tukifika hapo tunaweza kujivuna kwamba tunawatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuteuliwa ni heshima unayopewa na Mungu na yule anayekuteua. Nami nafikiri Rais wetu alivyokuja hapa juzi aliyokuwa anazungumza ni aliyoshauriwa na kuambiwa. Sasa nataka kutoa *caution* tu kwamba, jamani tujitahidi sana kumwambia Rais mambo ya ukweli ili asaidie Taifa hili katika kulileteа maendeleo yaliyo sahihi. Mkimdanganya, naye akipotoka, atatuambia yale yasiyo sahihi na utakuta wenyewe tunaumana, tunazungumza mambo yasiyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri mpango wa maisha bora ni mpango mzuri ambao unamfurahisha kila mmoja. Tutetee ukweli katika Taifa hili, maana mpango wa kuishi duniani ni mpango wa Mungu wala si wa fisadi. Mpango wa kuishi duniani kwa kuishi vizuri, kwa kuishi vyema ni mpango wa Mungu, wala si wa binadamu, tuwatetee watu waliotuleta humu ndani na lazima *pattern* yetu sasa ya kuwasaidia Watanzania ibadilike. Unaweza kuangalia hii *Finance Bill* ukazungumzia *virtually* vifungu vingi na ukapata maneno ya kueleza yasiyo sahihi. Jana nimeeleza vipengele, vyombo vya kuboresha teknolojia ya kuendeleza uzalishaji ndani ya nchi ili tukusanye kodi zaidi, vyote *they have been rendered incompetent completely! Where is TIRDO, where is TEMDO, where is CAMARTEC? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya maneno kwa uchungu mkubwa sana na imenichukua muda kufika mahali na kuamua kwamba lazima haya maneno niyaseme na Wabunge wenye nia njema na Taifa hili ni lazima wayaseme tena bila kuogopa. *We can not allow this*, Taifa hili ligeuke *man eat society*. Hapana! Lazima tujenge heshima ya Taifa, watu wetu tuwatengenezee mazingira ya maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye madini ni dhambi kubwa ambayo tumefanya, kwani ni lazima tu-*deplete* madini yote, tuyachimbe tuyamalize leo? Lazima tuchimbe kwa mikataba mibovu? Kisha tunawaona watu wetu hawana maana, tunawafukuza kabisa tunasema ninyi hamna maana, tokeni na wanatoka kweli! Jamani, hii ni aibu kubwa sana kwa Taifa letu. *Is unfortunate*, tumefikia mahali hapo, tumegawa mali za Taifa hili bila kujua!

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumzia habari ya mtu mmoja ambaye nilikutana naye katika benki moja ya Dar es Salaam, anasema pale watumishi wanaofanya kazi nchi hii wanaotoka nje, wanapokwenda kwao hawatozwi kodi, hapa wanakwenda kutoa kodi *South Africa*, vinginevyo zile fedha zote zinakwenda *off shore banking*, huko ambako hakuna kodi huko *Jamaica* na kwingineko.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wanaofanya vizuri, wanaolitumikia Taifa hili kwa mema nawapongeza sana na Mungu awabariki sana kwa sababu wapo wengi wanaolitakia Taifa hili mema. Wale wanaofikiri kwamba nguzo yao kubwa ni pesa, waendelee na nguzo yao ya pesa, lakini sisi tuna Mungu nyuma yetu na tutaendelea kutembea kwa kujivuna kifua mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii, lakini nimeona niyaseme haya, lakini kabla sijamaliza, ninachoomba kwa hili la kodi ya mafuta ya kupikia ambayo kazi nimefanya na watumishi wa Hazina tukaenda Asia, tukatembelea Malaysia, tukarudi, naomba ichaguliwe timu ya Wabunge watatu, hii kodi iwe *suspended* leo hii ili twende kuiangalia tulete majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, someni kanuni zenu vizuri maana hapa hata ukilia machozi ya damu, kama huna hoja ambayo sisi wenzio wote tutakuja kuamua, hujasema kitu, umesema tu masikitiko yako. Vinginevyo kama anavyosema Mheshimiwa Mporogomyi, kama *seriously* anayo alete hoja hapa wote tuamue tuifikirie na tuifanyie maamuzi. Hivyo alivyosema sio rahisi labda Waziri mwenyewe kama anajua habari hiyo aamue yeye, kufanya maamuzi yeye inawezekana.

Kwa hiyo, naomba sana mwelewe, tunavyo-*discuss* hapa, nguvu zetu zote, sasa hivi tuna kanuni mpya hoja binafsi zipo, Miswada ya Kamati ipo, vyote vipo, msipovileta kwa namna hiyo tutakuwa tunaendelea kusema kwa sauti halafu inakuwa hivi hivi.

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza, nakushukuru kwa kuniona kwenye orodha. Pia nimpongeze Mheshimiwa

Waziri kwa hotuba nzuri kuhusiana na Muswada huu wa Fedha. Namshukuru sana kwa sababu ameusoma kwa umahiri mkubwa, lakini pia kuna mambo mawili ambayo nataka kutoa kama angalizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwenye Kamati ya Fedha kuna mambo tulikubaliana tukategemea kwamba Mheshimiwa Waziri na timu yake watayachukua na kuyaweka kwenye masahihisho.

**NAIBU SPIKA:** Mmeyapata masahihisho enhee?

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshayapata, lakini haikufanyika hivyo. Sasa nasema hivyo kwa sababu wewe una miaka mingi hapa.

Kwa kawaida, Kamati zinapokuja na mapendekezo na mmekubaliana huko na Wizara au Waziri, kuyapuuza mapendekezo au mabadiliko yaliyoombwa na yakakubalika ni kutafuta *confrontation* na Bunge kwa sababu Kamati ile iko kwa niaba ya Wabunge wote walioko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hii itakuwa ni mara ya kwanza na ndugu yangu atakuwa na miezi kadhaa kwenye Wizara hii atakuwa anaanzisha *precedence* mbaya. Nasema hilo nitaeleza kwa kirefu, lakini pili kwenye Kamati ya Fedha tulionyesha wasiwasi wetu kwamba Wizara hii sasa inaanza kuwa *supra ministry* na nashangaa Mawaziri wengine wamenyamaza tu, kwa sababu hakuna Wizara ambayo ina nguvu kuliko nyingine, Wizara zote zinafanana. Haiwezekani kuwa na Wizara moja ambayo inaweza kukuingilia Waziri wa sekta nyingine akafanya anavyotaka kwa kisingizio cha *Public Finance Act*, nadhani ni kupotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara zote zina *equal power* na wana maamuzi yao. Kwa hiyo, kuamua ukachukue fedha kutoka shirika moja, kuna njia mbili tu unazoruhusiwa, aidha, shirika hilo kama linalipa kodi, yaani wanatakiwa kulipa kodi au wewe kama Serikali, kama ni *shareholder* usubiri ulipwe *dividend* kama kuna utaratibu huo. Vinginevyo ni kitu Wazungu wanakiita *money taking* ambayo sio halali kwa sababu mashirika yale yanajipangia bajeti zake, yanatakiwa yaendeleze mipango yake, wanatakiwa kuwa na akiba, sasa unafika mahali unasema fedha zilizobaki nazihitaji, maana yake nini? Maana yake ni kwamba, lile shirika hawatakiwi hata kuwa na *incentives* ya kutengeneza *excess which means* mashirika haya yatakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili ni kwamba, unayapa *incentives* au motisha ili yatumie fedha ovyo ili mwisho wa mwaka wasionyeshe wana fedha *excess*. Sasa nia ya Serikali sidhani kama ni hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kawaida Serikali hizi, tumeiga jinsi ya kuziendesha tangu *historically* Wahindi, hata Waingereza waliiga kwa *system* ya Kihindi. Uendeshaji wa Serikali ni ule ule sawa na kuendesha gari. Nikikupa gari yangu, *reverse* itabaki kuwa ni *reverse gear* ile ile, huwezi kubadili ukasema hili gari la Diallo nitaanza *reverse* kwa kuweka *gear* ya kwanza, utagonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda sana *doctrine* ya utawala ibaki pale pale, Wizara ziwe zinaheshimiana kati ya Wizara moja na nyingine. Wakitaka kuchukua fedha ni mpaka Waziri mhusika akubaliane, atoe *consent* na hatukutaka kusema kwamba wawasiliane, maana haya mambo ya kuwasiliana ni lugha ambayo haipo. Mara nyingi huwa haitumiki, mnaweza kusema kwamba tumewasiliana na wadau lakini hamuwasiliani na wadau, tumesema ni lazima iwe *consent in writing* kutoka kwa Waziri mhusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda kwenye sehemu nyingine kodi kulingana na *maxim* ya *taxation* ni lazima ziwe na sifa kubwa nne. Lazima katika kodi kuwe na *fairness*, lazima iwe *non arbitrary* na ni lazima kodi iwe *economic,* huwezi kutumia shilingi mia tano kukusanya shilingi mia moja na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mmetoa kodi kwa walima miwa, *process* na utaratibu wa biashara ya walima miwa ni sawa na walima kahawa, pamba na chai. Sasa Taifa hili ni moja, kuna *tax payers obligation*, lakini bado kuna *state obligation* kuhakikisha kwamba wananchi wake wote kwa *equity*, yaani kama unanitoza shilingi mia tano kwa *income* yangu ya shilingi elfu moja aliye na *income* ya shilingi elfu tano *definitely* utamlipisha kodi ambayo ni *proportional* kwa ajili ya ile *equity*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda sana nielewe kwa nini Mheshimiwa Waziri amebanwa hapa kuhusu biashara ya miwa aka-*give in*, kama una *give in* kwa ajili ya *equity* na kwa ajili ya kuwa *uniform* katika *application* ya sheria zetu, *it has to apply* kwa mazao yote ya biashara, vinginevyo ni vigumu kutokuelewa kwamba inawezekana Mheshimiwa anayeshika hili dau yuko karibu na walima miwa au walima miwa ni walipa kodi wake. Sasa mkitaka kutufikisha huko tutashindwa kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa pamba kila siku tunalalamika hapa kwamba, *cost* ya kuzalisha kilo moja sio tunayoipata katika kuuza kilo moja ya pamba, lakini watu wamefumba macho, leo malalamiko kidogo tu ya kodi kwa kuuza kwa sababu *tax* ipo kwenye *goods and service* kwa kuuza, *transfer for goods from point 'A'* kwenda *point 'B'* wanatoza *VAT* ambayo ni *legal*. Sasa tunalalamika hapa juu ya *exemption*. Hii ni *exemption* nyingine ambayo ita-*apply* kwa zao moja sikubaliani nayo. Kama ina-*apply,* basi i-*apply* kwa mazao yote ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema nitazizungumza hizi *maxims* nne, *principles* ambazo kodi lazima izifuate. Usipozifuata tunakwenda nje ya msingi na Bunge hili, tutakuwa tunahalalisha kwenda nje ya misingi ya utozaji kodi na kwa hiyo, tutakuwa hatuna sababu ya ku-*claim* ile *legitimacy* yetu kutoka kwa wapiga kura, kama nilivyoeleza kodi lazima iwe na usawa na *openness, tax* lazima iwe *convenient* na *it has to be non arbitrary, tax collectors*, naomba ninukuu kutoka kwa Adam Smith, nadhani watu wengi mmesoma, kwenye karne ya kumi na sita, anasema: "*Tax collectors can not be allowed discretion in amounts claimed as taxation or in a manner and timing levies or else they will be corruption.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, hamuwezi kujitungia tu kodi mradi mmekuja hapa, Bunge limepitisha kodi inakwenda kokote tu, hatufuati misingi, lazima tufuate misingi ya utozaji kodi. Huwezi kunitoza kwa sababu nina kitambi, unitoze shilingi mia tano na kwa ambaye ni mwembamba kama Mheshimiwa Nkumba unamtoza mia moja, hiyo sio kodi hata kama tuki-e*ndorse* hapa, ni *violation* ya *human rights*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona niishie hayo kwa sababu nimeudhiwa sana na Mheshimiwa Waziri kwa kutokutusikiliza sisi mliotuchagua kuingia kwenye Kamati na nadhani taarifa ya Kamati mmeisikia. Kwa hiyo, nitamwomba, bado ana ruhusa ya kubadilisha hata kwa mdomo hapo hapo alipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa sababu inawezekana hatuzifuati, lakini tunapofikishana, sasa tuwe tunawahi kuleta *motion of amendment* masaa ishirini na nne ya kabla. Ina maana kuna matatizo na hutafika mahali Mheshimiwa Waziri akalishinda Bunge, haiwezekani maana ku-*lobby* hapa tutaambizana, wametudharau kwenye Kamati na ndiyo *you went no where*, itabidi u-*withdraw* Muswada na hii mtu asikudanganye, *Finance Bill* siyo *three line whip*. Kwa hiyo, anayesema siungi mkono hoja atasema siungi mkono hoja. Mungu akubariki. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kwa kawaida Mawaziri mkifanya *amendment* mkirudisha kwenye Kamati mnapata amani zaidi. Nikikusomea kanuni hapa nitakuharibia kazi yako sasa hivi. Sasa tunaendelea Mheshimiwa Blandes.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kidogo hoja yetu iliyoko mbele yetu hapa. Naomba kwanza niunge mkono ingawa nitakuwa na malalamiko yangu huko baadaye, lakini naomba tu niunge mkono kabla ya kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria iliyoko mbele yetu, naomba nichukue nafasi kumpongeza Mheshimiwa Waziri kuungana na Kamati ilivyoeleza kwamba sheria hii inagusa makali ya maisha kwa wananchi. Sasa nitamwomba Mheshimiwa Waziri kama kweli anajua itagusa makali ya maisha ya wananchi nimwombe ushauri wangu kama ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wote waliochangia mbele yangu wamewasikia, sasa namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu amegusa kwenye Wizara nyingine awe na mawasiliano mazuri kabisa na Wizara hizo, kwa sababu amegusa makampuni mengine pamoja na mamlaka nyingine ambazo ziko kwenye Wizara nyingine. Naomba sheria hii isiwe msumeno kwa watu wengine kuhakikisha kwamba maelewano yanatoka. Naomba sana Mheshimiwa Waziri awe wazi kuelezea Bunge lako Tukufu vigezo atakavyotumia viwe wazi kwa mazungumzo pamoja na mamlaka ambayo yako ndani ya sheria hii ili kusiwe na mchanganyiko au kutokuelewana na Wizara ambazo nimezitaja hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kushukuru sana Muswada huu kuja mbele yetu kwa kueleza kwamba mifuko ambayo inasaidia sana mafao kwa

wafanyakazi, naishukuru Serikali imeona umuhimu wa kuweka mifuko hii ambayo imetajwa kwenye sheria hii kwamba kutakuwa na mawakala kusaidia baadhi ya watumishi.

Naipongeza sana Serikali kwa ajili ya mifuko hii ambayo imefanya kazi vizuri na inawekeza kwenye maeneo mengi ambayo tunaona na ule uwekezaji wake unarudisha faida. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Mfuko wa *PPF* pamoja na *NSSF* ambao walijitoa kwenda Mwanza na kuwekeza mahali pale. Naomba ndugu zangu kwenye Mikoa mingine mje mwone hawa *PPF* na *NSSF* walivyowekeza pale Mwanza na fedha zao zitarudi na uhakika wanachama katika mifuko hiyo wasiwe na wasiwasi wajue fedha zao zitarudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itakuwa imepunguza kero kubwa ambayo ilikuwa inajitokeza pale Hazina. Kama Serikali imejiandaa hivyo kushirikiana na mifuko hii, nafikiri wastaafu wengi sasa watapata fedha zao bila ya kuwa na mambo ya nenda rudi, nenda rudi ambapo walikuwa wanahangaishwa pale Hazina. Naomba sasa mifuko hii mtakapoanza kazi ya kuwa Mawakala wa Serikali mtusaidie sana. Lakini mbaya zaidi ni kwamba mifuko hii iko Mikoani. Mimi nimezungumzia mifuko ambayo iko Mwanza pale *NSSF* na *PPF* ambayo imewekeza pale. Lakini wastaafu wengi wako vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba basi kutumia sheria hii na uwezo wa Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba huduma hii inawafikia wastaafu huko waliko isogezwe angalau kwenye Wilaya. Mkoani ni mbali, fedha zinaishia tu kwenye nauli na fedha zao zinapungua. Sasa kama hii mifuko itakwenda mpaka Wilayani, itakuwa imewasaidia sana wastaafu wetu. Naambiwa kwamba pale Mwanza bado kuna nafasi kubwa tu, wamepewa viwanja kwa ajili ya hii mifuko, naomba wajenge na sisi tuko tayari kusaidiana na fedha zile zitarudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ombi langu. Kuna ombi moja nimwombe Mheshimiwa Waziri asiitumie sheria hii kuzigandamiza mamlaka hizi ambazo zinatajwa kwenye sheria hii.

Lingine naomba basi hebu Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia tuzo ambayo ameieleza ya miaka mitatu. Mimi naona miaka mitatu, Kampuni moja inasema kwamba haijapata faida. Kama hajapata faida si afunge biashara yake! Tumeibiwa vya kutosha! Kama kuibiwa, tumeibiwa vya na kutosha na Wabunge hapa wanatoa sababu kwenye madini na kila mahali. Naomba basi Mheshimiwa Waziri awe karibu sana kuona kwa nini tusiweke hata miaka miwili baadaye tunaangalia mahesabu yake. Kwa sababu tuna wataalamu wazuri sana wa *TRA* ambao wanatusaidia kuhakikisha kwamba huyu bwana anasema uongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tukusanye mapato kwa wingi, hatujafikia malengo ya kuwabana hawa wafanyabiashara wasio na risiti ndani ya maduka. Wafanyabiashara wengi wanawatumia wananchi kuwalaghai kuwaambia kwamba kama unataka risiti nitakuuzia shilingi laki moja, kama hutaki risiti nitakuuzia Sh. 50,000/=. Kwa Mtanzania kama mimi lazima nitasema usinipe risiti. Hapa tunapunguza mapato yetu.

Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Kamati ya Fedha na Uchumi imeshauri kwamba wale wa *TRA* wapewe mafunzo zaidi pamoja, wapewe na nyenzo za kutosha na vifaa vya kutosha vya kuhakikisha kwamba wanambana huyu mfanyabiashara ambaye anadanganya Taifa kwamba anawauzia kwa bei ndogo. Niomba tu Mheshimiwa Waziri aje na mikakati ya kuhakikisha kwamba basi upotevu wa fedha ambazo zinapatikana katika punguzo la wafanyabiashara wachache, basi linazingatiwa *TRA* wapewe zana za kutosha za kuhakikisha kwamba wanadhibiti udanganyifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize suala la kutoa kodi ya *VAT* katika mafuta. Mimi nashauri sana ile asilimia 10 ibaki pale pale.

**NAIBU SPIKA:** Mafuta gani Mama?

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mafuta ya kula. Asilimia 10 ya *VAT* nasisitiza iendelee kuwa pale ili tulinde soko la mafuta ya karanga, mafuta ya alizeti na mafuta ya pamba. Hilo naomba Mheshimiwa Waziri aweke alama hapo ili aje na mikakati mizuri sana ya kuhakikisha kwamba tunakusanya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Mheshimiwa Waziri aje na maelezo atakapomaliza. Tutakubaliana sheria hii ipite na Mheshimiwa Waziri amesema kwamba fedha hizi zitawekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Naomba sasa anieleze ana malengo gani baada ya kuzikusanya hizi fedha na kuziweka kwenye Mfuko huu Mkuu na utafanya kazi gani hasa. Maana yake fedha zote ambazo leo asubuhi tumepitisha tumeshapitisha, sasa anakwenda tena kuchukua fedha nyingine za mamlaka pamoja na vitu vingine atueleze malengo hasa ameweka kiasi gani atakusanya ili tuje tuone sasa amefanikiwa zoezi lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba baada ya kuzikusanya hizi fedha kuweka kwenye Mfuko wa Serikali, ameweka vipaumbele gani vya matumizi ya hizi fedha? Lazima tuendelee na mipango. Bahati nzuri na Wizara yake na Mipango anayo hapa. Sasa atueleze baada ya kuzipata hizo fedha ameweka vipaumbele gani kuhakikisha hizo fedha basi tunazitumia vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie tu, kwa masikitiko yangu makubwa namwelewa Mheshimiwa Waziri, anatii sana maagizo ya viongozi wake wa juu. Jana nilikuwa nachangia kwenye Wizara yake, bahati mbaya muda ukawa umekwisha kwenye kifungu sikuweza kupata nafasi, lakini ninavyomwelewa Mheshimiwa Waziri suala la kusamehe kodi kwa majengo kwa wazee ni muhimu sana katika nchi yetu. Kwa sababu ni agizo kwa Rais na Mheshimiwa Waziri jana wakati anazungumza hapa alisema kwamba yeye anatekeleza sana maagizo ya viongozi wake wa juu na akatoa mfano kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa agizo zikatengwa shilingi bilioni 10 na ametenga.

Je, Rais wetu tarehe 5 Oktoba, 2005 alivyotoa agizo lake kwamba Kodi za Majengo kwa wastaafu itolewe, hilo nalo amekuwa ananiambia kwamba akazungumze. Mnakwenda kuzungumza nini Mheshimiwa Waziri na Mawaziri wa TAMISEMI? Kwa

sababu kama ni Waziri wa TAMISEMI aliagiza Halmashauri za Mitaa na Miji kwamba tarehe 1 Februari, 2007 bahati nzuri sana aliyepewa agizo hilo sasa hivi ni Waziri wetu Mkuu, mabadiliko ninayo ya kusisitiza kwamba Halmashauri zifanye hivyo, litekelezwe agizo la Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jana nimesikia Waziri ananiambia kwamba anakwenda wakaliangalie agizo la Rais unakwenda kuliangalia. Kwa kuwa Waraka ulishatolewa kwa kuwa wazee sasa hivi wanamtegemea Waziri wa Fedha ndio atakayewanusuru. Nimwombe sana misamaha mingi sana imetoka hapa tunaona kigugumizi gani kwa wazee hawa ambao walitumikia nchi yao wako nchini kwao kubadilisha kipengele kidogo cha majengo tukawasaidia kwa sababu pensheni yenyewe ni kidogo sana wanacholipwa. Sasa na Rais ameona hilo ameagiza bado tunasema kwamba tukaliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu wake kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wameifanya, ingawa yapo mapungufu kidogo ambayo nitayapitia kwa haraka haraka. Lakini kwa leo mchango wangu ni mfupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati napitia Muswada huu, kuna mambo nimetarajia kuyakuta, lakini kwa bahati mbaya sikuweza kuyaona na atakumbuka kwamba Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha hotuba yake hapa Bungeni kuna mambo aligusia kwamba angeweza kuleta mapendekezo ya kurekebisha sheria mbalimbali na hasa Sheria za Mamlaka ya Udhibiti.

Katika mapendekezo hayo, tulitarajia kwamba angeleta mapendekezo ya fedha ambazo zinapatikana kama ziada *surplus* ziweze kupelekwa kwenye Mfuko Maalum wa Serikali, lakini kwa bahati mbaya sikuweza kuiona katika Muswada huu. Mapendekezo hayo nilivyotegemea yalilenga kurekebisha vifungu mbalimbali vikiwemo *section 43* ya *TCAA*, *Section* 50 ya *TCRA*, *Section* 42 ya *SUMATRA* na *Section* 44 ya *EWURA* na kadhalika. Lakini sijui ni nini kimemtokea Mheshimiwa Waziri akashindwa kuleta marekebisho hayo. Mimi nadhani mapendekezo hayo kama yangekuwa ni mazuri tu, labda pengine baadaye watayafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati napitia Muswada huu, kuna vipengele fulani nimevitipia, ni hasa *section* ya 6, 8, 27, 36, 42, 44 na vingine. Hizi zinahusiana na mamlaka ya Waziri wa Fedha katika sheria hii ambayo tunakusudia kuitunga katika mchakato mzima wa kutayarisha bajeti za Mamlaka za Udhibiti. Awali kabla ya mapendekezo kuja hapa, mchakato wa bajeti za mamlaka hizi ulikuwa unatayarishwa na mamlaka zenyewe halafu zinapelekwa kwa Waziri mwenye dhamana, halafu baada ya hapo, bajeti inapita. Kama Waziri mwenye dhamana pengine alikuwa hakuridhika, basi angeweza ku-*appoint auditors* wakaweza kuangalia huo mchakato.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mapendekezo yanayokuja hapa ni kwamba, mchakato wa bajeti nzima za mamlaka zetu hizi utakuwa unaanzia kwenye mamlaka husika baadaye unakwenda kwa Waziri mwenye dhamana. Waziri mwenye dhamana hana mamlaka yoyote kuhusiana na huo mchakato wa bajeti ambayo iko chini ya Wizara yake, utaishia kwa Waziri wa Fedha ambaye atatoa *approval*. Kwa maana hiyo, anaweza akakubali au hakakataa kutegemea na jinsi atakavyoiona, sijaona mwendelezo mwingine kwamba asipoikubali itakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamesema hapa kwamba ni kwa nini Waziri mwenye dhamana ambaye ameaminiwa na Rais na Serikali kwa ujumla ambaye anaongoza mamlaka ambaye iko chini yake kwa nini asipewe mamlaka ya ku-*approve* hiyo bajeti ya mamlaka ambaye iko chini yake. Lakini pia wote tunafahamu kwamba Mamlaka za Udhibiti zina wadau wakuu watatu, mmojawapo akiwa Serikali, mwingine akiwa ni mlaji, *consumers* na wa tatu akiwa ni *suppliers* msambazaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika Muswada huu, tunachotaka kukifanya tunataka kumfanya mdau mmoja ambaye ni Serikali awe na meno awe na nguvu dhidi ya wadau wengine wale wawili na nasema hii sio sahihi. Kwa sababu kama tutamwachia Waziri wa Fedha yeye ndio a-*approve* bajeti ya matumizi, kwa mfano ya *TICRA, EWURA* sasa hii mamlaka itashindwa kudhibiti Serikali, haitaweza kufanya kazi kwa uhuru. Mimi nilikuwa nasema kwamba sioni kwa nini tubadilishe sheria iliyokuwepo. Sheria iliyokuwepo ni nzuri sana na nadhani ni mfano mzuri sana wa kuigwa na wenzetu. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha anajua majukumu mengi asilimbikiziwe na majukumu mengine haya ambayo naamini sio ya msingi hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hivyo kwa sababu kwenye vifungu vingi nakuomba ninukuu kidogo kile kifungu kimoja kinasema kwamba: "*Upon approval of any annual or supplementary budget under section 49, the Minister shall cause the budget to be submitted to the Minister responsible for finance for approval.*" Maana yake ni kwamba Mheshimiwa ambaye labda Mawaziri wa Maji akishapokea bajeti ya *EWURA* itabidi aipeleke Wizara ya Fedha wakaipitishe. Sasa huyo Waziri wa Maji kazi yake ni nini?

Mheshimiwa Diallo amezungumza hapa, tusitake kutengeneza kwamba Wizara moja ni kubwa kuliko Wizara nyingine, zote ziko sawa na zote zimekuwa *established* kikatiba. Sasa iko siku tunaweza tukamwachia Waziri wa Fedha, sisemi Mheshimiwa Mustafa Mkulo, labda mwingine akaja akawa *dictator* atanyanyasa sana hivi vyombo na ikitokea kwamba pengine hizo Mamlaka za Udhibiti zitafanya kazi ambayo haimfurahishi, watakuwa na fimbo ya kuwachapia ambayo ni hii ku-*approve* bajeti yao. Lakini pia nao watakuwa wanafanya kazi kwa uwoga, hakuna uhuru ile *independence* ya mamlaka inaondolewa na kifungu hiki. Tuwaachie wakae kama walivyokuwa wanafanya zamani, hatutapata matatizo yoyote na nadhani kazi ya mamlaka itakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukiingia kwa undani naiona, kama *insubordination,* kwa nini Waziri mwingine awe na mamlaka ya kuamua kazi za Waziri

mwingine? Mimi nadhani kama Wizara imeundwa iko pale, tuiachie ifanye kazi na ninayo mapendekezo yafuatayo:-

Ya kwanza, katika mchakato wa bajeti za Mamlaka za Udhibiti nilikuwa napendekeza kwamba mchakato mzima wa bajeti uishie kwa Waziri mwenye dhamana na sio vinginevyo. Pia nilikuwa napendekeza kwamba kwenye Muswada huu vile vifungu ambavyo vinampa Mamlaka Waziri wa Fedha kutoa *final approval* ya bajeti za mamlaka napendekeza kwamba vifutwe viondoke ili sheria ikae vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nilitaka kusema kwamba kama haya yatafanyika ambayo ninazungumza hapa sasa hivi, mimi nakuhakikishia kwamba hata wawekezaji kutoka nje watavutiwa na sheria hii kwa sababu ni mwekezaji gani atakuja kushindana awekeze hapa nchini labda katika maji au shughuli nyingine ambayo anajua mdau mwenzake ana nguvu, ana rungu ya kuweza kumdhibiti, hakuna mwekezaji ambaye atakuja hapa. Mwisho nasema leo sina mengi ya kuzungumza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, lakini wazingatie haya ambayo nimeyasema kwa leo na nawaunga mkono. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Lekule Laizer na Mheshimiwa Mnyaa namwomba naye ajiandae.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie kwenye Muswada huu. Nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja. Pili, niipongeze sana Mamlaka ya Kodi ya Taifa *TRA* kwa kazi nzuri wanayofanya ambayo kusema kweli kwa kiwango kikubwa ndiyo inatuwezesha katika maana ya bajeti ya Serikali kufanya haya mambo makubwa kabisa ambayo wote tunayashuhudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi hiyo, kiongozi wa *TRA* Bwana Kitilya anastahili pongezi za makusudi kwa sababu yeye ndiye Msimamizi Mkuu, lazima ana dira fulani inayoifanya *TRA*, yeye kama kiongozi kwa hilo. Mimi ni Muikolojia, Mtafiti wa wanyamapori. Kwa hiyo, mchango wangu unajielekeza zaidi kwenye sehemu ya 10 na 11 inayozihusu Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* ambazo zinapendekezwa kufanyika marekebisho yatakayomwezesha Waziri wa Fedha kuweza kuchota fedha zinazotoka kwenye Mashirika hayo. Naelewa azma ya Serikali kwa kupendekeza hivyo ni kuongeza uwezo wa kukusanya mapato kwa ajili ya Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ningependa kutoa angalizo zifuatazo:- *TANAPA* na Mamlaka ya Ngorongoro ni Mashirika ya huduma. Tena ni huduma maalum na ni nyeti za uhifadhi kwa wanyamapori ambao wote tunakubali na tunafahamu faida yake. Kwa hiyo, haya sio mashirika ya biashara kama ambavyo sura inajionyesha kwenye Muswada ulio mbele yetu hapa. Hayafanyi biashara na wala kwenye malengo makuu ya Mashirika haya sio kufanya biashara. Inayoonekana kuwa biashara ni matokeo tu ya shughuli zinazoendelea ambazo mapato yanayopatikana yanasaidia katika

kuendeleza uhifadhi huo kwa sababu huko nyuma tunafahamu mashirika haya yalikuwa yanategemea ruzuku ya Serikali kuweza kujiendesha. Lakini tulipofungua milango husus an ya utalii yaweze kutoza kwa watu wanaokwenda kuangalia wanyama hao, ndio yakaweza kupata uwezo wa kifedha kiasi cha kutotegemea tena Serikali.

Kwa hiyo, fedha hizi inayokusanywa na hayo mashirika inalenga katika kuyawezesha kutimiza majukumu ambayo yamekabidhiwa na sisi Watanzania kuhakikisha kuwa wanyamapori wetu tulionao wanaweza kuhifadhiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhifadhi wa wanyamapori bado una changamoto nyingi na ngumu sana. Hebu tufikirie kwa upande wa Hifadhi za Taifa kuna hifadhi takriban 15 hivi, lakini leo hii uwezo wa *TANAPA* wa kuzihudumia hifadhi zote hizi unatokana na makusanyo yanayotoka sana sana kwenye hifadhi mbili tu ya Serengeti na ya Kilimanjaro ambazo zinakusanya karibu asilimia 75 ya mapato yote ya *TANAPA*. Kwa hiyo, fedha zinazobaki zinakuwa zinategemea uwezo wa *TANAPA* kutoka Serengeti na Kilimanjaro. Kwa hiyo, ni lazima tuwe waangalifu tunaposema tunaweza tukachukua fedha kutoka *TANAPA*. Ulinzi wa wanyamapori bado ni mgumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa katika utafiti ambao kwa kushirikiana na watafiti wengine, sisi tulifika mahali tukaulizana: Je, hifadhi hizi tunazoziendesha kwa sasa tumefaulu kwa kiwango gani? Tuligundua kuwa na tulitoa chapisho hilo, bado wanyama wanazidi kupungua hata kwenye maeneo yenye ulinzi wa hali ya juu. Swali linalokuja ni kwamba na tunajiuliza kwenye toleo lingine litakalotoka kwenye kitabu kinachozungumzia Serengeti kwamba nani alipie uhifadhi wa wanyamapori? Je, dhahabu, pamba na vyombo vingine ndiyo vitolewe viende kusimamia uhifadhi au wanyama wenyewe waweze kujihudumia wenyewe katika maana kwamba kinachozalishwa kutoka pale kupitia mamlaka hizi ili ziweze fedha hizo kutumika kwa ajili ya uhifadhi wa hao wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, marekebisho yanayopendekezwa yanaweza kuleta mgongano wa mamlaka ya usimamizi wa sekta. Waziri mhusika wa mashirika haya kwa vyovyote vile ana wajibu wa kutekeleza sera na mipango ya uhifadhi wa wanyamapori kupitia mashirika haya. Leo hii ukimwingiza Waziri wa Fedha awe ndiye mwamuzi wa mwisho kwenye bajeti ya mashirika haya, itakuwa sio sawa. Ikumbukwe kuwa Waziri wa Sekta hii amekasimu mamlaka yake kwenye Bodi zinazohusika ndizo zinazoangalia mpaka hatua ya mwisho ya bajeti za mashirika haya, amekasimu yale madaraka. Kwa hiyo, Bodi ndiyo inakuwa ya mwisho katika kuidhinisha bajeti za uendeshaji ya Mashirika hayom yaani Uhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukimwingiza Waziri mwingine, maana yake ni kwamba Bodi inafanya mapitio ya bajeti, inawasilisha kwa Waziri wa Sekta, lakini Waziri wa Sekta anapeleka kwa Waziri wa Fedha. Huu ni mlolongo usio na sababu yoyote na utaongeza gharama isiyo na maana yoyote. Sio vizuri kutengeneza mazingira ambayo kunaweza kukawa na mashindano ya Mamlaka Waziri na Mawaziri wanashindana kwa sababu kuna mwenye Sera, Waziri wa Maliasili kwa kesi ninayoizungumza na Waziri wa Fedha katika maana ya fedha atakayeangaliwa ni nani

mwisho wa siku? Ni Waziri anayesimamia sera na sekta husika, lakini alinyang'anywa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani Waziri wa Sekta kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina, angeachiwa mamlaka ya kuangalia ni namna gani mashirika haya yanaweza yakachangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia kodi ya mashirika kwa Kiingereza *Corporate Tax*. Nafahamu na Waheshimiwa Wabunge wengine wamekwishasema kwamba mashirika haya yanalipa kodi za mashirika. Kama hayalipi, basi tuseme tutafute mwanya wa namna ya kuyawezesha yalipe. Lakini nafahamu yanalipa na huu ndio utaratibu mzuri wa kuhakikisha kuwa mambo yote yanaendeshwa kwa mujibu wa mamlaka zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe vile vile kuwa uhifadhi kwa wanyamapori una sura mbili au tatu hivi. Moja, usimamizi wa wanyamapori, yaani kuwalinda ni gharama kubwa kama nilivyosema. Yapo machapisho ambayo hata mimi nimeshiriki kuyachapisha baada ya kufanya tathmini ya gharama ya uhifadhi huo na kuna nguvu nyingi sana zinatumika katika kuhakikisha kuwa wanyama hao wanalindwa na wote tunawafurahia na watu wengine wanafurahi kutokana na uwepo wa wanyama hao kupitia sekta ya utalii.

Mimi nafahamu vile vile kuwa, pamoja na *TANAPA* na Ngorongoro kuonekana kuwa wanakusanya fedha nyingi sana, lakini nafahamu wanasaidiwa na mashirika mbalimbali kuhakikisha kuwa usimamizi huo wa wanyamapori wana uwezo kwa kiwango hiki tunachokiona. Wote tunafahamu kuna taasisi moja inaitwa kwa Kiingereza *Frankfurt Zological Society*. Hii leo ukiiambia *Franfurt* iondoe misaada yake hapa, fedha hii inayozalishwa na *TANAPA* haitoshi kabisa kuziba pengo ambalo *Frankfurt Zoological Society* wanatoa msaada kwa *TANAPA*, lakini pia wanatoa msaada kwa Ngorongoro.

Sura nyingine ya ulipaji wa wanyamapori ni utafiti kwamba ni lazima tufanye utafiti kuhakikisha kuwa wanyama hawa wanalindwa, wanasimamiwa kwa njia za kisayansi ili waweze kuendelea kuwepo. Bado sasa hivi ndiyo tunafikiria tuweke kwenye sheria kuwa mamlaka hizi zichangie kwa mujibu wa sheria kwenye mifuko ya utafiti wa wanyamapori utakaosimamiwa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania kwa kifupi *TAWIRI* ili kusaidia tuweze kuwa na uhakika wa kuwahifadhi hawa wanyama. Lakini pia mimi nafahamu na wote tunafahamu mashirika hata yanajishughulisha vilevile kwenye kuchangia kwenye kuchangia kwenye maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri tuwe waangilifu kuhakikisha kuwa hatuvurugi utaratibu mzuri ulipo na pale ambapo tunaona kwamba pengine tunaweza tukaongeza, basi tufanye hivyo kama nilivyosema, tuangalie kama kweli mashirika haya hayalipi kodi ya mashirika vya kutosha, yalipe. Mfumo huu upo ndani ya mamlaka ya Waziri husika ili kusudi tuzipate hizo pesa ambazo tunazihitaji na mimi nimekuwa nasema mara nyingi sana kwamba tukijipanga vizuri, *TANAPA* na Ngorongoro ni kati ya vyombo ambavyo ni vya nguvu sana kiuchumi na lazima tuseme hivyo.

Kwa mfano, tukiwekeza kwenye miundombinu ya kuingia kwenye hizo hifadhi utalii, utapanuka kwa kiwango kikubwa sana na kwa hiyo, pesa nyingi zitapatikana kupitia kwenye utalii ambao hausimamiwi na kuendeshwa na mashirika haya, bali mashirika haya yanatengeneza mazingira ya kuwezesha watu wengine waingie ili kusudi wafanye biashara na walipe kodi stahili ili kusudi Serikali iweze kupata mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuyape fursa mashirika haya pengine kama kweli tutanata kuyatoza katika mtazamo huo unaopendekezwa hapa, yawekeze kwenye biashara na tuyatoze kwa mtazamo huo kwa mujibu wa mapendekezo yanavyowekwa hivi kwenye miradi ile iliyowekezwa, sio kwenye majukumu ya msingi ya uhifadhi wa wanyamapori. Vinginevyo tutakuwa tunatengeneza kaburi la kuzika uhifadhi nchini na baada ya muda tujikute tumefeli kwenye suala hili ambalo siku chache kabla ya uhuru Mwalimu alisisitiza umuhimu wa kuwahifadhi wanyama na utajiri mkubwa huu tulionao wa asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, mimi nilidhani hivi vifungu vilivyoko kwenye sura ya 10 na 11 kwa sasa hata vingefutwa, hakuna ubaya. Lakini kama ni lazima, basi viendelee kuwepo katika maana ya tahadhari ya huko mbele, virekebishwe, ili Waziri wa Fedha asiwe na mamlaka ya mwisho kwa sababu nimesema hata Waziri mwenyewe amekasimu mamlaka kwenye Bodi kuidhinisha Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu na ningependa na mimi kama hawa wenzangu walivyosema kuipongeza sana *TRA*. Kwa ajili ya makusanyo mazuri wanayokusanya na ndiyo maana Serikali na nchi nzima inaendeshwa kwa ajili ya kazi yao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa kusema machache kama wenzangu walivyochangia kwamba kuna maeneo ambayo yanafaa kabisa yatazamwe na nianze na kodi ya simu. *Airtime*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia, kodi ya simu kwa kweli ni kubwa mno na siku hizi kila mtu ana simu hata vijijini. Ukiwakuta wachungaji wanaochunga mifugo kule porini, wote wana simu. Nikitaka kuwasiliana na nyumbani hata mchungaji aliyepo machungani nampigia simu, lakini bahati mbaya hii simu siku hizi itakujakuwa haitumiwi na watu wote. Kuna watu wenye simu, lakini anabeba tu apigiwe simu au a-*beep*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wenzangu ni mashahidi, wapigakura wetu kule ni wachache sana wanaokupigia simu. Anaku-*beep* tu umpigie. Wote ndivyo mlivyo. Kwa hiyo, mmeweka bajeti ya kuwapigia wapigakura wenu kwa sababu wao hawawezi kupiga kwa ajili ya gharama. Sasa mtandao huu ambao umeenea kila mahali tufaidike

wote. Hii kodi ipunguzwe ili kila mtu aweze kuwa na mawasiliano. Kama Serikali imeweka kodi kubwa, ni afadhali Serikali ipunguze hii kodi kwa ajili ya manufaa ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho kitakuja kushindikana na ni kizuri mno ni umeme. Huu umeme ambao tunasema kwamba utapelekwa kila kijiji, Mheshimiwa Rais alipohutubia Bunge alisema mpaka mwakani itakuwa ni Halmashauri moja tu ambayo itakuwa haina umeme nayo ni Nkasi. Lakini inawezekana umeme huo ukafika vijijini, ukashindikana kutumika kwa ajili ya gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la kodi ya madini. Sijui kwa sababu tumetawaliwa na Wazungu tukawa tunawaogopa mpaka sasa! Mpaka sasa tunawaogopa! Mpaka sasa tunawaogopa Wazungu hata kuwalipisha kodi tunawaogopa!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mzungu akija akitaka ku-*invest* kwenye madini anapunguziwa kwa muda wa miaka kadhaa. Kila mwaka yupo katika majaribio na hao nataka tu nitoe mfano, kwenye *Tanzanite One* wanalipa mrahaba bilioni moja na nusu kwa mwaka ndiyo wamelipa.

Twende kwa wachimbaji wadogo wadogo, hawa wachimbaji wadogo wadogo kwanza fedha zao zote wana-*invest* hapa hapa, hakuna anayehamisha fedha zake. Wamejenga hoteli nyingi sana Arusha, wamejenga majengo mengi sana ambayo hayo majengo bado tunawalipisha kodi. Wanalipa kodi ya uchimbaji, wanalipa ya majengo na magari wamenunua mengi na hayo magari bado wanalipia kodi na ajira wametoa nyingi tu. *Tanzanite One* hawajajenga hata kibanda, wanapanga hotelini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi biashara inayoendeshwa na wachimbaji wadogo wadogo ambayo Serikali inakusanya kodi si inazidi hiyo bilioni moja na nusu waliyolipa *Tanzanite one* ambao hawana hata jengo moja? Kwa hiyo, tuwaangalie wachimbaji wadogo wadogo tuwaenzi, ndiyo tutapata kodi. Lingine hawa *Tanzanite One* ndiyo wanapewa eneo kubwa, kwanza ni dhambi kubwa mno tukiwapa maeneo wachimbaji hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo kila siku nalizungumzia, Mheshimiwa Mungai alipochangia alizungumzia chai na magogo. Kuna jambo ambalo kila siku nalizungumza. Mimi natokea kwenye Wilaya ya mpakani. Kila siku naomba mtuwekee utaratibu wa mifugo tuweze kupeleka Kenya kwa magari. Kila siku! Sijui hamniskii! Sijui mnafanya nini! Au hamtaki? Mnataka tu tupite njia za panya twende Kenya! Lakini humu ndani Tanzania kuna utaratibu wa mifugo kusafirishwa kwa magari.

Sasa kwanini msituwekee utaratibu na sisi wa kupeleka mifugo kwa magari Kenya kuliko kuswaga kwa miguu ili na ninyi mdai kodi? Hatujakataa kulipa kodi, sasa tutamlipa nani kama hamtuwekei utaratibu? Ukipitisha ng’ombe kwa magari wanateremshwa, wanasema hakuna utaratibu. Mnawalipisha nini nao hawakuwekewa utaratibu? Mimi nahitaji sasa mtuwekee utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni masoko ya mtaji. Jamani, hii ni biashara kubwa na ni biashara nzuri ambayo haina mahangaiko. Lakini Watanzania hawajui. Ni watu kama akina Mungai wafanyabiashara wakubwa ndiyo wanajua. Lakini hata sisi wafugaji tunaweza tukafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiuza ng'ombe 20 napeleka kununua hisa tena, ni biashara nzuri kuliko hawa ng'ombe ninaowaswaga kila siku kwa sababu fedha zinaongezeka, sio kuchunga, si kutafuta maji na ni biashara nzuri sana kuliko kuchunga mifugo. Lakini wafugaji hawajui.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka elimu hii iende sasa kwa wafugaji. Kama mnataka tupunguze mifugo kwa njia ya kununua hisa na kuwekeza. Mimi nikiuza mifugo, madume 20 nanunua hisa, mwakani nauza hisa zangu napata fedha nyingi kuliko. Lakini hamsemi mnataka kung'ang'ania na kufanya biashara wachache. Kwa wale walioelimika tungejua hizi hisa za *NMB*, nadhani wafugaji wangeuza mifugo na kununua kwa sababu wao wana pesa. Kwa hiyo, nataka elimu hiyo ifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni fedha za *TANAPA* na Ngorongoro wenzangu wamezungumzia. Ndugu zangu, mimi naomba tuache fedha za Mamlaka ya Ngorongoro na *TANAPA*. Wanafanya kazi kubwa sana ambayo ingekuwa ni Serikali ndiyo inafanya isingeweza na tusingekuwa na wanyama. Wanyama wangeisha, lakini wao ndiyo wanalinda wanyama, utalii wao ndio wanatangaza na hata jamii inapata misaada mingi sana kutoka kwa mamlaka hizi. Pamoja na shule, kuna ile shule ya Mweka, pale ni Ngorongoro na *TANAPA*, Pansiasi wao ndiyo wanasaidia. Hakuna fedha ya Serikali inayoingia kule. Wao ndiyo wanaendesha hizo shule. Kwa hiyo, naomba na hilo litazamwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni mgao wa hizi fedha za Serikali. Hizi fedha za Serikali tunalalamikia kuanzia mnapogawa kwenye Wizara, kuna Wizara wanapata fedha haraka sana na kuna Wizara ambazo hawapati fedha. Hiyo Wizara isipopata fedha jua kwamba wananchi wameumia, kwa sababu kuna wananchi wanategemea miradi kutoka kwenye Wizara hizo. Sasa kama mkiweka upendeleo huko, kwa hiyo, mnaanza upendeleo huko, halafu mnakuja tena upendeleo kwenye Halmashauri.

Mimi kwa kweli sitamwogopa mtu yeyote nikiona kwamba Halmashauri yangu inanyanyaswa huku Halmashauri nyingine zinaendelea wanapewa fedha na wote tunategemea chungu kimoja. Nitapiga kelele hapa, hata mkinifukuza Bungeni mnifukuze lakini nitapiga kelele, nitasema. Kuna upendeleo mkubwa sana. Kuna Halmashauri nyingine wana magari mengi, wengine hawana magari. Nitoe mfano wa fedha za JK, hizi fedha tayari awamu ya kwanza na hii awamu ya pili.

Mheshimiwa Waziri alipotangaza fedha zilizotolewa, Wilaya yangu wameshangaa sana pamoja na Simanjiro. Mnaingia sasa awamu ya tatu mnakwenda shilingi bilioni 50, sisi hatukupata hata senti wala hauonekani utaratibu wa kupata. Wananchi wangu

wameshakasirika na hata hizo *SACCOS* wameanza kuvuruga, wamesema hata hizo fedha hatupati. Wanasema ni fedha za utapeli na lengo sio hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni upendeleo mkubwa sana kwa sababu wengine wanapewa awamu ya pili sisi hata hiyo awamu ya kwanza hatukupewa mpaka leo hii. Mtuambie leo kwamba Halmashauri ya Longido, Simanjiro na Halmashauri nyingine ambazo hazikupata kwamba hatukuwepo kwenye mgao huo na nataka jibu kwa sababu wananchi wananisubiri na sijui niende kuwaambia nini.

Nataka leo nipate jibu nikawaambie kwamba wasihangaike kwa sababu *SACCOS* za Longido hazipo. Nasikia sijui fedha zimepitishwa wapi! Kama fedha za Longido nimeona kwenye majedwali mmpeleka kwenye *Commercial Bank* na wao wamekwenda kufanyia biashara. Hivi *Commercial Bank* ni Longido? Kwa hiyo, naomba jibu mtuambie kama sisi hatumo.

Nheshimiwa Naibu Spika, tukitoka hapa, wananchi wanatusubiri tuulizwe maswali kuhusu umeme, maji, shule na tuulizwe fedha za *SACCOS.* Wananchi wanatusubiri wajue Serikali inafanya nini? Fedha zilizopitishwa kwenye Bunge hili ziende kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni ucheleweshaji wa fedha za miradi zilizopitishwa kwenye Halmashauri. Halmashauri inapitisha fedha mpaka Bajeti nyingine unakuta fedha za barabara au za maji hazikufika, halafu huku mnasema kwamba fedha zimerudi. Zimerudi kwa sababu gani na huku kuna Halmashauri ambazo wanasubiri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mnavyojadili inakuwa kama mnajadili Bajeti. Sasa hapa tunajaribu kumwezesha Waziri wa Fedha aweze kupata fedha ili afanye kazi ya kufanya hiyo miradi na vitu kama hivyo. Maana mnajadili ile hotuba ya jana ya Waziri wa Fedha, ile ndiyo maneno mnayosema ya namna hii. Hapa tunazungumzia namna ya kupata fedha za kufanya yale tuliyoyasema kipindi chote, sasa mkijadili kwamba mtambana, wengine mtatoa shilingi, hakuna shilingi hapa. Kama hamkutoa shilingi kule, hapa leo haipo.

Kwa hiyo, naomba mjielekeze kwenye utaratibu wa namna Serikali inaweza kuongeza mapato yake na sio kupunguza mapato yake. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Mohammed Mnyaa, halafu atafuata Mheshimiwa Prof. Mwalyosi.

**MHE. MOHAMMED HABIB MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi ya kutoa mchango wangu kwa kifupi leo jioni.

Napenda na mimi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ya Fedha pamoja na wasaidizi wake na upande mwingine nawapa pole kwa kazi ngumu waliyonayo na wavumilie kwa maneno yetu, lakini hiyo ndiyo hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wachangiaji wenzangu ambao sikusudii kuwajibu hata kidogo, lakini waliposema kwamba Wazira zote ni sawasawa, kisheria nakubaliana nao kwa upande mmoja, lakini *seniorities* za Wizara zipo na Wizara hii ni moja kati ya Wizara *senior* ambayo Wizara nyingi sana zinategemea Wizara hii. Kwa hiyo, kazi ngumu wanayo Wizara hii. Nakusudia kuchangia na pengine mimi leo niunge mkono hoja kwa mara ya kwanza ikiwa yatatekelezwa yale nitakayoyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze na hili suala la simu na kama ulivyotoa maelezo kwamba hoja iliyopo ni namna ya kupata fedha, sio kupunguza. Lakini Serikali imeweza kutueleza kwamba Makampuni haya ya simu yanalipa takribani shilingi bilioni 449.6 na kwa maana hiyo ni walipakodi wazuri.

Sasa basi katika huu ushuru wa bidhaa na huduma ambao umeongezwa au unakusudiwa kuongezwa kutoka asilimia saba mpaka kumi na mimi nasema ni mkubwa na hivyo kodi wanayolipa hayo makampuni itashuka na itashuka kwa sababu watumiaji wa hizo simu ambao ni wananchi ambao wengi wao ni wanyonge hawatamudu kama Mheshimiwa Laizer alivyosema. Kwa hiyo, mimi ningeshauri ibakie ile ile asilimia saba na isiongezwe mpaka asilimia kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa unatafuta fedha sehemu nyingine ili kufidia ile sehemu ambayo usiongeze kutoka asilimia saba mpaka kumi, ziko sehemu chungu nzima za kupata fedha nyingine na kipengele hiki kikabakia hivi hivi.

Kwa mfano, sote tunajua kwamba fedha inayoletwa kwa mambo ya Ukimwi na Semina zinazofanyika ambazo haziwafikii walengwa. Kuna Semina nyingi zinazofanyika, posho zinazotolewa kwenye hizo semina Sheria zinaweza zikakatwa kodi. Posho za Wabunge zinaweza zikakatwa kodi, semina ziko nyingi Mawizarani ambako zinaweza zikakatwa kodi huko, lakini simu isiongezwe. Hiyo ni mipango mingine ya kupata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni misamaha ya kodi na hapa nakusudia misamaha ya kodi ya mafuta hasa kwa makampuni haya yanayokuja kuwekeza kwenye madini. Ni ukweli usiopingika kwamba wana misamaha mingi ya kodi ikiwemo hii kodi ya mafuta ya kuendeshea mitambo na majenereta.

Lakini vilevile inafahamika sasa hivi kwamba makampuni haya kabla hayajachimba, madini tayari yanapata faida kwa biashara ya mafuta. Kuna biashara ya mafuta inayofanyika na imepelekea baadhi ya sehemu huko kanda ya ziwa, mafuta ya petroli na dizeli ni rahisi kuliko Dar es Salaam. Yaani madhumuni yao ya kutafuta madini, basi kwa upande mwingine wanabiashara ya mafuta, sio siri inafahamika. Kwa hiyo, misamaha ya kodi hii ni ya kuondolewa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo nataka kuzungumzia linatokana na utozwaji kodi mkubwa mara nyingi sana. Waheshimiwa Mawaziri wakitoa mifano ya hizi kodi wanatoa mifano ya nchi mbalimbali na hata sisi Wabunge tunapenda kutoa

mifano ya nchi mbalimbali. Lakini mifano ile tunayoitoa ilingane na hali halisi ya eneo linalotuhusu sisi. Kwa mfano katika hii kodi ya *income tax* ya asilimia 30, halafu kuna *VAT* ya asilimia 20. Kuna ushuru wa Bandari, kuna ushuru wa *stamp* na ushuru wa bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii kampuni ukiiangalia pamoja na kwamba sisi Wabunge tunapendelea Serikali iwe inapata mapato mengi, lakini vilevile mapato haya yaendane na ile huduma kwa maana kwamba wakati tunaisifu *TRA* kwa kukusanya shilingi bilioni 300, basi napo tutoe ulinganisho: Je, Kenya wanakusanya shilingi bilioni ngapi au Uganda wanakusanya shilingi bilioni ngapi? Ni kweli wanafanya kazi nzuri tuwapongeze lakini tulinganishe kama tunavyolinganisha mambo mengine na wakati sisi tunatoza *VAT* asilimia 20: Je, hawa wenzetu wanatoza shilingi ngapi?

Sasa ukija unasema unaongeza kwa mfano kama ile ya simu ya asilimia saba mpaka kumi ukasema, mfano kama aliousema Mheshimiwa Waziri kwamba na Kenya wanatoa hiyo hiyo na Uganda hiyo hiyo. Je, kipato cha Wakenya kinalingana na kipato cha kwetu au kipato cha Uganda kinalingana na kipato chetu? Kwa hiyo, kuna misingi ya kuangalia, sio suala la Kenya wanafanya hivi na sisi tufanye hivi. Tuwe tunalinganisha kwa mantiki ya hali halisi ya uchumi wetu na hali halisi ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi kodi za *income tax*, *VAT* na nini utaona kampuni *at the end of the day* asilimia 50 ya faida yake inatoka pamoja na hizo ushuru nyingine. Sasa yeye ikiwa ametengeneza shilingi milioni 10 faida, shilingi milioni tano itoke, sasa kidogo hapo ni lazima tuangalie na iko haja haya makampuni pamoja na kwamba tunataka makusanyo, lakini tuyape unafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utozaji wa kodi labda niseme na ninukuu mifano mingine ya duniani, kwamba, wale walipaji kodi wakubwa huwa wanathaminiwa sana, huwa wanapongezwa, wanaheshimiwa kwa sababu ni walipakodi wazuri.

Leo Wizara ya Fedha au *TRA* mimi sijasikia, wala sijaona kitendo cha kufanya angalau katika kila mwaka kukawa na *insentive* fulani ya wale walipakodi wakubwa kama motisha huwazawadia kama ni *certificate* au kitu chochote kwa kuwapa moyo wa kulipa zaidi ili uwafanye na wengine wajitahidi walipe kodi zaidi. Sijaona kitu kama hicho! Duniani yanatendeka, walipakodi wakubwa ni watu ambao wanaoheshimiwa na wanathaminiwa sana. Hapa kwetu kwanini hakuna?

Kwa hiyo, ninaomba Waziri wa Fedha alichukue hilo ili kuwapa motisha walipakodi wakubwa. Kiwepo kitendo cha kuwathamini na wao wajue kwamba nimethaminiwa. Ikiwa leo mtu anakwenda kwenye mashindano fulani anapewa kombe au nishani na zawadi nyingine, leo mlipa kodi mkubwa ambaye anatusaidia kwanini usimthamini au kumzawadia? Ni kitu ambacho kifikiriwe na kifanyike kwa sababu kitasaidia watu wengi kulipa kodi.

Kadri utakapoweka kiwango cha kodi kikubwa, basi kwa vyovyote vile ukwepaji wa kulipa kodi utakuwepo kulikoni kuweka kodi ambayo kwa wastani mtu atatamani

kulipa kodi. Kwa hiyo, ni *practise* kote dunia nzima, ukiwa unaweka kiwango cha kodi kikubwa, watu watakwepa tu kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili suala la mamlaka mbalimbali ambalo wachangiaji wengi wamelizungumza kwa hamasa kubwa na ni kweli lina utata.

Katika Muswada huu majukumu mawili makubwa aliyopewa ni mazito na mimi naungana na Mheshimiwa Blandes na wengine kwamba ile kuidhinisha na kuzikubali bajeti za mamlaka mbalimbali hili lisiwe katika dhamana ya Mheshimiwa Waziri wa wa Fedha. Waziri wa Sekta anatosha, iwe kama zamani.

Lakini kinyume chake lile la pili suala la kumpa uwezo wa kuamua kiwango gani cha fedha anaweza kuchota katika mamlaka hizo, lifanyiwe utaratibu mwingine. Lakini haya makampuni ni kweli wakati mwingine wana *access* na Serikali, inahitaji hizi fedha na wao pengine wamezikalia tu, matokeo yake wanalipana safari kubwa kubwa. Hili haliwezi kuvumilika na Waziri wa Fedha lazima aingilie kati.

Kwa hiyo, Waziri wa Fedha ni kweli lazima awe na jicho la ku-*monitor* hizo mamlaka nyingine ili pale kwenye *access* na wakati Serikalini tunahitaji tuweze kuzipata fedha zile. Lakini lifanywe katika uangalizi mkubwa pasije pakawa na mgongano na kimaslahi bayana ya Waziri yule wa Sekta ile na Waziri wa Fedha. Hilo ni ukweli lizingatiwe na lifanyiwe juhudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba kuwasilisha maelezo yangu ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Kuunga mkono ulisema hivyo. *(Kicheko)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nami nianze kwa kujieleza ni nani kuhusiana na nitakayochangia ili niondoe *conflict of interest*. Kweli nipo kwenye Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, lakini vile vile huwa napenda kujiita mimi ni Mwanamazingira. Hicho ni kifupi, mimi weledi wangu *(profession)* yangu ni *Conservation Biologist*. Kwa hiyo, *Conservation that is my profession*. Kwa hiyo, nitapenda nitumie muda mwingi zaidi nizungumzie juu ya kile kipengele cha 10 na 11, nadhani ni Mashirika au Mamlaka za Ngorongoro na Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kama alivyosema ndugu yangu Ndugai asubuhi, Mashirika haya yana kazi moja kubwa *(the biggest)* ni uhifadhi *(conservation)*, ndio kazi zao. Nchi nyingi kama alivyosema, hasa zilizoendelea,

wanayapa fedha mashirika yanayofanya uhifadhi. Kwa hiyo, Hazina inatoa fedha badala ya kuchota kutoka kwenye mashirika hayo kwa sababu shughuli za *conservation* hazizalishi. Ukishazungumza kwamba ni Mradi wa *Conservation*, mara nyingi hata kodi huwa zinaondolewa kwa sababu hazizalishi. Kwa hiyo, hatungetegemea mtu aanze kufikiria kuchota fedha kwenye sekta za *conservation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mashaka kwamba, nijuavyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha siyo Mhifadhi, yeye ni mtu wa kukusanya pesa. Kwa hiyo, mambo ya uhifadhi yeye yuko mbali sana na anaweza asiwe na uchungu nayo. Kwa hiyo, lengo lake ni kukusanya fedha, siyo kuhifadhi. Tumeona hapa nchini, mgongano kati ya uhifadhi na *development*. Kila inapotokea kuna mgongano kati ya uhifadhi na *development*, c*onservation* inakandamizwa. Mifano mizuri, mradi wa kujenga hoteli kwenye *realm* ya Ngorongoro imeleta matatizo mengi sana, licha ya kwamba vigezo vyote vya EIA vilikuwa vinasema hapa, lakini tumepata shida, baadaye kwa kudra za Mwenyezi Mungu, *Conservation* ime-*win*.

Sasa hivi tunazungumza kuhusu Ziwa Natron, licha ya makelele ya watu wa uhifadhi, wanasema jamani pale kuna haja ya kupahifadhi, kuna rasilimali na viumbe ambao tunaweza kuwatumia kwa utalii tukapata hela nyingi *on a sustainable basis* kwa miaka mingi ijayo, hatutaweza kuimaliza. Wenzetu wameng’ang’ana hapa, lazima mradi ule ujengwe, *forget about conservation issue*, tutajenga tu. Kwa hiyo, hiyo najaribu kuonyesha jinsi mgongano kati ya *conservation* na *development* ulivyo, *always conservation* ina-*fail*, inapigiliwa msumari, hiki ndiyo ninachokiona hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii ikikubalika, ina hasara kubwa kuliko faida. Moja, sisi kwenye Kamati yetu ya Maliasili na Utalii tumekuwa tunawabana Waziri, Naibu Waziri na Watendaji kwamba, muongeze shughuli zenu kuongeza mapato ili msadie kuchangia kwenye maendeleo ya hifadhi nyingine, muwe wabunifu. Hawa watakatishwa tamaa sasa kwamba, kama sisi tunafanya kazi, tunakuwa wabunifu kwa ajili ya kuchangia tena kule ambako sisi tulikuwa tunajinusuru kwa ajili ya *conservation*, hawataweza kuzalisha, itapunguza mapato ya Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Ngorongoro. Matokeo yake, kwa upande wa Hifadhi za Taifa kwa mfano, kama alivyosema Mheshimiwa Ndugai, Hifadhi zinazozalisha na kutoa *excess* sana ni Kilimanjaro, Serengeti, Manyara, Arusha kidogo na Tarangire. Hifadhi nyingine kumi zilizobaki hazizalishi. Kwa hiyo, maendeleo ya Hifadhi hizo yanategemea hii *excess* inayopatikana kwenye hifadhi hizi tano.

Sisi tumesema hizi Hifadhi zimefikia mwisho, yaani ukiendelea kuongeza utalii pale, unaziua. Tu-*open-up* maeneo ya Kusini mpaka kwenye Milima ya Livingstone tuweke hifadhi, tuvutie utalii ili tukuache huku juu kupumue kidogo. Tumewaambia hawa Hifadhi za Taifa wawe ndio *Pioneers,* kuwekeza kwenye miundombinu ya kwenda kwenye Hifadhi za Kusini ili wawekezaji binafsi nao waone, halafu wa-*take over*. Kwa utaratibu huu, ina maana mazalisho yatakuwa kidogo, hela hazitatosha kuendesha hifadhi zilizobaki na hizo mpya tunazozitarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Ruaha ambayo tunataka iwe *the Biggest in Africa*, pengine *in the World* haina fedha na ndio inaanza. Tunategemea hizi Hifadhi

nyingine za Kaskazini zizalishe pesa kwa ajili ya Hifadhi hiyo.  Sasa leo hicho kidogo kinachozalishwa kwa ajili ya Hifadhi hiyo, mnataka mkiondoe kiingie *Treasury*, mtaua hizo hifadhi hazitaendelea.

Kibaya zaidi ni kwamba, zile Hifadhi za Kusini hazitaendelea milele, zitabakia hivyo hivyo.  Utalii utabaki Kaskazini na *eventually* zile Hifadhi zita-*collapse*, zitakufa kwa sababu zitakuwa *over utilized*. Kwa hiyo, *at the end of the day*, Hifadhi za Kaskazini hazitapata fedha kutokana na utalii na Hifadhi za Kusini zitakuwa *un-developed*, hakuna *resources* za utalii, kwa hiyo, utalii hapa nchini uta-*collapse*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri atueleze, ndio anataka kutufikisha huko? Sisi wengine tunasema hapana, huo siyo utaratibu mzuri, tuziache Hifadhi hizi kama tulivyopanga mwanzo, ziendelee kuzalisha.  *Excess* inayopatikana, tu-*develop* Hifadhi zilizobaki ili kusambaza utalii maeneo mengine ya nchi hii kwa kutumia *resources* hizo zilizozalishwa kwenye Hifadhi za Kaskazini. Kwa namna hiyo, mtatusaidia watu wa Kusini. Kwangu hapa ni ushindani kati ya Kaskazini na Kusini, hamtaki sisi Kusini utalii uendelee, ndivyo mnavyotaka kufanya kwa kunyang'anya fedha ambazo tungepata kuendeleza kule Kusini, mnataka kuzichota na sisi hatuwezi kukubali hilo!  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, sikubaliani na hoja ya kuchota fedha kwenye mamlaka hizi mbili na nipo tayari kupambana mpaka hiyo itakaposhindikana. Kama inabidi mnalazimisha, basi tufanye *Environmental Impact Assessment* ya Muswada huo.  Tufanye *Cost Benefit Analysis* ili tuone *cost* ni kubwa kuliko faida *or vise versa*. Tulikubaliana hapa kwamba, kuna kitu kinaitwa *Regulatory Impact Assessment*, basi tutumie hiyo basi kama namna ya kuweza kuangalia hii inafaa au haifai.  Nataka niwahakikishie vyovyote mtakavyofanya itasema hapana.  Kwa hiyo, huo ndio msimamo wangu na hii itafanya pengine na Muswada mzima nisikubaliane nao, kwa sababu ya hicho kitu kidogo tu.  Hilo mkiliondoa, mimi sina matatizo na hayo mengine.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa kidogo kwa kumalizia, mafuta yale walikuwa wanaita Moto Poa, kiujanja ujanja sasa wameamua wasiite hivyo.  Moto Poa ile bado ipo pale pale. Tunaondoa kodi kwenye mafuta wakati lengo letu ni kuongeza mapato ya Serikali.  Ninyi mnatoa kodi kwenye Moto Poa; asiwadanganye mtu, ili upike maharage, utahitaji debe zima la mafuta yele!  Kwa hiyo, *it is just as expensive as* kutumia lita moja ya mafuta ya taa.  Kwa hiyo, humsaidii mtu yeyote hapa nchini, *you are not saving the environment at all*.  Mnamsaidia mwenye mradi huo; mnataka kumpa hizo pesa mwenye kiwanda hicho.  Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mporogomyi, nilimsikia hapa kwamba, tunawatengenezea watu fulani mazingira ya kujipatia faida na kutajirika hapa nchini halafu sisi tunabaki hohehahe!  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *this is one case*, ni mradi mmojawapo ambao una lengo la kumpa manufaa mwekezaji na si ajabu huyu siyo Mtanzania, ajitengenezee fedha za bure tu zimekaa nje nje halafu sisi tuumie.  Siyo utaratibu, siyo haki na siyo kitu cha kuwatendea Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naomba nirudie, nitapenda suala la Mamlaka ya Ngorongoro na Hifadhi za Taifa ziachwe. Kama mnalazimisha, tufanye *Cost Benefit Analysis*, tuiache kwanza, *let us do Cost Benefit Analysis* na mimi nihusishwe kwa sababu ni Mhifadhi, nijue *aspects* za uhifadhi za kuingiza kwenye *components* hizo za ku-*compare*. Moto Poa ilishapita, walijitetea watu wa Mazingira lakini maelezo yangu ndiyo hayo, siyo kitu chenye tija hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. HERBERT J. MNTANGI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango wangu katika Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2008.

Wakati nilipokuwa nikichangia katika Hotuba ya Bajeti ya Jumla ya Waziri wa Fedha, mwanzoni mwa Mkutano huu, nilitoa maoni mbalimbali kuhusu mambo yafuatayo:-

Kwanza, kukua kwa idadi ya wajasiriamali wadogo wanaojitambulisha rasmi na kuwa tayari kulipa kodi ya mapato katika viwango vya chini kwa wastani wa mapato yao.

Pili, kuongezeka kwa wajasiriamali wadogo wadogo ambao wanayo makao maalumu ya biashara zao. Hii inathibitisha kwa jinsi vibanda na madirisha maalumu ya biashara yanavyoendelea kujengwa katika maeneo mbalimbali pembezoni mwa nyumba za makazi ya watu katika maeneo mengi ya miji nchi nzima.

Hii ni dalili nzuri ya kukua kwa biashara na wigo mzuri wa utambulisho wa walipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchambua *The Finance Act, 2007 na The Finance Act, 2008*, nimeona nia njema ya Wizara ya Fedha kuwajali wajasiriamali wadogo kama ifuatavyo: The Finance Act 2007, kiwango kisichotozwa kodi mapato chini ya TSh. 960,000; na The Finance Act 2008, kiwango kisichotozwa kodi ya mapato chini ya TSh.1,200,000. Sheria imeongeza wigo wa kiwango kisichotozwa kodi ya mapato toka TSh. 960,000 – 1,200,000. Kwa hali hii, Wizara inastahili kupongezwa.

Kwa kuzingatia mfano huo hapo juu, upo unafuu pia kwa viwango vingine kwa mlinganisho wa Sheria ya 2007 na 2008 kama ifuatavyo:-

(i) Kwa Jumla ya pato la Sh. 2,000,000

| **Sheria ya 2007** | **Sheria ya 2008** |
|---|---|
| Kodi ilikuwa: | Kodi ilikuwa: |
| 15% ya kiasi cha zaidi ya | 15% ya kiasi cha zaidi ya |
| Sh. 960,000 sawa na | Sh. 1,200,000 sawa na |
| 2,000,000 – 960,000 x 15% | 2,000,000 -1,200,000 = 800,000 x 15% |
| Kodi = Sh. 156,000 | Kodi = 120,000 |

(ii) Kwa Jumla ya pato la Sh. 3,000,000

| | | |
|---|---|---|
| **Sheria ya 2007** | **Sheria ya 2008** | |
| Kodi Sh. 180,000 + 20% ya | | |
| Kiwango zaidi ya 2,160,000 | 15% ya Pato zaidi ya | |
| 3,000,000 – 2,160,000 = | Th. 1,200,000 | 800,000 x 20% = 168,000 |
| = 3,000,000 - 1,200,000= | | |
| + <u>180,000</u> | 800,000x 15% = | |
| Kodi: = Sh. 348,000 | Kodi: Sh. 270,000 | |

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi siyo mtaalam wa kodi, nitapenda Mheshimiwa Waziri anisaidie kupitia mahesabu niliyotoa kama yapo sahihi. Iwapo yapo sahihi basi mfumo huo naupongeza sana na utaendelea kuhamasisha wajasiriamali wadogo kujitokeza zaidi na kujitambulisha kama walipa kodi kwa mfumo wa kuwa na TIN Namba.

Kwa sasa ipo haja ya kutaka Wizara ya Viwanda na Biashara, kutekeleza kuweka kanuni ili sheria iliyopitishwa ya uandikishaji wa biashara kuchukua nafasi ya leseni za Biashara ianze kutumika haraka ili kuipa nguvu zaidi sheria ya kuwa na TIN Namba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI**: Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka hizi zilianzishwa ili kufanya kazi Maalum ya Uhifadhi na kuendeleza shughuli za uhifadhi, kama vile kuongeza Hifadhi za Taifa. Kwa maana hiyo, kimsingi duniani kote mamlaka za namna hii, hupewa fedha na serikali na siyo kunyang'anywa fedha (kwa ajili ya maendeleo). Kama serikali inahisi kuna matumizi mabaya ya fedha kutokana na kuwa na fedha nyingi, imbane Waziri na siyo kuzipora fedha.

Waziri wa Fedha kwa kawaida ni mpenda pesa, kwa maana kuwa, lengo lake ni kukusanya fedha nyingi iwezekanavyo, kwa kawaida hana uchungu na masuala ya uhifadhi. Kwake masuala ya maendeleo ni ya kipaumbele kuliko ya uhifadhi. Kwa mtazamo huo, Waziri wa Fedha anaweza kupuuza matumizi fulani ambayo kwa kweli ni ya muhimu kwa uhifadhi.

Mifano ipo wazi, ambapo tumeona kila panapokuwa na mvutano kati ya uhifadhi na maendeleo mara kwa mara maendeleo hushinda. Mfano wa hivi karibuni ni Mradi wa Magadi wa Ziwa Natron. Nia ya serikali kuruhusu ujenzi wa hoteli ya kitalii kwenye realm ya Ngorongoro ilileta mjadala mrefu sana, kabla ya Uhifadhi kushinda licha ya Sheria na *EIA* kuwa wengi na upande wa uhifadhi.

Mapendekezo haya yakikubaliwa, itakatisha tamaa sana watendaji katika mashirika hayo na kupunguza ubunifu, uzalishaji na kisha mapato ambayo hayatatosha kuipa serikali na kuhudumia mashirika hayo.

Inajulikana wazi kuwa ni hifadhi chache tu kati ya 15 (yaani Serengeti, Kilimanjaro, Manyara, Tarangire na Arusha National Parks) zinazozalisha ziada inayotumika kuendeleza hifadhi kumi zinazobaki hususan kusimamiwa nchi. Hivi karibuni imeongezwa Hifadhi kubwa Barani Afrika ya Ruaha inayojumuisha maeneo ya Ihefu. Kama serikali itachukua ziada inayozalishwa na Hifadhi tano za Kaskazini, basi itakuwa vigumu kulinda na kuimarisha na hata kuendeleza hifadhi hii mpya. Zaidi ya hapo, suala la kupanua wigo wa utalii nchini (pamoja na mapato ya serikali), kusini kwa kutumia mapato ya hifadhi zilizopo kaskazini itashindikana. Matokeo yatakuwa *over utilization* ya hifadhi za kaskazini, kitendo kisichokuwa endelevu na mwisho tutaua hifadhi hizi za kaskazini na bila kuendeleza zile za kusini.

Napendekeza hoja hii isikubaliwe hata kidogo kwa vile itakuwa na athari kubwa zaidi ya kimazingira na kiuchumi. Kama ni lazima sheria hii ipite, basi ifanyike *EIA* kuainisha athari na faida zake *(Cost/Benefit Assessment).*

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii inapaswa kuangaliwa upya, hasa kwa sura mpya ambayo Waziri wa Fedha anayotaka kuijenga. Haieleweki na inazua masawli mengi:-

(a) Hivi Mashirika au Mamlaka za udhibiti zina udhaifu gani ambao Wizara ya Fedha inaona iingilie kati ili isimamie bajeti zake?

(b) Je, kutakuwa na uhusiano/mawasiliano gani kati ya Bodi/Waziri mwenye dhamana na Waziri wa Fedha?

Mapato yatokanayo na utozwaji wa kodi kwa mizigo katika malori yaendayo katika barabara kuu kwa kutumia *Weigh Bridges* huvuja sana. Udhibiti na ushuru katika maeneo hayo ni mdogo sana. Ni muhimu serikali ikae chini na wadau mbalimbali serikalini, kuhakikisha mapato yanakusanywa vizuri.

Kodi za Manunuzi katika Maduka inapotea nyingi. Wizara isichoke kuendelea kuwataka wanunuzi kudai risiti kwa kila bidhaa inayonunuliwa. Fedha nyingi sana inapotea.

Uandikishwaji wa maduka yanayostahili kulipa kodi ni muhimu ufanyike kwa makini sana. Bado maduka mengi hayapo kwenye regista ya walipa kodi

Nawatakia heri Waziri na Manaibu wake, kwa kazi nzuri kwa mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake na Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, *"Perpetual Loss Makers (Income Tax Act)"*, kurekebisha sheria za kodi ili kukusanya kodi toka kwa wafanyabiashara wanaoendelea kufanya hasara kwa muda mrefu na kutolipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kweli tuanze na *rate* hiyo ya 0.3%, lakini tujielimishe kwa kuwa huenda *rate* hii ikawa ndogo na ikabidi baadaye tuiongeze kwenda 0.4% au 0.5%.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu ifahamike kwa walipa kodi husika kuwa hiyo 0.3% siyo *final tax*, idara bado ina mamlaka ya kufuatilia na kukusanya kodi zaidi kama kodi hiyo ipo. Nimefarijika kwamba, kilimo, afya na elimu havihusishwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya kuondoa *VAT* kwenye magunia ni msaada mkubwa kwa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu wake wawili, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hiyo, kwa kazi nzuri ya kutayarisha Muswada huu na kuuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, ninayo machache ya kuchangia. Waziri wa Wizara ya Fedha katika hotuba yake ya bajeti, alitoa mapendekezo mbalimbali ya sheria zinahusiana na mamlaka ya udhibiti ikiwemo *EWURA, TCRA, SUMATRA, TCCA* na *PPRA.* Marekebisho hayo yanalenga uwezekano wa kurejesha serikalini ziada ya fedha ya tozo zinazoruhusiwa na sheria kutozwa na mamlaka hizo.

Marekebisho hayo yanahusu vifungu namba 8, 42, 44 na 46 vya Muswada unaolenga kubadilisha sheria ya fedha kwa kubadilisha sheria mbalimbali za udhibiti na kumpa Waziri wa Fedha mamlaka ya kupitisha *(approve)*, bajeti za mamlaka za *EWURA, SUMATRA, TCAA* na *TCRA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yaliyopo kwa sasa yamebadilishwa na sasa yamelenga katika mchakato wa kutayarisha bajeti ya mamlaka hizo. Kwa sasa, mamlaka hutayarisha bajeti zao na kuziwasilisha kwenye kipengele cha 49 cha *EWURA*, 25 cha *PPRA*, 47 cha *SUMATRA*, 54 cha *TCRA* na 36 cha *DAWASA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mapendekezo haya yatatekelezwa, tutakuwa tumeenda kinyume na maudhui ya sera ya ushindani ya mwaka 1999, ambayo ndiyo iliyosimamia uanzishwaji wa mamlaka za udhibiti.

Hii itakuwa ni kuingilia uhuru wa mfumo wa udhibiti. Mfumo huu usipokuwa huru, utaleta matokeo mabaya kwa uchumi wa Taifa letu. Itaongeza muono wa *regulatory risk* na hivyo kupunguza *credit rating* ya nchi.

Nchi yetu ikiwa na *credit rating* mbaya, basi itapata shida kuvutia uwekezaji katika sekta husika na hata pale wawekezaji/nchi ikikopa itafanya hivyo kwa gharama kubwa zaidi.

Kwa mtazamo huu, ndiyo maana sera ya ushindani ikawa na mfumo tofauti wa kugharimia shughuli za udhibiti wa kupitia kwenye tozo *(levies)*, gharama ambayo itabebwa na watumiaji huduma katika sekta zinazodhibitiwa na mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kama ilivyo kwa mamlaka nyingine za udhibiti hususan Benki Kuu, ambayo ni mdhibiti wa sekta ya fedha, haiingiliwi kwa namna ambavyo inalengwa na mapendekezo ya sasa. Mfumo wa sasa wa kupitiwa bajeti za mamlaka na Waziri mwenye dhamana za mamlaka husika, unatosha kuleta *checks and balances.* Kama nia ni kuiwezesha serikali kupata ziada inayotokana na makusanyo ya tozo, basi mapendekezo yalenge kwenye vipengele vya awali mfano, kama inabidi kurekebisha Sheria ya *EWURA*, kipengele cha 49 basi marekebisho yaliyopo, yaani kipengele cha 49A(1) yaondolewe, yabaki yale ya kipengele cha 49A(2).

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yote niliyoyatoa hapo juu, kimsingi yanalenga kuzipa mamlaka za udhibiti uhuru *"Regulatory Independence"* dhidi ya serikali, walaji na wasambazaji. Pia tukiondoa mapendekezo ya marekebisho hayo tutakuwa tunaendana na sera tulizojiwekea na hivyo kuongeza ufanisi wa marekebisho ya mfumo wa uchumi, kuwa uchumi wa soko na kuzidi kuwavutia wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kuishukuru sana serikali, kwa niaba ya wakulima wadogo wa miwa *(outgrowers)*, kwa uamuzi iliyochukua na kufuta tozo la *VAT* kwenye huduma zinazotolewa na vyama vya wakulima za kuandaa mashamba ya miwa, kukata, kupakia na kusafirisha miwa kwenda viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufutwa kwa *VAT* kwa huduma tajwa, kutaokoa gharama za uzalishaji na kutahamasisha wakulima kuboresha utunzaji mashamba ya miwa, mavuno kwa kila eka na ubora wa miwa kwa kuwa na sukari nyingi zaidi *(sucrose% in sugarcane).*

Mheshimiwa Naibu Spika, faida nyingine zitakazopatikana ni kuimarisha vyama vya ushirika au umoja wa wakulima kifedha kutokana na michango ya wakulima, ambayo itaviwezesha vyama kununua matrekta na *grab loaders* za kupakia miwa ya wakulima. Yote haya yataishia katika kuongeza ufanisi na uzalishaji wa sukari nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii, kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Prof. Mustafa Mkullo, Naibu Mawaziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa Muswada huu mahiri, wenye lengo la kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi pia niwaombee Mwenyezi Mungu, awape afya, nguvu, ari ya kazi na mshikamano ili waweze kutimiza azma yako katika kutekeleza Muswada huu. Vile vile kabla sijaanza kutoa mchango wangu, nitamke rasmi kuwa ninaunga mkono Muswada huu mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wazee sasa hawana uwezo wa kuzalisha mali hivyo tunapowadai kodi za majengo fedha za kulipa watapata wapi. Hivyo basi, kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa nchi hii alishatoa agizo la kuwasamehe, sioni sababu serikali yetu kupata kigugumizi kwa suala hili. Ninaomba wakati wa majumuisho, Waziri atoe maelezo kuna sababu zipi zinazokwamisha agizo hili zuri la Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Wabunge wenzangu kuwa, Bandari ya Dar es Salaam ni bandari mama, ambayo ina uwezo mkubwa sana wa kuingiza fedha za kutosha serikalini. Tatizo kubwa katika bandari yetu, huduma za bandari yetu sio nzuri na kusababisha wateja wengi kuhamia bandari nyingine mfano Mombasa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba serikali iboreshe huduma ya bandari yetu ya Dar es Salaam, pamoja na kuondoa msongamano wa makontena bandarini ili makontena mengi yaweze kupakuliwa kupitia bandari hii. Vile vile Waziri atoe ufafanuzi wa kuboresha huduma ya Bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Wabunge wenzangu, kuwapongeza Watumishi wa *TRA* kwa kazi kubwa wanayofanya ya kukusanya mapato mbalimbali yanayopitia kwenye idara yao, kwani kila mwaka makusanyo yao yamekuwa zaidi ya makisio yao ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba pongezi hizi ziendelee kuwatia moyo ili juhudi hizi ziendelee kwa maslahi ya Watanzania. Hivyo, ninaiomba serikali iendelee kuwapa motisha ili kuwatia moyo na kuwafanya wasipokee rushwa kwa wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba serikali itambue kazi kubwa zinazofanywa na Mbuga za Wanyama; Ngorongoro na *TANAPA*, kwani mapato wanayokusanya ni makubwa sana na fedha hizi zimekuwa na faida kubwa kwa Watanzania hususan vijiji vinavyozungukwa na mbuga hizo; mfano, kujenga barabara, shule, zahanati, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi ni kuzingatia mgawo wa fedha hizo zijulikane za kwenda serikalini, zinazobaki kuendesha mbuga hizi, pamoja na asilimia za maeneo husika. Ni vyema hoja hii aitolee maelezo msimamo wa Wizara ni upi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono njia mbalimbali za kuingiza fedha katika serikali yetu, bali ninaomba serikali baada ya kupata fedha iangalie maeneo

muhimu ya kupeleka fedha ukiwemo Mkoa wa Singida, ambao unasemekana ni Mkoa wa mwisho kwa uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba serikali iwe makini kuondoa kodi ya bidhaa kwenye viwanda; mfano, mafuta ya mboga ni bora viwanda vilipe kodi lakini watumiaji waondolewe kodi ili kuwapa unafuu watumiaji ambao wengi wao ni maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kurudia tena kuwa ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ninawatakia utekelezaji wenye tija.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana! Waheshimiwa Wabunge, sasa naona itabidi tumwite mtoa hoja aweze kutoa ufafanuzi katika vifungu mbalimbali, ambavyo vimetolewa maelezo na Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, akimaliza yeye, tutaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima, siyo Kamati ya Matumizi maana sasa tunatunga sheria. Mheshimiwa Waziri, amemwagiza Mheshimiwa Naibu Waziri aweze kujibu hoja.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii uliyotupa. Napenda kutoa shukrani za dhati Wabunge wote waliochangia Muswada huu kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale waliochangia kimaandishi. Ninaomba nianze kuwatambua Wabunge waliochangia kwa maandishi, lakini vile vile kwa kuzungumza na nianze na waliochangia kwa kuzungumza:-

Kwanza, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda - Mbunge wa Handeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji - Mbunge Baraza la Wawakilishi kwa niaba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Joseph J. Mungai – Mbunge wa Mufindi Kaskazini, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga – Mbunge wa Singida Kusini, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro – Mbunge wa Vunjo, Mheshimiwa John M. Cheyo – Mbunge wa Bariadi Mashariki, Mheshimiwa Job Y. Ndugai – Mbunge wa Kongwa, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes – Mbunge wa Karagwe, Mheshimiwa Anthony M. Diallo – Mbunge wa Ilemela, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi – Mbunge wa Kasulu Magharibi, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa – Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa – Mbunge wa Shinyanga Mjini, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi – Mbunge wa Ludewa, Mheshimiwa Michael L. Laizer – Mbunge wa Longido na Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa – Mbunge wa Mkanyageni kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Diana M. Chilolo na Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, kwa maoni na ushauri wao na pia kwa kuunga mkono Muswada huu. Ilituchukua muda sana kuwaridhisha kwenye sehemu mbalimbali za

Muswada huu ambazo zimejitokeza tena jioni na leo. Ilituchukua siku mbili, lakini baada ya hapo Kamati ya Fedha na Uchumi iliridhika kwamba, tuliyoyasema na tuliyoyakusudia na ambayo leo yamewasilishwa hapa, ndiyo sahihi na ndiyo yanafaa kuingia kwenye Muswada wa Fedha wa 2008. Tulimsikia Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii asubuhi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda alipowasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda vile vile kutoa shukrani zangu kwa Kambi ya Upinzani, kwa maoni na ushauri wao mzuri na niwahakikishie, huwa tunayasoma mnayoyasema na yale ambayo tayari tunakuwa tumeshayafikiria, tunayaingiza kwenye taratibu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nianze kujibu hoja mbalimbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo: Hoja ya kwanza, Mamlaka za Udhibiti kuchangia katika Mfuko wa Serikali: Mamlaka ya Waziri wa Fedha na Uchumi kudhibiti, kusimamia na kuratibu fedha za umma, yamebainishwa chini ya sheria mama inayosimamia masuala ya fedha za umma sura ya 348. Chini ya sheria hii, Waziri wa Fedha na Uchumi, amepewa pia mamlaka ya kutoa miongozo kuhusu matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya kurekebisha Sheria za Mamlaka au Wakala na Taasisi nyingine za Serikali, yana lengo la kumwezesha Waziri wa Fedha na Uchumi kutekeleza ipasavyo majukumu yake chini ya sheria ya fedha za umma. Aidha, mashauriano baina ya Wizara ya Fedha na Uchumi na Mawaziri wa Sekta zinazosimamia Wakala na Taasisi yatafanywa kiutawala. Miongozo na taratibu za uchangiaji huu zitaandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba, moja ya mambo ambayo yalizungumziwa sana kwenye Kamati ya Fedha ni hili kwamba sasa Wizara ya Fedha na Uchumi inataka kuunda ama kutengeneza kilichoitwa *Super Ministry* na kwa tafsiri hiyo, Waziri wa Fedha ni Mkubwa kuliko Mawaziri wengine wa Kisekta. Sisi hatutaki kuingia huko, lakini tunachosema ni kwamba, masuala yanayohusu fedha kwa mujibu wa sheria ni ya Waziri wa Fedha. Masuala kwa mfano ya maji ni ya Waziri wa Maji. Masuala ya miundombinu ni ya Waziri wa Miundombinu. Kwa hiyo, masuala ya fedha popote yalipo nchini, yapo chini ya usimamizi wa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana Bunge hili mwaka 2001 waliona ni busara kusema kwa sheria. Kwa hiyo, sheria ya fedha ikapitishwa na Bunge na ikarekebishwa mwaka 2004. Kwa hiyo, hatusemi kwamba hapa na kujidai kwamba Waziri wa Fedha kawazidi kimo wale wengine, ingawa Uingereza amewazidi yule *Chancellor of Exchaquer*, kawazidi wenzake! Waziri Mkuu wa Uingereza anakaa namba kumi, sijaingia mle lakini nasikia kuna mlango wa ndani kwa ndani unaoingia namba 11 ambako anakaa *Chancellor of Exchequer*. Sasa hayo ya Waingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapa, tusikilize Waheshimiwa Wabunge kwamba, sheria iliyopitishwa na Bunge inasemaje; *part II* ni *control and management of public finance. Duties and powers of Minister and the Treasury*. Katika kifungu kinachotafsiri *Minister* ni Waziri wa Fedha na Uchumi. Kifungu cha 5 kinasema; *it shall*

*be the duty of the Minister; (a) to develop and implement a micro-economic and fiscal policy framework for the United Republic and shall for that purpose supervise and monitor the finances of the United Republic*. Hicho ni kifungu cha 5. Kifungu cha 9 kinasema, *the Minister may make such regulations or give such directions as may appear to him to be necessary or expedient for the proper carrying out of the objects, purposes and provisions of this Act and assuring of the safety, economy and advantage of the public revenue and public property*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachoona hapa siyo kutaka kuingia kwenye mamlaka kwa namna yoyote ile ya Mawaziri wengine wa kisekta. Tunachosema ni kwamba ni lazima Waziri wa Fedha aelewe fedha zinasimamiwaje upande wa mapato na upande wa matumizi. Nitoe mfano, Waziri wa Utumishi; ukitaka wewe kuajiri mtumishi yeyote Wizara yoyote ni lazima upate kibali cha Waziri wa Utumishi. Ukitaka kuunda Wakala kwa mfano wa Wizara yako, huwezi kufanya hivyo mpaka muundo ule uidhinishwe na Utumishi na hiyo sisi hatudhani kama ni kumnyanyasa yule Waziri ambaye anataka kuunda ule Wakala. Mimi nafikiri ni majukumu haya ambayo yamepangwa na sheria na ndilo ambalo tunataka kufanya hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa inahusu kuondoa kodi katika miwa na mazao mengine; kwamba katika Muswada huu ni miwa tu ndiyo imeguswa kwa kuondolewa VAT na kwamba mazao mengine kama chai, uvunaji wa misitu na leo tumesikia kama pamba haikutajwa. Ni kweli haikutajwa, lakini mpaka kufikia kukubali kwamba, VAT iondolewe kwenye sukari, kazi kubwa sana ilifanyika na ninawashukuru hapa wenzetu wa *TRA* kwa kazi kubwa waliyofanya ya kutafiti na kuweza kumshawishi Mheshimiwa Waziri wa Fedha kukubali kwamba, *VAT* isitozwe pale ambapo Chama cha Wakata Miwa, wanavuna miwa na wanaibeba mpaka kiwandani na kwamba, *VAT* itachajiwa kutoka kwenye mazao ya sukari. Sasa tunachukua hili la mazao mengine na kurudi nalo Wizarani.

Nitaomba kwamba, bado kuna kazi ya kufanya kwa wale ambao wapo kwenye sekta hizi na wanataka wasamehewe *VAT*, kwa sababu haiwezekani kwa idai ya mazao tuliyonayo nchini, ukasema unasamehe *VAT* yote, hiyo itakuwa nadhani hujafanya sawa sawa. Pamoja na kutaka kuwa *open*, *equitable* na *fair*, hiyo sasa itakuletea mazingira mengine ambayo unaweza kuchajiwa kwamba, *you have been un-reasonable*. Kwa hiyo, nasema inabidi wale wa kwenye ile sekta wajenge hoja kwamba na wao wafutiwe *VAT* na wakifanya hivyo, hatua za kujiridhisha kwamba *VAT* inastahili ikifutwa, basi nina hakika Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atafanya hivyo chini ya Mamlaka ambayo amepewa na sheria na italetwa hapa kwa kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu ilikuwa inahusu tozo ya 0.3% kwa mashirika yanayopata hasara. Tulizungumza vizuri sana, tukaelezana vizuri sana na wenzetu kwenye Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, wakaridhika kwamba tena imechelewa kwa sababu ni kweli kuna mashirika hapa nchini makubwa tu ambayo yamewekeza hapa, lakini toka waingie hawajalipa kodi ya mapato. Kodi ya mapato nchini ni 30%. Hawalipi kwa sababu wanapotengeneza yale mahesabu yao kwa sababu ya misamaha ambayo walipewa, *Capital Allowances*, wanapopata faida kwa ajili ya kodi

wakiunganisha ule msamaha, wanaonyesha hasara, kwa hiyo, hawalipi kodi na mengine tukiyataja hapa tutashangaa. Kwa hiyo, tukafikiri haiwezekani, *this is not possible*, kwa hiyo, tukajifunza duniani kule. Wenzetu Wizarani na kwenye Mamlaka ya Mapato, wakaenda kwenye nchi ambazo zina mpango huu wa kutoza kodi hii kwenye mapato ghafi na wakarudi na elimu ya kutosha.

Kwa hiyo, tunachofanya hapa ni kusema sawa wewe hupati faida kutokana na biashara yako kwa sababu ya msamaha huu, lakini unafanya mauzo na tunajua kweli unatengeneza faida na wewe unakubali. Sasa sisi utatulipa kidogo lakini cha kutosha kutokana na mauzo ghafi yako. Sisi siyo wa kwanza na lengo sasa la kufanya hivi ni kwamba, tufike mahali ambapo wao wenyewe wataona ni bora kulipa 30% kuliko 30% baada ya kukokotoa pamoja na ile misamaha badala ya kulipishwa 0.30%. Kama tukiona kwamba 0.30% haizai matarajio yetu, tunatarajia kwamba tutarekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini 0.30%, hiyo inawiana vizuri sana na 30% ambayo inatozwa kwenye faida baada ya kuweka matumizi na gharama za kuendesha haya mashirika?

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nne inahusu ununuzi wa samani na magari kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Hili limesemwa siyo leo tu, lakini hata wakati Waheshimiwa Wabunge, walipokuwa wanachangia katika bajeti za Wizara hasa Wizara ya Fedha na Uchumi, lilitajwa hili. Mheshimiwa Waziri alijibu na alisema kwamba, hili tayari limeshaanza kufanyiwa kazi na Wizara ya Miundombinu na tunatarajia kwamba katika mwaka huu wa 2008/2009 tutapata jawabu la jambo hili. Sisi tukiri vile vile kwamba ni kweli kuna sababu ya kuchukua hatua kwenye mambo haya ikiwa ni moja ya mkakati wa kupunguza matumizi ya Serikali kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja namba 5 inahusu shughuli za Steve Doaring ziwe *zero rated* kwamba wasilipe VAT. Hii ni hoja ya ndugu yetu Mohamed Missanga, ambaye alikuja kwenye Kamati kule ya Fedha na Uchumi, akalizungumzia vizuri sana na leo amelirudia vizuri sana. Jambo hili lilifika Mahakama ya Rufaa; Mahakama ikaamuru kwamba tozo ambalo *TPA* walikuwa wamepewa walipe. Niseme hapa kwamba, sisi tumelipokea kwenye Kamati ya Fedha na uchumi na kama tulivyomwambia Mheshimiwa Mbunge pale, leo nitarudia kwamba tulilichukua na tumelichukua, tutakwenda kulifanyia kazi na kulitolea maamuzi. Tunajua kwamba, kama alivyosema Mombasa hawatozwi, tunajua, lakini ni lazima tulifanyie kazi na tujiridhishe kwamba huduma hii ya melini inafaa kusamehewa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya sita inahusu ushuru wa kusafirisha ngozi ghafi nje utozwe kwa shilingi kwa kontena badala ya asilimia inayotumiwa sasa. Kwa mujibu wa sheria hii, mauzo ya ngozi ghafi nje ya nchi yanatozwa asilimia 40 ya thamani ya ngozi au shilingi 400 kwa kilo kutegemeana na kiwango cha ipi kubwa, 400 ikiwa kubwa kuliko asilimia 40 ya thamani ya ngozi basi inachukuliwa ile kubwa na nyingine kuwa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu uliwekwa ili kuzuia udanganyifu wa thamani na hivyo tunaamini na huu unatosheleza dhamira hiyo. Hoja ambayo tumeipokea ni kutoza *flat rate* kwamba, kontena la futi ishirini basi tukubali tutoze dola elfu kumi na tano na kontena la futi 40 tutoze dola elfu 30 mara mbili ya 15, sawa lakini ni lazima tujiridhishe kama kuna sababu ya kubadilisha hili, maana sababu siyo tu kwamba tunataka kuepuka udanganyifu kwenye biashara hii, lakini vilevile tunataka kwa kadiri tuwezavyo, ngozi zisipelekwe nje. Ngozi ghafi tutengeneze viwanda vya ngozi hapa na tulikuwa navyo, kama dola 15 au 30 baadaye zitakuja kuonekana kwamba zinatufikisha hapo sawa, lakini na hili pia tutaendelea kulifanyia kazi, kuna haja ya kushauriana na hapo tutakaporidhika kwamba kubadilisha kutoka ilivyo sasa kwenda kwenye mapendekezo ya sasa basi itafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya saba inahusu misamaha ya kodi kwa makampuni ya madini, ushauri huu tumeupokea na umezungumzwa mara nyingi na Serikali inajiandaa wakati ikisubiri taarifa ya Kamati ya Jaji Bomani itakapojadiliwa na Bunge mwezi Oktoba mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nane ni *Withholding Tax* asilimia mbili kwa wasio na *tin*; ni azma ya Serikali kuwasajiri wafanyabiashara wote na kuwapatia vitambulisho vya walipa kodi. Hata hivyo, wapo wafanyabiashara wadogo wadogo kama vile wapambaji, fundi washi, fundi bomba na kadhalika, ambao huduma zao zinahitajika Serikalini lakini hawachangii katika mapato ya Serikali na wao kwa hiari yao hawajajiandikisha lakini tungefurahi sana kama wangejiandikisha. Tunasema wakati hilo likifanyika tuwabane, kwa hiyo, wewe kama ni fundi mwashi ukija kuomba kazi Serikalini ukapata, utalipwa lakini tutakukata asilimia mbili, kama ukiona hiyo itakuumiza basi ukajiandikishe, lakini niseme kwamba, fikra zetu kule Wizarani ni pana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu akitujalia hapo Watanzania watakapokuwa wamepata vitambulisho, basi sisi na wenzetu kwenye Mamlaka ya Mapato, tutatafakari kuona jinsi ambavyo tunaweza kumwandikisha kila Mtanzania mwenye umri kwa mfano wa miaka 18, pamoja na makampuni yaliyopo nchini na kuwapa kila mmoja *tin* na kuwataka kila mmoja atuambie kwa mwaka analipa kodi gani ama halipi, kama hulipi utupe sababu kwamba sina kazi, lakini hayo ni ya siku za usoni, kwa sasa hivi hili la asilimia mbili kwa wale ambao hawajajiandikisha na wana namba ya *tin* basi watatozwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tisa inahusu *pay as you earn* na hoja hapa ya Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, imeongezeka sana. Naomba nieleze kwamba, utozaji wa kodi ya *PAYE* kwa kweli haijaongezeka kama tunavyodhania. Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia katika Muswada huu walidhani kwamba imeongezeka, sisi tumefanya hesabu kabla na baada ya kusikia hizi hoja kujiridhisha kama tulikuwa hatukukosea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi kwa mwezi kwa viwango vya mwaka jana aliyekuwa akipata sihlingi laki moja kodi ya *PAYE* unakatwa pale unapolipwa mshahara ilikuwa shilingi elfu tatu sasa hivi mwaka 2008 ni 0 kwamba kima cha chini hakitakatwi

kodi. Kama ulikuwa unakatwa shilingi laki mbili kodi ya mshahara uliokuwa unakatwa ilikuwa shilingi elfu kumi na tisa, mwaka huu kodi inayopendekezwa ni shilingi elfu kumi na tano, shilingi elfu nne chini ya mwaka 2007/2008 na kama mshahara wako ulikuwa laki tano kodi ambayo ungelipishwa 2007/08 ilikuwa shilingi 86,000, kodi ya sasa italipishwa shilingi 67,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla kodi ya *PAYE* imepungua na haikuongezeka, lakini tutafurahi kama tutaambiwa tumekosea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kumi inahusu kiwango cha *VAT,* ambacho kinatumika nchini cha asilimia 20 kuwa ni kikubwa ukilinganisha na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuna vigezo ambavyo ni lazima uviingize kwenye uamuzi wao wa kwamba asilimia 20 ni kubwa kuliko kwa mfano, asilimia 16 ya Kenya au asilimia 18 ya Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, thamani ya fedha yetu imetofautiana kwa sababu mbalimbali. Kwa sasa tunadhani kwamba, asilimia 20 ya *VAT* kwa uchumi wetu na malengo yetu ya kutoza kodi ikiwa la msingi ni hilo wanaloita kulipa kodi kwa hiari, mara nyingine wanasema kwamba, asilimia 20 bado inafaa kutozwa. Bado tunalitazama sana suala hili na jinsi tunavyoendelea kulitazama, ninaamini kwamba, tukiona kuna haja ya kubadilisha, nawahakikishieni Waheshimiwa Wabunge tutabadilisha, lengo letu ni kuwezesha ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutumia neno moja la jirani yangu kule Meru (kutekenya uchumi), ndiyo lengo letu ili ukue, kwa hiyo. kama tukiona 20 inadumaza …

**NAIBU SPIKA:** Hicho cha kwao wala siyo Kiswahili. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Kama asilimia 20 inadumaza uchumi, basi tutabadilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kumi na moja ni kero za ucheleweshaji wa malipo ya pensheni zisitokee tena. Serikali imetafakari ushauri wa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamelisemea jambo hili na baadhi ya wastaafu kuhusu malipo ya pensheni kwa wastaafu wenyewe ambao watahamishiwa katika mifuko mbalimbali ya pensheni kwa ajili ya malipo ya pensheni na kufikia uamuzi wa kuendelea kuwalipa kwa kipindi cha miezi sita sita kama ilivyokuwa hapo awali, baada ya hapo ni malipo ya mwezi mmoja mmoja, tutawalipa pensheni yao kwa miaka mitano iliyobaki kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uamuzi huu, Serikali inapendekeza kurekebisha sehemu ya 7, 11, 12, na 14 ya Muswada ili kubainisha kuwa, Serikali itawasilisha fedha za mafao ya wastaafu waliohamishiwa katika mifuko husika katika kipindi hiki cha miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili sasa hata sisi kule Wizarani, Fedha na Uchumi, maana yake hata sisi tuna mioyo tena mingine laini, linakera kwa sababu hata sisi hawa ni ndugu zetu, nia yetu kabisa ya dhati suala hili la wastaafu liishe ili tuanze kuzungumzia mambo mengine. Nakiri Mheshimiwa Waziri, Naibu mwenzangu na Watumishi wenzangu kule Hazina na sisi linatukera. Kwa hiyo, suala hili tutalisimamia sasa; siyo kuhusu hili lililosemwa hapa la jinsi tutakavyowalipa, lakini kutafuta jinsi ambavyo itatuwezesha kupunguza adha ya wazee hawa mara nyingine kusafiri mbali na wakati pensheni yenyewe wanayokwenda kuchukua ni ndogo na mara nyingine inaishia kwenye safari. Hilo limesemwa katika majibu mara nyingi hapa wakati wa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tunalishughulikia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushuru wa bidhaa kwenye muda wa maongezi kwa simu za mikononi, ongezeko la kodi ya muda wa maongezi ni sawa na shilingi kumi kwa dakika ikilinganishwa na gharama ya muda wa maongezi wa shilingi 350 kwa dakika hivyo ni dhahiri ongezeko hili haliwezi kuwa na athari katika uwekezaji na upanuzi wa huduma kama inavyodaiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii asilimia 7 - 10 ambayo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamechangia na wanashauri kwamba ibakie hivi hivi, niseme kwamba, lilikuwa na kazi kweli na limeanzia mbali. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, amefanya kazi kubwa sana ya kuwasiliana na Mawaziri wenzake wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuzungumza nao, Kenya wapo kwenye asilimia kumi, Uganda wapo kwenye asilimia 12, sisi tulikuwa kwenye asilimia saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na asilimia saba hiyo, haikutosha tu kupeleka kumi kwa sababu Uganda wapo 12 na Kenya wako kumi hapana, tumejiuliza maswali mengine; hivi kwa mfano ni kweli kwamba, gharama zote zitakazotokana na ongezeko la kodi hii zitatupiwa mlaji? Kama ni hivyo ninawaomba *TCRA* ambayo ndiyo wadhibiti wa hawa wenzetu wafanye kazi yao, maana sisi tunajua kwamba wenzetu hawa wa mawasiliano wana faida ambayo inaweza kuchukua sehemu ya hii kodi na kwamba si lazima mlaji alipe. Najua kwamba, hilo ndilo wazo ambalo linatumiwa na hata wakati ule ambao tulikuwa tunatoa mapendekezo haya, walikuja kujenga hoja kwamba, mkifanya hivyo tutawagonga walaji, sisi tukawaambia hapana hiyo siyo haki kwa sababu faida wanayoitengeneza hata wakitumbukiza hizi gharama zote kwenye faida wanayotengeneza bado watatengeneza faida ya kutosha na sisi tunajua hesabu kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakiendelea kung'ang'ania kwamba, watatoza wananchi sehemu yote hii ni dhahiri kwamba, baadhi ya wananchi ambao wana *cell phones* wataanza kuondoka au wale ambao wana-*beep* wataongezeka. Hao sina tatizo nao, maana wakiku-beep watarudisha *call* kwa hiyo *you will make a call, any way* itafikia mahali ambapo hawawezi tena kumpasia mlaji gharama hizi, itabidi waamue.

Haya ni maarifa ya biashara, wawe na wateja wengi ambao wanatumia simu zao na laini zao ama wawe wachache *and they will have to determine* mahali ambapo wataishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tukajiridhisha kwamba, hii ni halali na kwamba, inaweza kubebeka na haitakuwa na athari kwenye uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kumi na tatu ni kodi kubwa ya hoteli kwa wafanyabiashara ndogo. Sheria ya ushuru wa hoteli inatamka kwamba, mmiliki wa hoteli au nyumba ya kulala wageni ambayo haijasajiliwa kwa ajili ya kukusanya *VAT*, kulipa ushuru wa hoteli kwa kiwango cha asilimia 20 ya mapato kutokana na huduma ya malazi. Kwa mujibu wa sheria hiyo, ushuru unaotozwa kwenye nyumba ya kulala wageni unapaswa kulipwa kwa Halmashauri ambapo ushuru unaolipwa na hoteli hulipwa na Serikali Kuu. Sheria inamsamehe mfanyabiashara anayesajiliwa kwa ajili ya kukusanya *VAT* kwa kuzingatia kuwa, wateja wake watatozwa *VAT* na kutoza tena ushuru wa hoteli ingekuwa ni kutoza kodi mara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, wafanyabiashara wa hoteli wanashauriwa kuwasilisha maoni yao kuhusu kodi na ushuru wa hoteli kwenye kikosi kazi cha kurekebisha mfumo wa kodi kinachosimamiwa na Wizara ya fedha na Uchumi na pale watakapofanya hivyo, basi tutatazame kama ni hekima kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kumi na nne ni taratibu za kisheria kwa kutumia mapato ya ziada. Hoja hii ililetwa na Mheshimiwa Cheyo asubuhi ingawa hakuchangia rasmi. Tunadhani ni vizuri tukaeleza maana hii inatokana na zile fedha ambazo Mheshimiwa Rais amesema kwamba, zitakwenda kwenye kilimo. Upo utaratibu wa kisheria wa kuingiza matumizi ya ziada kwenye Bajeti ya Serikali endapo yatapatikana mapato ya ziada kugharimia matumizi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mapato ya ziada kama haya kupatikana, Serikali itaamua maeneo ambayo mapato hayo husika yatatumika na kwa hilo ambalo aliulizia Mheshimiwa Cheyo, tayari maamuzi yameshafanyika. Hatua hii ikishakamilika ikijulikana ni wapi ziende, Wizara ya Fedha na Uchumi, inaandaa Muswada wa Matumizi ya Ziada *(Supplementary Estimate),* ambayo inabainisha vifungu ambavyo fedha zile zingerekodi. Muswada ukishatengenezwa unajadiliwa na Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge, halafu Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge ikisharidhika linaletwa hapa na Waheshimiwa Wabunge wanapata fursa ya kujadili na kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nina muda kidogo, ninaomba nijielekeze kwenye mambo ambayo yalisemwa mchana huu na Waheshimiwa Wabunge waliozungumza na mengine ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliyataja, wakati alipowasilisha Muswada huu. Inaelekea Waheshimiwa Wabunge, hawakusikia vizuri. Jambo la kwanza, linahusu mafuta na malighafi za mafuta yanayoingizwa nchini. Ukurasa 30 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, asubuhi ilisema na ninaomba niisome:

"Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mkutano wa wadau wa mafuta ya kula ulifanyika hapa Mjini Dodoma tarehe 25 Julai, 2008. Mkutano huu ulishirikisha wakulima wa mbegu za mafuta ya wenye viwanda vya kutengeneza mafuta ya kula yanayotokana na mawese. Aidha, kwa kuzingatia hoja za wadau, Serikali imeamua kwamba, kwanza Tanzania iendelee kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia kumi kwa mafuta ghafi ya kula yanayoagizwa kutoka nje ya nchi. Pili, Serikali itafanya utafiti kubaini mahitaji halisi ya Taifa ya mafuta ya kula na mazingira ya kuzalisha mbegu zaidi kwa kuwa hadi sasa utafiti uliopo umeonyesha kwamba, hakuna mafuta ghafi yanayoagizwa kutoka nje ya nchi, badala yake mafuta yanayoagizwa kutoka nje yanakuwa tayari yamepitia hatua kadhaa za usindikaji."

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu kutoka Kigoma Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, alikasirika sana wakati akichangia jambo hili na sisi tulimwelewa kwa sababu Kigoma kuna ardhi kubwa. Nadhani ni mawese ambayo anataka yalimwe au tayari yanalimwa ingawa siyo mengi sana na kwa hiyo inaelekea kifungu hiki kilimpita. Sasa namwomba kwa heshima zote, hasira ipungue kidogo, tayari Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi alikwishalisemea na asivunje rekodi yake ya kuunga mkono Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge mwingine ambaye amechangia hapa kwa kuzungumza alikuwa ni Mheshimiwa Mungai, yeye alisema kwamba, sheria hii inamwezesha Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi kuchota. Tumeona kwamba, kwa kweli sivyo, kutakuwa na mashauriano na usimamizi alioushauri wa *eyes on hands off* na Wizara ya Fedha na Uchumi ni sehemu ya dhamira hiyo kwamba, tunataka kujua fedha za Serikali ziko wapi, siyo matumizi tu. Lengo la hili siyo kuzichukua, maana tumesikia Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa amesema, kule nyuma kabla mamlaka hizi hazijafikia hapa zilipo, zilikuwa zinapata ruzuku kutoka Serikalini na hata sasa kama ikibidi kweli kwamba kuna mamlaka ambayo itahitaji ruzuku ni lazima itakuja Hazina tu. Kwa hiyo, tunachosema kwa kuanzia siyo kwenda kuchota fedha, lakini basi tuanze kuelewa na kama nilivyosema ni jukumu tu la Waziri wa Fedha na Uchumi *to understand these things* na haingilii mamlaka ya mtu yeyote, yeye anazungumza fedha tu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ninawaombeni sana tutembee pamoja kwenye hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo Mheshimiwa Mungai alilisema linahusu *inadequate disclosure* ya baadhi ya mashirika yetu. Usipokuwa muwazi kwenye taarifa kwa wanahisa, basi unapotosha wale wanahisa na alitoa mfano wa Benki moja. Mimi siyo msemaji wa Benki hii, lakini kwa kuwa aliitaja, nami niitaje *CRDB.* Alichosema ni kwamba, *EPS* ni *earnings per share*, yaani kila hisa moja imechuma kiasi gani, kipato cha hisa kabla ya gawio, akasema hiyo haionyeshi, kwa hiyo, wanahisa wanapunjwa maana wanapewa gawio dogo. Nadhani ni vizuri kuelewa na hiyo faida inayobaki inaenda wapi. Benki hii na Benki nyingine na sisi ni wasimamizi wa hizi Benki vilevile, wanapotoa gawio ile faida inayobaki inawekwa kwenye *reserves* na inasaidia katika kukuza na kujenga uwezo wa kuzalisha zaidi kile wanachofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, inafika wakati hii Benki ama hili shirika, linakuwa imebakiza faida kubwa sana kwenye mizania yake kuliko ule mtaji wa msingi na pale wanatoa hisa za upendeleo ama *Bonus Shares.* Benki hii imetoa na kila hisa uliyonayo, kwa kufanya hivyo wamekupa gawio isipokuwa linakuwa limechelewa tu. Sisi tunaridhika tunapotazama haya mabenki na Benki Kuu ambaye ni Msimamizi Mkuu ameridhika. Ninawahakikishia Waheshimiwa Wabunge, kama kungekuwa na dosari, tayari Benki Kuu ingekwishachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, alizungumza vizuri sana, kwa kweli nampongeza. Anasema hawa wenzetu wa Ngorongoro na *TANAPA*, wana jukumu kuu la uhifadhi; ni sawa na wanayo majukumu mengine mengi, lakini hiyo siyo sababu ya kutosha ya kumnyima Waziri wa Fedha na Uchumi, fursa ya kuelewa kinachoendelea kuhusu matumizi ya fedha mle ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema inaweza kutokea kwamba, kutakapotokea mashauriano kati ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri mwenzake wa sekta, kwamba kumbe hili tunalosema wala siyo, hawa watu ili tuwaongezee uwezo wa kushiriki vizuri zaidi kwenye kukua kwa uchumi, siyo tu wanahitaji kuchukuliwa fedha, wanahitaji fedha zaidi. Kwa hiyo, anaanza kuumwa kichwa sasa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni wapi apate fedha za ziada za kuwapa hawa ili washiriki vizuri kwenye kukuza uchumi wetu? Kwa hiyo, si upande mmoja tu na lengo la Muswada huu na vipengele hivi vina nia nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba kutatokea na kukinzana kati ya Waziri wa Fedha na Waziri wa sekta *why*? Kwanza, kutakuwa na utaratibu, kanuni, miongozo na vigezo vilivyotajwa baada ya hili vitabuniwa, lakini Waziri wa sekta hawezi kwenda kwa Waziri wa Fedha kwa ajili ya ugomvi, maana nia yetu ni moja, uchumi wetu ni mmoja, Serikali ni moja, mimi siamini kama tukifanya hili jambo kwa nia nzuri hilo litatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ndungai alisema pia itakuwa rahisi sana kwa Waziri wa Fedha, kuona fedha pale kuliko kuona wanyamapori. Nadhani tutaona tu wanyamapori na hata sasa tunawaona tu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Missanga pia amelizungumzia. Mzee wangu lile la *Steve Doaring* kama nilivyosema, tunakwenda nalo litatazamwa. Tutazame ni wapi na ni kitu gani ambacho hatujakiona; kama kipo basi tutakirekebisha. Hii kodi ambayo imeshasemwa na Mahakama ya Rufaa ilipwe, itabidi ilipwe.

Hoja nyingine ya Mheshimiwa Mohamed Missanga ilikuwa inahusu ushuru kwenye mafuta mazito, ambao lengo lake ni kupunguza gharama za uendeshaji ili zile gharama za uendeshaji zipungue bidhaa inayozalishwa iwe na bei nafuu kwa Mtanzania. Kinadharia, nakubali kabisa kwamba ndivyo ilivyo, lakini sasa kwa bahati mbaya ile bei kwa mlaji ni mlolongo wa gharama nyingine za uzalishaji na misululu mingine hapa katikati kabla ile bidhaa haijamfikia mlaji. Kwa hiyo, pamoja na kwamba, tungetegemea kuondoa ushuru kutapunguza bei kwa mlaji, ninakiri kwamba, ukitazama bei inaongezeka utasema basi haifanyikazi. Nafikiri mantiki hapa tuseme basi kama huu

ushuru hautolewi kwenye mafuta ghafi haya, bei kwa mlaji ingekuwa kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa ingawa bado ni juu kuliko ambavyo tunatarajia.

Namshukuru Mheshimiwa Aloyce Kimaro kwa kutupongeza kuhusu hatua zilizochukuliwa kuhusu mafuta ya kula kwa ile asilimia kumi, lakini vile vile kutupa moyo kwamba, Muswada huu ni mzuri na unafaa kupitishwa na Wabunge. Tahadhari zake tusinunue *furniture* nje na magari ya kifahari tumeshalijibu.

Mheshimiwa Anthony Diallo, alizungumza naye siyo kwa hasira lakini kwa nguvu na nadharia nzuri sana. Namshukuru sana, ametukumbusha misingi ya kodi nzuri na utozaji mzuri wa kodi *equity, fairness, convenience, openness and non arbitrariness*. Ndilo tunalojaribu kulifanya. Pia alisemea kuhusu kuondoa *VAT* kwenye miwa, tumesema kwamba na sekta nyingine basi na wao wejenge hoja halafu tuone kama itawezekana kuondoa *VAT*.

Halafu Mheshimiwa Esther Nyawazwa, namshukuru sana kwa kutupa moyo, vigezo vitakavyotumika vitawekwa lakini hatudhani kama ni vyema tukaweka kwenye Muswada huu wa Fedha. Pamoja na kwamba, tunahamishia ulipaji wa pensheni kwenye Mifuko hii na mabenki ya wastaafu wetu bado, tunakiri kwamba, haijamaliza tatizo la usumbufu. Mimi ninawaahidi tu kwamba, sisi tumeridhika kwamba, bado na tunalifanyia kazi kujaribu kupunguza hii adha. Kwa mfano, tuna *sub-treasury* katika kila mkoa, tayari tunafikiria jinsi ambavyo tunaweza kutumia hawa wenzetu pale kwa kujibu baadhi ya maswali na haja za wastaafu wetu badala ya wao kufunga safari kuja Dar es Salaam na mambo mengine. Haya ni mambo ambayo yatakuja kuonekana matunda baada ya kufanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtoa hoja, Waheshimiwa Wabunge, napenda kutumia Kanuni ya 28(2), kuongeza muda usiozidi dakika 30 ili tuweze kumaliza shughuli tulizonazo. Endelea Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Esther Nyawazwa alisemea kuhusu kusamehe kodi kwenye majengo ambayo ni ya wazee na alitaja Agizo la Rais. Kama ni Agizo la Rais, itakuwa *specific,* nadhani na hilo wala halina haja sana ya kulijadili. Kama tulivyosema, kusamehe kodi huku kumeachiwa Halmashauri na wenzetu wa mapato ya kodi, ambao ndiyo watashughulikia jambo hilo.

Ukisema tu wazee wasamehewe kodi mbona ni pana sana, tunafahamu wazee wengi sana ambao ni matajiri sana na hawana haja ya kusamehewa kodi, kuna nyumba za wazee ambazo ni nyumba za wageni. Nyumba iliyo kwenye Halmashauri, nisingedhania wangesamehewa kodi. Kama ni kile chumba ambacho mzee anaishi na hana uwezo, nafikiri wenzetu kwenye Halmashauri na Mamlaka ya Mapato Tanzania, watatumia busara zao. Wao nina hakika watafikia mwisho mzuri kwa hao wazee wetu maana nao ni wazee wao vile vile.

Mheshimiwa Blandes, nakushukuru sana kwa uliyoyasema, tutayachukulia maanani isipokuwa kufuta hivi vifungu hapa bwana unatuweka pagumu? Mimi naomba hiyo tusiendeleze maana unasema tufute hivi vifungu. Tukivifuta vifungu hivi ndiyo tena hapo mambo hakuna *game*. Kwa hiyo, naomba utuelewe.

Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa naye amezungumza vizuri sana, lakini natarajia kwamba, baada ya kutoka jasho hapa na maelezo yote haya na yeye vile vile atatuunga mkono.

Halafu Mzee Michael Lekule Laizer, mzee wetu kule amezungumza kuhusu wapiga kura, sawa nafikiri yote hayo tunaelewa ni jukumu letu kujibu. Kwenye madini Mheshimiwa Laizer tunaogopa Wazungu hata kuwatoza kodi hatuwatozi. Sijui kama ni kweli, lakini mara nyingine napata tabu sana kuzungumza Kiingereza. Sidhani kama tunawaogopa, hatuogopi hata kidogo. Ingekuwa hivyo, basi hata mwalimu asingethubutu mwaka 1961, hawa ni *size* yetu tunawaendekeza tu.

Utaratibu wa mifugo kupelekwa Kenya kwa magari, utatuwia mgumu kidogo inabidi tukazanie kujenga viwanda vya ku-*process* hawa ng'ombe wetu. Najua kuna kiwanda kinajengwa Arusha na kuna vingine vinajengwa. Kwa hiyo, hili silijui sana. Alisema wasipitishe ng'ombe kwenye njia ya panya. Sasa Mheshimiwa Laizer tutazungumza, maana ni ndugu yangu na jirani yangu, hii ya ng'ombe na magari.

Masoko ya mitaji, nakubaliana na yeye kuna haja ya kupeleka masoko kwa Watanzania wote na si kwa wafugaji tu. Najua imefanya sana, toka soko la hisa lilipoanza mwaka 1994 lakini ni dhahiri kwamba, bado kuna juhudi zinazohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Wakati nasema naongeza muda, nilitumia kifungu cha 28(2), kumbe hicho kinatumika mchana. Sasa cha jioni ni kifungu cha 28(5), kwa hiyo, tunaendelea.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilitaka tuweke tu kumbukumbu sahihi. Hii ibara ya 3 ambayo inaendelea na mambo hayo hayo

ya mamlaka ya Waziri. Nilitaka kusema, sheria zote zinazoanzisha haya mashirika ya umma, zinatamka wazi kwamba, wanapomaliza kutengeneza.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza Mheshimiwa Mbunge. Ibara ya tatu inasema; *this Part shall be read as one with the Capital Markets and Securities Act hereinafter referred to as the "principle Act."* Mbona haihusiki na hayo unayosema?

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upo sahihi, mimi niliona nisimamie kwenye hilo kwa sababu ukiendelea ukurasa wa 4 kwenye ibara ya 3 inazungumza juu ya fedha, bado hazijapelekwa kwenye *Consolidated Fund Services*. Sasa ndiyo maana nikasema nisimame kwenye hicho kifungu.

**MWENYEKITI:** Huwezi kwa sababu tunatunga sheria kufuatana na ilivyo hapa. Tujadili sasa, kama kuna mabadiliko katika kile kifungu unataka kubadilisha nini badala yake?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 14

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba ibara hii kwa sababu hizo hizo.

**MWENYEKITI:** Ibara mpya ya 14.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Ibara ya 14(c), pale ambapo kuna *the income tax payable by a corporation with perpetually under lived loss for three consecutive.*

**MWENYEKITI:** Wewe unasema nyingine haina (c) ina (a) *and* (b). *Okay* endelea Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Kwamba, hizo sababu zilizotumika kwa *agricultural business*, *health,* pamoja na *education*, basi zitumike kwa *local companies* zinazofanya *electrification* kwa sababu nazo zina umuhimu kama huo. Kwa hiyo, zinaweza kutumika na hiyo *electrification project.* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umekipata anachokisema?

Mheshimiwa Mnyaa, naomba urudie tena. Tupo ukurasa wa 12, ibara iliyokuwa ya 15 sasa ni ya 14, kwenye marekebisho ukurasa wa kwanza; *(c) by adding immediately after subsection (7) the following new subsection: The income tax payable by a corporation with perpetual unrelieved loss for three consecutive years of income under paragraph (a) of subsection (1) shall not apply to a corporation conducting agricultural business or engaged in the provision of health or education."* Sasa ameuliza umeelewa swali lake?

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nirudie katika ibara hiyo hiyo, lakini kwenye hii sheria ya *income tax* kwamba, kuna *section* inayosema; *The income tax payable by a corporation with perpetual unrelieved loss for three consecutive years of income under paragraph (a) of subsection (1) shall not apply to a corporation conducting agricultural business or engaged in the provision of health or education.* Sasa nilikuwa nauliza kwa nini Mheshimiwa Waziri asiongeze na hii *local electric companies* yanayofanya *electrification* ambayo sababu hizo hizo nazo zina-*apply* kwa hiyo ya mwanzo?

**MWENYEKITI:** Anasema *electrical companies*.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaliangalia hilo na tunaweza tukaliongeza.

**MWENYEKITI:** Hapana bwana, hapa tupo kutunga sheria, tukianza kuangalia tutaweka wapi baadaye yale mtakayoyaangalia mtayatupa wapi?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 17

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara hiyo, *subsection* (b) inayozungumzia juu ya 3% *on turnover;* sijui kama tuko pamoja?

**MWENYEKITI:** Anza tena. Marekebisho ya hii ibara yapo ukurasa wa 2, kifungu kidogo cha (i) kinasema ni *clause* 18 umeyaona? Sasa msikilizeni.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Sasa swali ninalouliza; je, hii sheria itaweza kutumika pia kwa makampuni ya madini yaliyo na mikataba ambapo pametokea matatizo kama haya ambapo makampuni yametengeneza wanachoita *commercial profits*, lakini hajatengeneza *taxable profit*? Nilikuwa nataka ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, ulitaka kusema kwamba, je, makampuni ya madini nayo yatahusika? Huna tatizo na ilivyowekwa; hujui kwamba makampuni ya madini yatahusika, ndiyo swali hilo tu maana hapa tunatunga sheria?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo lazima iwe hivyo, kwa sababu makampuni mengi ya madini yana Mikataba Maalum na Kamati ya Mheshimiwa Jaji Bomani imependekeza mapendekezo maalum. Kwa hiyo, tutayachambua yote, yaani mikataba maalum waliyonayo na maekelezo ya Mheshimiwa Jaji Bomani.

Kwa hiyo, kama inawezekana tutaziweka, lakini siyo lazima kwa sababu kama mkataba unasema kitu kingine, itabidi tu-*negotiate* ule mkataba kabla hatujafikia kwenye hii.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kama ni hivyo, basi kwa sababu hii sheria ina-*apply*, tukishaitunga labda waweke *except* ili ijulikane, lakini ukiweka hivi mimi sioni kwa nini wale wasilipe.

**MWENYEKITI:** Tunachokijadili sasa ni kutunga sheria kama ilivyo hapa, haina tatizo lolote. Watakapokuwa wana-*apply* kama wakiona inabidi na madini wa-*apply*, wata-*apply* kwa sababu hapa tunatunga sheria hatutaki ufafanuzi *whether* tunatunga sheria. Kama haya maneno ungekuwa unasema hayatoshi, badala ya kusema *rate* inakuwa 0.3% iwe 10% au iondoke kabisa *that will be the discussion*.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ndiyo hasa ninachokisema hapa na hii siyo mara ya kwanza kwamba, kwamba, *unless* inapotungwa inakuwa na *exception* kama hutaki hiyo sheria i-*apply* katika *a certain section*. Ilivyo hivi sasa, sisi tutakaosoma hii sheria na mtu mwingine ataona kwamba hii sheria ina-*apply* kwa watu wote ambao wana mtindo wa kupata *profit*. *Profit* ambayo huwezi ukaitoza kodi, *because* ndiyo alivyokuwa anazungumza Waziri hata kwa *speech* hii, ndiyo ilikuwa dhana yake kwamba, tunapoteza mapato mengi, watu ambao wana-*declare* kwamba wana hasara kumbe wana faida.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, tunasema kitu kimoja kwamba, haya maelezo ni *enabling clause;* kama angeandika hapa ingebidi aandike kila kitu ambapo haiwezekani.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 19

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ufafanuzi uliotolewa na Mheshimiwa Waziri, ninaomba sasa kwa heshima kubwa, baada ya kurejesha kodi ya mafuta ya kupikia, niunge mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, mimi nakubaliana na kuunga mkono sawa, hata ungepinga sijui ungepingaje, kwa sababu tunatunga sheria hatutoi shilingi ya Waziri au nini, hapa tunatunga sheria? Kama wewe umeridhika kwamba sheria imetungwa sawa sawa basi vizuri.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge*

*Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, wakati ananijibu nilikuwa na hoja ambayo nilitoa kuhusu mgongano kati ya Wizara Mama na Wizara ya Fedha. Kwa kuwa tunatunga sheria, nataka twende moja kwa moja ile ibara ya 27 ambayo ni ya 26 sasa, ambayo inaendelea ukurasa wa 17 ule ni mwendelezo wake pale (13)(a)(1), nataka niisome ili nijieleze vizuri katika hoja yangu. "*Upon approval of annual or supplementary budget under section 13, the Minister shall cause such budget to be submitted to the Minister responsible for finance for approval.* Taasisi moja inakuwa *managed* na Mawaziri wawili na *approval* wawili. Je, huo siyo mgongano?

**MWENYEKITI:** Sasa wewe una-*amend* nini?

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mimi nina-*amend* kwamba, *approval* ya Waziri wa *Finance* iondoke kwa sababu *approval* tayari ipo pale juu huwezi ku-*approve*.

**MWENYEKITI:** Sawa utapata maelezo lakini huwezi ku-*amend* kwa kusema bila kuleta *amendment* yoyote.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Nakubaliana lakini itakuwa ni kulitumia Bunge vibaya, kupitisha jambo kama hili la *approval* mbili kwa kitu kimoja wakati Serikali ni moja na Kamati ilishauri na walitueleza kwamba, walimshauri Waziri hakusikia. Tumemweleza wakati tunachangaia hapa hajataka kusikia. Sasa tunasimama tena dakika hii kweli *approval* mbili ni sawa sawa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. JEREMIAH S. SUMARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nifafanue hoja ya Mheshimiwa Ndugai kama ifuatavyo:-

**MWENYEKITI:** Ufafanue kifungu hiki, maana yake nini; anavyosema Mheshimiwa Ndugai hizo shida zipo au vipi na kama zipo unasema nini ndiyo swali lenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. JEREMIAH S. SUMARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, hicho kifungu kinatambua mamlaka ya sekta; *Minister* ni Waziri wa Wizara ile, anayo mamlaka kamili kuhusu ile bajeti yake na anapo-*approve* ni kwamba, sasa kakamilisha ile bajeti. Tunasema Waziri wa Fedha sasa anafanya vitu viwili tu kuamua ni kiasi gani ambacho inawezekana hii Wizara ikachangia kwenye Mfuko Mkuu wa Fedha au ni kiasi gani ambacho wao wenyewe watapatiwa.

Vile vile Waziri wa Fedha anasema ni kiasi gani kitabaki kwenye ile Wizara. Kwa hiyo, Mawaziri wote wawili wanayo *role* na sioni kama kuna mgongano. Niseme, tukipe hiki kifungu nafasi ya kufanya kazi. Kama itatokea na hatuoni jinsi ambavyo kutatokea mgongano hata kidogo maana Waziri ana *role* yake na huyu ana *role* yake. Nilitoa mfano, kama utaniruhusu; wakati unapotaka kuajiri wafanyakazi kwenye Wizara

yoyote ni lazima wale wafanyakazi wapate *approval* na Waziri aridhike. Hiyo haitoshi, lazima uende kwa Waziri wa Utumishi ndiyo ikamilike. Kwa hiyo, sioni mgongano hapo.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hili analolisema la Waziri wa Fedha, kuweza kuchukua kuingiza katika Mfuko Mkuu lipo kwenye kifungu cha pili ambacho mimi sijaligusa. Ipo *covered* vizuri kwenye kifungu cha pili cha hiyo sheria. Kifungu cha kwanza kinasema, Waziri wa sekta ata-*approve budget* au *supplementary budget*. Halafu Waziri wa Fedha naye ana-*approve* nini wakati amesha-*approve* Waziri wa Sekta?

Kwa hiyo, abakie Waziri wa Sekta a-*approve* halafu ibakie hii *section* ya pili, kama anavyotaka yale mamlaka ya Waziri wa Fedha kuangalia na kuweza kuchota fedha kama akitaka kufuatana na maelekezo mengine. Pale kuna mgongano ambao upo wazi kabisa kwenye kifungu cha kwanza.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa sababu ni sheria, hatuelezi mambo yote yanayotakiwa kuelezwa kwa kuwa Shirika lina pesa na Serikali inataka izichukue kidogo. Tunapokuja kwamba Shirika limetengeneza hasara, Waziri wa Sekta anampelekea Waziri wa Fedha ku-*approve*. Sasa hapo tatizo liko wapi?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaweza tukapiga kelele mpaka kesho hapa hatutoki, mradi ninyi hamkuleta hoja ya kufanya *amendment*, tunazungumza tu hapa. Mngekuwa mmeleta hoja, mtoa hoja huyu wa kufanya *amendments* angeungwa mkono na wenzake, Waziri angejibu, kama haturidhiki, tungepiga kura. Sasa hatuwezi kupiga kura kwa sababu hakuna hoja *substentive* ambayo ililetwa kwa mujibu wa Kanuni. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Blandes.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima zote nasimama kulisaidia tu Bunge lako kwenye Kamati. Kwa mujibu wa Kanuni ya 86, ikisomwa pamoja na Kanuni ya 84(3): Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi alitoa taarifa kuhusiana na maeneo ambayo Serikali na Kamati zilikuwa zimekubaliana. Moja ya eneo ni hili na ndiyo maana hata fursa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wangeliweza kuleta marekebisho, hawakuweza kuitumia kutokana na uelewano huo kwenye Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeliweza kusimama kutumia Kanuni ya 87(1), kuomba Muswada huu urejeshwe kwenye Kamati, lakini sikufanya hivyo kwa sababu naamini kwamba, maelewano ambayo yalikuwa yamefikiwa katika Kamati ya Fedha na Uchumi na Serikali katika maeneo haya, yangeliweza kutekelezwa kwa kufanyiwa marekebisho kama tulivyokuwa tumekubaliana. *(Makofi)*

Ndiyo maana tatizo la Waheshimiwa Wabunge sasa hivi tunaliona wazi kwamba, hawakutendewa haki. Kwa hiyo, mimi ningeliomba niishauri Serikali kwamba,

Mheshimiwa Ndugai amejenga hoja ya msingi sana, kwa jinsi kilivyoandikwa kifungu hicho cha kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukasema tu kwamba, yale maneno ya kumpelekea Waziri wa Fedha *for approval* tuyaondoe au iwe *of course to be submitted to the Minister for Finance.* Sasa yale ya pili, ule uwezo wake wa kutumia madaraka yake kiasi gani kibaki kwenye Shirika hilo au Taasisi yameelezwa na Wizara. Tunasubiri tuone hiyo Kanuni na miongozo ya Kiutawala ambayo Serikali imeahidi kutoa. Hilo lisipofanyika, maana hata Kanuni au kifungu chenyewe kilivyoandikwa, hakisemi kwamba Waziri wa Fedha atatoa miongozo hiyo. Tunataka tuiamini Serikali kwa maana hiyo, lakini Sheria ikipita kama ilivyo, haina hata hizo *guidelines* ambazo zinaachiwa sasa ziwe za kiutawala. Hiyo ndiyo sehemu ya tatizo ya Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara haina tatizo, kama tunaweza tukaishia pale *Minister response for Finance. (Makofi)*

Kwa kuongezea, pia nataka kukiri kwamba, tulikubaliana kwamba Waziri atatunga Kanuni na kwa kawaida Kanuni zinatungwa baada ya Sheria kupitishwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, lazima tukubaliane na aliyoyasema Mheshimiwa Chenge; ni sahihi tu kama mtu amekuja na *amendment* na kama Kamati ili-*assume* kule kwamba alivyosema ndiyo itakuwa kwenye *amendment schedule* hamna; sasa hiyo *assumption* ya kwenye Kamati inatoka wapi? Kwa sababu inasema Kamati ina uwezo wa kushauri tu na siyo kufanya mabadiliko, kama mnataka kufanya mabadiliko kuna kifungu kingine alichosema Mheshimiwa Chenge mwenyewe, wakati nilimwambia tukisoma hiki kifungu mtapata matatizo, anaweza mtu akasimama hapa akasema naomba Bunge liamue turudishe huu Muswada kwenye Kamati, inawezekana hapa na mimi sina namna nitasema ndiyo.

Mradi mlisema kule, sasa hapa ndivyo ilivyo, si kweli. Kwa hiyo, hata kama *you are right,* kama Waziri hataki kubadilisha hapa hatuna namna ya kufanya, maana ninyi hamkutoa taarifa ya hoja, wala hakuna hoja, mnazungumza tu hapa. Mnazungumza vizuri sana, lakini Kanuni hairuhusu. Kwa hiyo, Wabunge mmefanya kazi, ndiyo maana nawaambieni ya kuwa someni Kanuni, chukueni hatua. Kwa hiyo, tumshukuru Waziri amekubali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 29

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wepesi kabisa, kifungu hicho ningependekeza kama tulivyofanya kwenye ...

**MWENYEKITI:** Ishirini na nane mpya tunataka tuwe *very clear;* tuko wote, 29? *(Kicheko)*

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Kifungu hicho cha 28 Mheshimiwa Mwenyekiti kama mpya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Mlingwa hebu tupe utaratibu, unazungumzia kifungu gani?

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Kile cha 29 kipya kilichokuwa cha 30.

**MWENYEKITI:** *Okay* tuendelee.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Kwenye ile inayosomeka 10(a)(1) kama tulivyofanya kwenye 13(a)(1) ile sentensi ya kwanza mwisho isomeke *the Minister responsible for Finance.* *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, popote ambapo lipo neno hilo, nafikiri tunakubali kwamba litatolewa. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47

Ibara ya 48
Ibara ya 49

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 50
Ibara ya 51

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2008**
***(The Finance Bill, 2008)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imeupitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2008 *(The Finance Act, 2008),* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja marekebisho yake. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja itolewa imuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani wote wameafiki na kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha umepitishwa na Bunge lako Tukufu. Sasa nina maelezo machache; kuna wengi waliandika na kuuliza kwa nini Waziri hakuweza kuhitimisha hoja yake na akamwachia Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa mujibu wa Katiba, Naibu Waziri anaweza kumsaidia Waziri. Ibara ya 55(2), pamoja na Mawaziri waliotajwa katika ibara ndogo ya kwanza, Rais aweza baada ya

kushauriana na Waziri Mkuu, kuwateua Naibu Mawaziri. Naibu Mawaziri wote hawatakuwa Wajumbe wa Baraza, lakini kuna mahali wanasema *okay, number four;* Mawaziri na Manaibu Waziri wote watateuliwa kutoka miongoni mwa Wabunge. Hapana, kipo kifungu kinachosema, atamsaidia Waziri.

*No,* nilichojaribu kueleza hapa ni kwamba, Naibu Waziri alijibu badala ya Waziri na mwingine akasema kwani anaumwa. Mwingine hakuandika hata jina lake. Kufuatana na Kanuni zetu, hapana nimechanganya zipo kwenye Kanuni ya Bunge kwenye maelezo ya Kanuni zetu. 53 inamtaja Naibu Waziri. Hiyo inasema, Rais aweza nimesema.

Idadi yote ya Manaibu Waziri ambao watawasaidia Mawaziri katika utekelezaji wa kazi na shughuli zao. Kwa hiyo, Waziri hapa alimteua Waziri Msaidizi wake, amsaidie kujibu kwa sababu ya hitilafu iliyotokea. Kwa hiyo, hakuna baya lililotokea. *(Makofi)*

Yeye mwenyewe alitaka kujibu, lakini muda ulikuwa umekwisha. Kwa hiyo, hakuna tatizo lilitokea pale. La pili, nililokuwa napenda kulisema, Waheshimiwa Wabunge, tunakokwenda bila kutumia Kanuni jamani inaonekana ina-*sound* vizuri, hapana. Tutumie Kanuni, leo tumeingia kwenye kutunga Sheria.

Mkisoma ile sehemu yote ya utungaji wa sheria, Sura ya Nane inatueleza namna ya kutunga sheria. Maana mngeweza, mtu akasimama hapa, mnasema mnafika tena tunaomba Mheshimiwa Spika, Muswada huu uondoshwe.

Mimi sina budi kwa mfano, mnaosema mlikubaliana kwenye Kamati, Waziri hakusikiliza na ikithibitika kwamba Waziri hakusikiliza na mtu ametoa hoja kwamba, Muswada sasa uondolewe kwenye Kamati tulipo hapa, urudishwe tena huku. Nitaamua uondolewe kweli. Ndiyo maana nikasema Mawaziri mnajua *implications* za hii?

Kwa hiyo, Waheshimiwa mkisoma humu ndani hakuna mtu atakayekaa hapa bila usalama. Watu watakaa kwa salama humu ndani, lakini tukianza hivi tu haiwezekani.

Wabunge wote walikuwa na hoja, lakini wapi mlitoa taarifa kwamba, mnataka kuleta *amendment?* Kwa hiyo, ndiyo hivyo na inasema Kamati ina uwezo wa kumshauri Waziri tu, lakini haina uwezo wa kumbadilishia, sana sana ni ku-*loby* tu humu ndani kwamba tukifika mahali tuseme bwana Muswada huu urudishwe kwenye Kamati.

Spika, akiona inafaa anawaambia rudini kwenye Kamati na ukirudi kwenye Kamati ndiyo itabidi Waziri aanze upya.

Wakati huo huo, Mawaziri mnapofanya *amendments* zenu ni vizuri mkashirikiana na Kamati yenu, mkakubaliana kwamba yale yote mliyokubaliana ndiyo yanayokuja katika Meza hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa naomba tujifunze hiyo na Kanuni mzisome, kwa sababu tukienda bila kufuata Kanuni tutaona kazi yetu ni ngumu na nyinyi wenyewe mtaona kama mnaonewa, lakini kumbe hamkusoma Kanuni.

Baada ya kusema hivyo, nina tangazo moja tu kwamba, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Tafrija, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba, kesho tarehe 28 kutakuwa na tafrija ya kujipongeza baada ya kumaliza Mkutano wa Bunge la Bajeti. Tafrija hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Tafrija za Bunge hapo *Basement* kuanzia saa mbiliusiku. Kwa hiyo, Wabunge wote mnakaribishwa.

Baada ya tangazo hilo, napenda kuahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 02.15 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 28 Agosti, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*